# Nipashe

Jumanne Agosti 20, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580001

www.ippmedia.com

w.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Mahakama yasikiliza tepu, video kesi ya kina Mbowe

UKURASA 4




UKURASA 13

# Unyama mauaji ya kusikitisha

• **Wauaji** wadaiwa ndugu wa familia moja, wamuua shangazi, mtoto wake kisa... *Endelea ukurasa 2*




Baadhi ya daladala zikiwa ndani ya kituo cha Makole, jijini Dodoma jana, baada ya madereva wake kugoma kwa muda kutoa huduma ya usafirishaji abiria. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Hoteli, teksi kicheko SADC

UKURASA 3

## Mgomo daladala waathiri kazi kwa saa 6 Dodoma

UKURASA 2

**MICHEZO** ZAHERA AICHOMOLEA YANGA BETRI ARUSHA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Unyama mauaji ya kusikitisha

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia watu wanne, wakiwamo watatu wa familia moja, wakituhumiwa kuhusika na mauaji ya shangazi yao, Kalekwa Shiku.

Shiku (50), anadaiwa kuuawa kwa kupigwa kichwani na usoni kwa kitu chenye ncha kali na mtoto wake, Kuyonza Kubeja (30) kwa lengo la kurithi mali.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, akiongea na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, alidai mauaji hayo yalitokea Juni 18, mwaka huu katika Kitongoji cha Mwakundi, Kijiji cha Mishepo, Kata ya Mwantini wilayani Shinyanga Vijijini.

Kamanda Abwao alidai kuwa baada ya kuuawa, mwili wa Shiku ulitupwa kwenye bwawa ukiwa umefungwa kwenye kiroba.

Aliwataja wanaowashikilia kuwa ni ndugu watatu; Jumanne Kwangu, Daniel Kwangu na Emmanuel Kwangu, ambao alidai wote wamekiri kwa jeshi hilo kuhusika na mauaji hayo, huku akidai kuwa mtuhumiwa wa nne, Mihayo Ferdinand naye alikiri kuchukua ng'ombe tisa na kwamba tayari alishawauza wanne.

Kamanda Abwao alidai watuhumiwa hao baada ya kumuua Shiku, pia walishirikiana kumuua Kuyonza Kubeja, mtoto wa Shiku.

"Baada ya mahojiano kuhusu mauaji ya marehemu Kuyonza Kubeja, Agosti 8, mwaka huu, askari wa Jeshi la Polisi walion-doka na watuhumiwa Emanuel Kwangu na Jumanne Kwangu kwenda Mpanda mkoani Katavi walikomuua kijana huyo.

"Kijana huyo walimuua kwenye pori la Mlima Kasanga. Askari walifanikiwa kupata mabaki ya mifupa, nywele na meno ya marehemu," Kamanda Abwao alisema.

Alidai kuwa watuhumiwa baada ya kubanwa walikiri kuhusika na mauaji hayo kwa kuahidiwa kupewa Sh. milioni moja kwa kufanikisha mauaji ya shangazi yao na Sh. milioni 1.2 na ng'ombe tisa kama wangemuua na mtoto wake.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mishepo, Mashaka Alex, alidai kuwa baada ya kupewa taarifa za kuwapo kwa mwili binadamu uliotupwa kwenye bwawa waliuopoa na kuuzika, lakini baadaye walijitokeza ndugu waliowasimulia mkasa mzima na kuamua kufukua kisha kuuzika tena baada ya uchunguzi wa polisi.

"Baada ya kusikiliza maelezo ya ndugu zake, vijana waliotuhumiwa kuhusika na lile tukio tuliwaweka chini ya ulinzi wa sungusungu ambao ni ndugu wa familia moja na walipobanwa walikiri kumuua pia mtoto mkoani Katavi," Alex alidai.

Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa mikoa yenye idadi kubwa ya matukio ya mauaji, hasa ya wazee yanayoripotiwa kwa Jeshi la Polisi.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyantole, Jason Rwekaza (42), akifunika uso kukwepa kamera za waandishi wa habari, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma jana na kusomewa mashtaka ya kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa shule hiyo. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Mgomo daladala ulivyokwamisha shughuli kwa saa 6 jijini Dodoma

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHUGHULI mbalimbali jana zilisimama kwa zaidi ya saa sita jijini Dodoma, kutokana na mgomo wa madereva wa daladala kushinikiza kuondolewa kwa wafanyabiashara wadogo waliovamia kituo cha daladala Sabasaba kwa madai kuwa wamehodhi eneo kubwa na kuhatarisha usalama wao.

Nipashe ilishuhudia abiria wakiwa kwenye vituo mbalimbali wakisubiri usafiri hali iliyosababisha baadhi kuchelewa kazini.

Kutokana na hali hiyo, baadhi yao walilazimika kukodi pikipiki na bajaji ili kuwahi kufika kwenye maeneo yao ya kazi.

Mmoja wa abiria ambaye ni mkazi wa Chamwino Ikulu, Daudi Matonya, alisema mgomo umewaathiri na kusababisha kuchelewa kazini kwa kuwa usafiri huo umekuwa msaada kwa wananchi wengi.

Alisema ikitokea mgomo wa daladala huwaathiri, hivyo kuiomba serikali ichukue hatua za haraka kuondoa kero inayowasababisha kugoma.

Akizungumza mbele ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, Mwenyekiti wa Madereva hao, Shukuru Mushi, alisema wamefikia uamuzi huo kutokana na kuchoshwa na ongezeko la idadi ya wafanyabiashara hao kuendelea kuvamia kituo hicho.

"Hatupingani na uongozi wa jiji letu ila tunachopinga ni ongezeko la wafanyabiashara hawa ndani ya standi ya daladala hapa. Ukikanyaga nyanya za mtu hapa tunalipishwa tenga zima. Tumechoka na kero hii, Mkurugenzi tunaomba utusaidie," alisema.

Mushi alisema awali walikuwapo wafanyabiashara wachache lakini kwa sasa wameongezeka na wanapanga bidhaa chini kila eneo ndani ya kituo.

"Mbaya zaidi wachoma nyama na mahindi humu ndani wanatumia majiko yenye moto wa mkaa na wanayaweka karibu na magari yetu. Tukiwaambia kuwa ni hatari wanatuambia tuondoe magari yetu, tunaomba utusaidie moto huu utakuja kusababisha maafa humu ndani," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kutokana na hali ilivyo na maafa ya moto yaliyotokea mkoani Morogoro, ni hatari kwao kama eneo hilo litaendelea kuwa na matumizi holela ya moto.

Pia alisema kituo hicho kinahudumia zaidi ya daladala 2,500 kwa siku moja na hivi karibuni kuna mabasi makubwa yameongezeka yanayotoa huduma kutoka mjini kati kwenda mji wa Kiserikali Mtumba na Chamwino.

Alisema kutokana na msongamano huo umesababisha hivi karibuni dereva mwenzao kumgonga mwananchi mmoja ndani ya kituo na kuhukumiwa kifungo cha mwaka mmoja jela.

Naye Amina Ramadhani anayefanya biashara zake ndani ya kituo hicho, alisema ni kweli wanalazimika kufanya biashara ndani ya kituo hicho kutokana na kuwafuata wateja. Ramadhani alisema walianza wafanyabiashara wachache, lakini wameongezeka na kusababisha kufunga baadhi ya njia za daladala.

Kutokana na shinikizo hilo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Kunambi, aliagiza wafanyabiashara wenye matolori, wachoma nyama na mahindi na wengine wanaofanya biashara katikati ya kituo hicho, kuondoka mara moja ili kupisha magari.

"Najua kila mtu anahaki ya kutumia eneo hili, lakini kuna watu wamevamia mpaka katikati ya daladala. Ninawataka kuondoa biashara zenu humu, njooni mnione nitawafanyia utaratibu wa kupata maeneo mbadala," alisema.

Hata hivyo, aliagiza kuorodheshwa kwa majina ya wafanyabiashara wote ndani ya kituo hicho ili kupangiwa maeneo mengine ya kufanyia biashara.

# AfDB yaipa Tanzania bilioni 400/- za barabara

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeipatia serikali ya Tanzania Dola za Marekani milioni 180 (Sh. bilioni 414.07) kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa barabara ya njia nne, kuzunguka Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilometa 110.2 kwa kiwango cha lami.

Halfa ya utiaji saini wa mkopo huo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam, huku ilielezwa kuwa kukamilika kwa mradi huo kutaiwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji katika ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema kusainiwa kwa mkataba huo kutaongeza kiasi cha fedha ambazo zimetengwa na AfDB kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara nchini kutoka Dola za Marekani milioni 858.16 hadi Dola bilioni 1,038 (Sh. trilioni 2.39).

"Benki ya Maendeleo ya Afrika itaipatia serikali ya Tanzania mikopo yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 180, kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko, na uboreshaji wa miundombinu ya huduma za jamii katika Jiji la Dodoma," alisema James na kuongeza:

"Kupitia mkataba huu, Benki ya Maendeleo ya Afrika itatoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 138 kupitia dirisha la Benki ya Maendeleo ya Afrika, na Dola za Marekani milioni 42 zitatolewa kupitia mfuko wa Serikali ya China unaosimamiwa na AfDB."

Alisema AfDB pia imeonyesha utayari wa kufadhili ukarabati wa barabara ya Bagamoyo-Pangani-Tanga kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato, na kwamba maandalizi yameanza.

Alisema mradi wa ujenzi wa barabara hiyo utakapokamilika utaboresha huduma za usafirishaji katika mji wa Dodoma na kuchochea biashara ndani na nje ya nchi.

INAENDELEA UK.8

HABARI KITAIFA

# Korti yaelezwa mwalimu mkuu alivyodaiwa kubaka mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma, imemsomea maelezo ya awali Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyantole, Jason Rwekaza (42), ambaye anakabiliwa na makosa saba ya kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa shule hiyo.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Frola Mtarania, na kusomewa maelezo ya awali na mwendesha Mashtaka wa Serikali, Clement Masua.

Masua alidai kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kaulananga (jina linahifadhiwa), na kuwa alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi huyo kuanzia Mei mwaka 2017.

Mwendesha mashtaka huyo alidai zaidi kuwa mshtakiwa aliwahi kufanya mapenzi na mwanafunzi huyo mara saba.

Alisema mara ya kwanza mshtakiwa alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo tarehe isiyojulikana Mei mwaka 2017 katika maeneo ya Mlole Manispaa ya Kigoma/Ujiji na mara ya pili ni Juni 7, mwaka 2017 maeneo ya Mwandiga Wilaya ya Kigoma.

Wakili huyo aliendelea kuieleza mahakama kuwa mara ya tatu mshtakiwa alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo Agosti 16, mwaka 2017 maeneo ya Mwandiga Wilaya ya Kigoma na mara ya nne mshtakiwa alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo Machi 22, mwaka 2018 maeneo ya Bigabilo Wilaya ya Kigoma.

Alidai mshtakiwa alifanya mapenzi



na mwanafunzi huyo mara ya tano Julai 10, mwaka 2018 maeneo ya Bigabilo Wilaya ya Kigoma na mara ya sita alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo Februari 5, mwaka 2019 maeneo ya Kahabwa Manispaa ya Kigoma/Ujiji na mara ya saba mshtakiwa huyo alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo Februari 10, mwaka 2019 maeneo ya Kahabwa Manispaa ya Kigoma/Ujiji kisha kupata ujauzito.

Alidai kuwa baada ya uongozi wa Shule ya Sekondari ya Kaulananga kulifahamu tukio hilo, ulitoa taarifa kwa wazazi wa mwanafunzi huyo.

Kwamba Mei 31, mwaka 2019, tukio hilo liliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kati na polisi walifanya mahojiano na mwanafunzi huyo, kisha alimtaja mshtakiwa kuwa ndiye aliyempatia ujauzito na baadaye mshtakiwa alikamatwa na alipohojiwa kwenye maelezo ya onyo alikana.

Aliendelea kudai kuwa polisi walipomaliza upelelezi walimpeleka mshtakiwa huyo mahakamani.

Kwa mujibu wa Masua, upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mashahidi 10 na vielelezo viwili, na kuomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Thomas Msasa, uliomba mahakama kutoa amri ya kupima vinasaba (DNA), ili kuthibitisha kama mshtakiwa huyo ndiye aliyempa mwanafunzi huyo ujauzito.

Baada ya upande wa utetezi kutoa ombi hilo, Hakimu alisema wataendelea kusikiliza makosa ya kubaka, na siku ya hukumu hatalihusisha kosa la mimba mpaka watakapopima vinasaba.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 26, mwaka huu, kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi.

Mshtakiwa huyo huyo awali aliposomewa mashtaka dhidi yake alikana, na yuko nje kwa dhamana ya wadhamini wawili ambao walitoa barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata, na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tano kwa kila mdhamini.

# Idadi ya vifo ajali ya lori Moro yapaa

**Na Waandishi Wetu**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kufuatia ajali ya moto wa lori la mafuta mkoani Morogoro, imeongezeka na kufika 97 baada ya majeruhi wengine wawili kufariki dunia jana, wakati wakiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Majeruhi mmoja alifariki juzi mchana na mwingine jana alfajiri, hivyo kusababisha idadi ya wagonjwa waliosalia Muhimbili kuwa 18 kati ya majeruhi 47 waliopokelewa hospitalini hapo Agosti 10, mwaka huu. Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, aliwataja waliofariki dunia ni Rosijo Mollel (35) na Neema Chakachaka (30).

"Majeruhi wa ajali ya moto wamebaki 18 wote wapo katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) wakiendelea kupatiwa matibabu kwa hiyo kati ya wagonjwa 47 waliopokelewa 29 walifariki dunia," alisema Aligaesha.

Alisema Neema Chakacha alilazwa ICU jengo la wazazi alifariki dunia jana alfajiri wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Mkuu huyo wa mawasiliano alisisitiza watu kuendelea kuchangia damu kwa ajili ya majeruhi hao na wagonjwa wengine wenye uhitaji.

Idadi hiyo ya waliopoteza maisha inatokana na ajali ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli kuanguka eneo la Msamvu mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.

**Imeandikwa na Mary Geofrey na Agness Shayo**

# Wenye hoteli, teksi kicheko SADC

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUTANO wa 39 wa Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) umeacha kicheko kwa wamiliki wa hoteli, wafanyabiashara na madereva teksi jijini Dar es Salaam.

Wafanyabiashara hao wamesema walipata wateja wengi na kiwango kikubwa cha fedha wakati wa mkutano huo, tofauti na siku za nyuma ambazo kipato chao kilikuwa cha wastani.

Mkutano huo wa wakuu wa nchi 16 zinazounda jumuiya hiyo, ulifanyika kwa siku mbili kuanzia Jumamosi ukitanguliwa na shughuli mbalimbali zilizoanza Agosti 5, mwaka huu zilizodumu kwa wiki takriban mbili. Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, kuhusu fursa walizopata kutoka na mkutano huo, wamiliki wa hoteli na madereva taxi jijini, walisema wamevuna pesa za kutosha kwa kuwa katika kipindi chote hicho walikuwa wamejikita kuhudumia idadi kubwa ya wateja.

Meneja wa Hoteli ya Four Points by Sheraton Dar es Salaam (zamani New Africa Hotel), Augustine Baraza, alisema kwa muda wote ambao mkutano wa SADC ulikuwa unafanyika, walipokea wageni wengi hotelini hapo.

"Japokuwa hoteli yetu ni mpya, lakini tulipokea wageni wengi, wengine walikuja kulala na wengine walikuja kupata chakula, kwa kifupi tumenufaika sana na mkutano huu," Baraza alisema.

Meneja Mawasiliano na Masoko wa Hoteli ya Hyatt Regency Dar es Salaam (The Kilimanjaro), Lillian Kisasa, pia alisema hoteli yao imenufaika kwa kiasi kikubwa na mkutano huo.

"Ujio huo mkubwa sana kwa nchi, wakuu wa nchi takriban saba walilala hotelini kwetu, tumepeperusha vizuri bendera yetu ya Tanzania na kuipatia hoteli yetu hadhi ya kihistoria na kuongeza heshima iliyopo miaka yote," Kisasa alitamba.

Aliongeza kuwa mkutano wa SADC uliletea fursa mpya na kujenga urafiki mzuri na uaminifu kwa nchi ambazo zilikaa katika hoteli yao.

"Pia tumejifunza mtindo wa maisha wa nchi mbalimbali kwa kipindi kifupi hasa katika mpangilio mzima wa ratiba za kazi, ukarimu, mavazi na jinsi ya kuishi nje ya nyumbani," Kisasa alisema.

Msemaji wa Hoteli ya Southern Sun, Judith Mager, alisema: "Tumepokea wageni wengi sana kipindi cha mkutano wa SADC kwa sababu hoteli yetu ipo jirani na sehemu ambayo mkutano ulikuwa unafanyika, tumenufaika sana kusema ukweli."

Dereva teksi eneo la Posta jijini, Manase Joel, anayefanya kazi na kampuni ya Mbugani Safari, alisema kipindi chote cha mkutano huo alikuwa 'bize' kuhudumia wateja waliokuwa wanaingia na kutoka kwenye eneo ulikofanyika.

"Si haba, tumezikusanya kusanya, abiria walikuwa wengi, nilikuwa nawapeleka sehemu mbalimbali, kiukweli SADC imeninufaisha," Joel alisema.

Athuman Said, dereva taxi jijini, alisema aliwasafirisha abiria wawili waliotoka katika mkutano wa SADC kwa nyakati tofauti, mmoja akimpeleka Hoteli ya Tiffan na mwingine Hoteli ya Peacock na malipo yao yalikuwa makubwa.


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA BOSTON AUCTION MART, WAUNGWANA AUCTION MART AND JOSINA COMPANY LIMITED,**

Kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali lifuatalo:

| NAMBA | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MMILIKI DHAMANA | AINA YA DHAMANA | AUCTION COMPANY | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAMBA | TAGENDA/MOREGA,JUMA | MAKUNDI/PONSIAN,ODRICK | TOYOTA PRADO T944DKN | JOSINA AUCTION COMPANY | MWANZA | 30/08/2019 | SAA10:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 2 | PAMBA | CHACHA/SOLONGAI,CHACHA | CHACHA/SOLONGAI,CHACHA | NYUMBA | BOSTON AUCTION MARTS | MHANDU-MWANZA | 03/09/2019 | SAA10:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 3 | PAMBA | ATHANASE/DEUS, JOHN | ATHANASE/DEUS,JOHN | NYUMBA | BOSTON AUCTION MARTS | MKOLANI | 04/09/2019 | SAA10:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 4 | KIJITONYAMA | KAVISHE/ODRAN MARIANA | QUIRINE/OLIVERY,SHILIMA | NYUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | TEGETA WAZO MADALE | 04/09/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |
| 5 | TEMEKE | **SHABAANI,TATU** | AKIDA,SAIDI,ALLY | NYUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | YOMBO,VITUKA | 06/09/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |
| 6 | TEMEKE | SHOO MENYIOFORO,WILDARD | SHOO MENYIOFORO,WILDARD | TOYOTA PICK UP T 763ACX | WAUNGWANA AUCTION MART | TEMEKE YARD | 30/08/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |
| 7 | TEMEKE | KATEME/T,ANNA | KATEME/T,ANNA | NYUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MBAGARA MISSION | 07/9/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |
| 8 | TEMEKE | PANGANAS N LUBELI | PANGANAS N LUBELI | NYUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | CHANIKA | 13/9/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |
| 9 | KARIAKOO MKUNGUNI | KIMARIO/ADRIAN, ABIUD | KIMARIO/JOSEPH,SELESTIN | PREMIO T 704BEB | WAUNGWANA AUCTION MART | SINZA | 27/8/2019 | SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (nyundo itakaposhushwa) , salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.

i. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

ii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**Kwa mawasiliano:**

**Mratibu wa MIKOPO AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**

**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**

**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**

**Simu ya Dalali husika: +255768203040 JOSINA AUCTION COMPANY**

**+255766547732 BOSTON AUCTION MARTS**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215381302

KESI YA KINA MBOWE

# Mahakama yaangalia vielelezo picha za video

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, imeangalia picha za video wakati vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, anayedaiwa kuwataka wananchi walio tayari kwenda kuchukua vitambulisho vya mawakala ofisi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, Kinondoni.

Mbowe kupitia tepu na video iliyorekodiwa Februari 16, mwaka huu, wakati wakifunga kampeni ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kinondoni, alidai kuwa mawakala wao wameapishwa siku tano zilizopita, lakini bado hawajapokea vitambulisho vya kusimamia uchaguzi. Vielelezo hivyo video na tepu za tukio hilo, iliangaliwa jana katika ukumbi wa kituo cha mafunzo ya Mahakama iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi ya uchochezi dhidi ya vigogo tisa wa Chadema.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Dk. Zainabu Mango, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jaqline Nyantori.

Upande wa utetezi uliongozwa na Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, Jeremia Mtobesya na Hekima Mwasipu.

Shahidi wa sita Koplo Charles, aliiomba mahakama kutumia kamera ya video na tepu kuonyesha tukio la mkutano huo na mahakama ilikubali.

Mbali na washtakiwa, wabunge wengine wa Chadema waliohutubia mkutano huo ni, Peter Lijualikali, Sese Mwambe, Waitara Mwita, David Silinde, walionekana jukwaani kwa nyakati tofauti wakihutubia wananchi.

Washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa Zanzibar, Salim Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Katika picha hizo mahakamani, Msigwa akiwa ameshika vipaza sauti alisikika akisema: "Nimekuwa mteja wa polisi mara kadhaa, sheria za nchi hazituzuii mtu yeyote kutembea na panga, kisu, mkuki, rungu na mawe," alisikika.

Naye Mbowe akiwa ameshika vipaza sauti alisikika: "Uoga ni dhambi kwa Tanzania, Rais wa Afrika Kusini Jacob Zumo alilazimishwa kujiuzulu, Magufuli ni nani? Nimekaa naye bungeni zaidi ya miaka 15 kila mtu Magu, Magu mtu mmoja mfupi," alisikika na kuendelea:

"Dikteta wa Zimbabwe katolewa, Magufuli mwepesi kama karatasi, kiongozi wa kata ya Hananasifu yupo mochwari amekamatwa na vibaraka wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamemuua," alisikika Mbowe akihutubia wanachama wake.

Vile vile, Mbowe alisikika akihutubia kwamba mawakala wa Chadema bado hawajapewa vitambulisho vya kusimamia uchaguzi Februari 17, 2018.

Awali mahakama hiyo ilitupilia mbali pingamizi la utetezi na kukubali ombi la kukubali kuonyesha mahakamani tepu hizo.

Mapema mahakamani hapo, Koplo Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi, alidai kuwa alikimbilia kwenye gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Pia alidai mihemko hiyo ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya serikali.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuripoti mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika Viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video, ilipofika saa 10 jioni alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani, nilimsikia Mbowe akitoa kauli ya kufanya hamasa ya kuichukia serikali," alidai na kuongeza:

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Prof. Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka huu, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja hivyo wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16, mwaka huu, barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni Wilaya ya Kinondoni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya Ofisa wa Jeshi la Polisi, Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili, Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi, kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja hivyo kwenye mkutano wa hadhara mshtakiwa Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba, "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii... wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano...watu wanapotea...watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome...," alinukuliwa na kudaiwa kuwa maneno yaliyoelekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.




Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akisajili laini yake kwa kutumia alama za vidole katika banda la kampuni ya simu ya Tigo, katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi za SADC jijini Dar es Salaam juzi. Tigo ilikuwa mdhamini mkuu wa intaneti ya bure katika mkutano huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# CAG awapa vijana mbinu za mafanikio

**Na Moshi Lusonzo**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG), Prof. Mussa Asad, amesema uadilifu, hofu ya Mungu na kujiamini katika utendaji wa kazi ni baadhi ya mambo yanayomfanya mtu kuwa huru katika uwajibikaji kwenye maisha yake ya kila siku.

Prof. Asad ameyasema hayo jana wakati wa kongamano lililowakutanisha wanafunzi 450 kutoka mikoa mbalimbali nchini wanaotarajiwa kujiunga na vyuo vikuu. Alisema katika kuhakikisha taifa linapata watu wachapakazi na wanaojiamini, ni lazima vijana hao kuhakikisha wanakuwa na mambo hayo matatu ili kupata mafanikio.

Prof. Asad alisema katika hatua hiyo ya elimu kila kijana lazima ajisahihishe kutofanya makosa ya nyuma kwani muda huo umepita na badala yake wasome kwa bidii wakitambua wana jukumu zito katika jamii zao.

"Mtu anayejiamini ambaye hawi na shaka katika uwajibikaji wake ni yule anayezingatia kufanya kazi kwa uadilifu, kuwa na hofu ya Mungu na kujiamini kile anachokifanya kama anaamini kipo sahihi kwa jamii," alisema Prof. Asad.

Alisema anatambua katika kipindi hicho cha ujana kuna mambo mengi yanayowazunguka, lakini kama wakielewa umuhimu wao wa kwenda kulingana na muda pamoja na kuweka jitihada kwa kile wanachokifanya, watakuwa wameshinda ndoto zao.

"Tunajua mabadiliko ya teknolojia yaliyoendelea kwa sasa duniani. Hata hivyo, si kigezo cha vijana kujisahau katika mitandao ya kijamii, badala yake ni wakati mwafaka kuangalia namna ya kutumia katika kujiajiri na kutafuta fursa ya kujiinua kimapato," aliongeza kusema.

Mwenyekiti wa Vijana wa Taasisi ya An nahl Trust iliyoandaa kongamano hilo, Ally Mnondwa, alisema malengo ya mkusanyiko huo ni kuwapa vijana waliohitimu elimu ya kidato cha sita mbinu bora ya kutambua fursa zinazotokana na elimu ya chuo kikuu.

Alisema mikutano kama hiyo inafanyika kila mwaka na kushirikisha vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi.

# Serikali kuimarisha ukaguzi ubora elimu

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amekabidhi magari 30 kwa maofisa elimu mkoa kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu nchini.

Akikabidhi magari hayo jijini Dar es Salaam jana, Jafo aliagiza magari hayo aina ya Toyota Land Cruiser yatumiwe na maofisa elimu wa mikoa 26 na mengine manne kwa ajili ya Idara ya Elimu Tamisemi kufuatilia maendeleo ya elimu nchini.

Alisema gharama za kununua magari hayo ni Sh. bilioni 2.72 (Sh. milioni 72 kwa kila gari), akieleza kuwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kuboresha sekta hiyo muhimu.

"Ili kufanikisha suala la uboreshaji wa elimu nchini, tulianza na mkakati wa kukarabati shule kongwe na hadi sasa, jumla ya shule 62 zimefanyiwa ukarabati kati ya 89 za awamu ya kwanza na leo ninawakabidhi maofisa elimu 26, magari yenu ya kutembelea kwa ajili ya kufanya ukaguzi katika shule zenu," Jafo alisema.

Aliongeza kuwa serikali imejibu kilio cha maofisa hao ambao hawakuwa na usafiri na badala yake walikuwa wakidandia magari ya viongozi wengine, changomoto ambayo ilisababisha washindwe kutembelea shule zote.

Jafo pia aliwaagiza maofisa hao kuhakikisha wanafuatilia na kusimamia ukarabati wa magari yao ili yasichakae mapema.

HABARI KITAIFA

# Mahakama yawafutia kesi vigogo wa TPDC

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewaondolea kesi ya matumizi mabaya ya madaraka dhidi ya vigogo watano wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), akiwamo Mkurugenzi Mtendaji James Mataragio baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuona hana nia ya kuendelea kuwashtaki.

DPP kupitia Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, amewasilisha hati ya Nole kwamba anaiomba mahakama kuiondoa kesi hiyo chini ya kifungu cha 91 kidogo cha (1) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kwamba hana nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Wankyo alidai kuwa hati hiyo imewasilishwa Julai 10, mwaka huu, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kevini Mhina. Wakili wa utetezi, Emmanuel Makene, alidai kuwa hana pingamizi na maombi ya Jamhuri.

Hakimu Mhina alisema kwa kuwa DPP amewasilisha maombi ya kuwaondolea mashtaka washtakiwa, mahakama yake imekubali kuwaondolewa chini ya kifungu cha 91 kidogo cha (1) cha CPA.

Mbali na Mataragio, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Kaimu Meneja wa Uvumbuzi, George Seni, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Utawala, Wellington Hudson, Mkurugenzi wa Mkondo wa Juu, Kelvin Komba na Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Edwin Riwa.

Hata hivyo, wakati kesi hiyo inaondolewa mahakamani hapo, Mataragio hakuwapo kusikiliza kesi yake.

Katika kesi ya msingi, Mataragio na wenzake walikuwa wanadaiwa kuwa wametenda kosa hilo kati ya Aprili 8, 2015 na Juni 3, 2016. Inadaiwa wakiwa watumishi wa umma na waajiriwa wa TPDC kwa nafasi zao, wakati wakitimiza majukumu yao kwa makusudi walitumia madaraka vibaya.

Inadaiwa kuwa washtakiwa walibadilisha na kupitisha bajeti na mpango wa mwaka wa manunuzi wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016 kwa kuingiza ununuzi wa kifaa cha utafiti cha airborne gravity gradiometer survey ndani ya Ziwa Tanganyika bila ya kupata kibali cha bodi ya wakurugenzi ya shirika.

Inadaiwa kitendo hicho kinakiuka kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kwa lengo la kujipatia manufaa yasiyo halali ya Dola za Marekani 3,238,986.50 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 7.2 kwa Bell Geospace.

Washtakiwa waliposomewa mashtaka yao walikana kwa nyakati tofauti na walikuwa nje kwa dhamana.



Mwandishi wa Habari, Erick Kabendera akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayomkabili kuahirishwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Uchunguzi kesi ya Kabendera haujakamilika

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha zaidi ya Sh. milioni 100 inayomkabili mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustino Mmbando, baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, aliyepangiwa kuwa na udhuru wa kikazi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini upelelezi wake bado haujakamilika.

Wakili wa utetezi, Jebrah Kambole, alidai kuwa wanaomba Jamhuri kuharakisha upelelezi kwa sababu mshtakiwa anakabiliwa na tuhuma ambazo hazina dhamana.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Agosti 30, 2019.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019 katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173, 247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Katika shtaka la tatu mshtakiwa anadaiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

# Yetu Microfinance yapigia debe elimu kuhusu hisa

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya Yetu Microfinance imesema bado kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi hususani wajasiriamali wadogo kuhusiana na elimu ya hisa ili wafahamu namna ya kunufaika na hisa hizo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Altemius Millinga, katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa wanahisa wake uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Kwa sababu sisi tunadili na wananchi wa hali ya chini, wengi elimu yao siyo kubwa kwa hiyo hata elimu ya hisa wengi wao hawana, bado hawafahamu ni namna gani anaweza kununua hisa kiwango gani ambacho kitampatia faida," alisema Millinga na kuongeza:

"Dhana nzima ya suala la hisa ni kizungumkuti kwa wanahisa wengi hasa katika benki kama hizi za kwetu, tunapambana sana kuwaondoa Watanzania katika hali ya umaskini, lakini pia tunahitaji kuwa na nguvu kubwa ya kuendelea kuwaelimisha katika mambo muhimu yatakayowasaidia kuwatoa katika shida hiyo na elimu ya hisa nayo ikiwamo."

Alisema lengo kubwa ni kuwasaidia wananchi ambao hawana sifa za kukopa katika benki nyingine ili kuanzisha miradi yao na kujitegemea.

"Hawa ni wananchi ambao wakienda kukopa katika benki nyingine wanakosa sifa, kwa hiyo sisi huwa tunafanya kazi ya kuwaunganisha kwenye vikundi vya biashara ili kuwapa mkopo waweze kujiajiri."

Alisema kwa sasa wamefikia hatua ya kuwahudumia wakulima wadogo kwa kuwapatia mikopo midogo kwa kutumia dhamana mbadala.

"Mabenki mengi mikopo yao huwa ni mikubwa, lakini sisi mkulima akihitaji kukopa hata Sh.600,000 ambayo hawezi kupata katika benki nyingine, sisi tunamkopesha kwa kutumia dhamana mbadala," alisema Millinga.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Asasi sasa ziisikie serikali

**SERIKALI** imetangaza orodha ya asasi za kiraia (NGO), zilizofutwa kutoka kwenye daftari la usajili kutokana na mabadiliko ya kisheria. Asasi hizo zilisajiliwa kwa sheria namba 24 ya mwaka 2002 na sasa zinawajibika kusajiliwa upya kwa kutumia sheria namba 3 ya mwaka 2019.

Tunapongeza nia ya serikali kwa kusimamia kazi na shughuli za asasi hizo za kiraia ambazo zimekuwa nguzo katika kupambana na umaskini nchini zikijuhusisha na masuala ya elimu, afya, kilimo, uwekezaji na utetezi wa wanawake na watoto.

Tunazikumbusha NGO kuwa hata hivyo licha ya kuwapo na maelezo kuwa asasi hizo zinasaidia juhudi za kuondoa umaskini, kuna madai mengine kuwa kuna mambo ambayo yanalalamikiwa.

Haya ni pamoja na kuwa wapo baadhi ya wahusika kwenye asasi hizo licha ya kupokea mamilioni ya dola hawazitumii kuwawanufaisha wananchi na badala yake wanajinufaisha wenyewe na si kuwaletea wananchi kile kilichotarajiwa.

Ndiyo maana wakati mwingine sheria zimetaka kupata taarifa za fedha na pia kuwaonyesha wasajili taarifa za mashirika hayo zilizohuishwa kabla ya kupata usajili mpya unaoambatana na Sheria namba 3 ya 2019.

Aidha, wakati kuna ukosoaji huo tunaona kuwa kuna haja ya NGO kuzingatia maelekezo ya serikali kwani kuna baadhi ya mijadala sehemu mbalimbali duniani inayosema kuwa asasi hizo zinaongozwa na sera za Kiliberali.

Uliberali unaamini kuwa vikundi vya wahamasishaji vikiwamo asasi za kiraia vinafanyakazi nzuri zaidi katika kutoa huduma badala ya serikali zikiwamo za Afrika hivyo kuzipuuza serikali zao.

Halikadhalika kuna ukosoaji kuwa asasi hizo zinawajibika zaidi kwa wahisani wanaozipa fedha kuliko serikali au wananchi wanaowahudumia kwa vile lengo la taasisi hizo ni kupata fedha kutoka kwa wahisani hao na kwamba miradi zinazoifanya inakidhi na kulinda matakwa ya wale wanaotoa fedha na wakati mwingine hazijali hali halisi.

Cha msingi kinabaki kuwa hakuna wa kupinga umuhimu wa NGO ndani ya jamii. Serikali haiwezi kufanya vitu vyote pekee yake bila kuungwa mkono na wadau wengine kama asasi za kiraia, mashirika ya dini na sekta binafsi.

Azaki zimefikisha maji vijijini, umeme jua, huduma za afya kusaidia wenye magonjwa, zimekemea maovu kama mila potofu vijijini, ikiwamo kuoza watoto na daima zinashirikiana na serikali kuwaendeleza Watanzania.

Kwa kifupi hakuna taifa lisilokuwa na mashirika ya kiraia na Tanzania inaendelea kuyahitaji na mchango wake ni muhimu mno. Tunakubaliana wote kuwa kila jambo linasimamiwa na sera na sheria.

Kwa hiyo asasi hizo zina nafasi ya kipekee na ya muhimu. Hakuna sababu ya kuchezea fursa hiyo ya kujisajili upya hasa kwa hizo zilizoondolewa kwenye daftari la msajili.

Azaki zimesikia kuwa baada ya kukamilika kwa zoezi la usajili serikali itatoa tena nafasi ya kujiandikisha katika kipindi cha miezi mitatu.

Wale ambao hawatafanya hivyo watafutwa usajili na hakutakuwa na kibali cha kufanyakazi zake.

Tunazishauri taasisi hizi kushirikiana na serikali katika kuwekeza na kuendeleza huduma za kijamii zinazotolewa na taasisi hizo muhimu, kwa kukubali kujisajili kwa mujibu wa sharia mpya.

Itoshe kusema kuwa asasi hizi zimefanya kazi kubwa kulinda, kujenga na kutetea jamii ni vyema kuendeleza ushirikiano na serikali katika azma nzima ya kuwatumikia wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Serikali iendeshe operesheni ya kusomba pamba ya wakulima

Na Raphael Kibiriti

**NIANZE** kama Mtanzania kuipongeza serikali kwa kufanikisha kwa kishindo Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), uliohitimishwa juzi jijini Dar es Salaam.

Ni bayana kwamba mkutano huo umeongeza alama kwa taifa na hasa baada ya lugha adhimu ya Kiswahili kupitishwa kuwa miongoni mwa lugha rasmi nne zinazotumika SADC, zikiwamo za Kingereza, Kifaransa na Kireno.

Lakini pia umeongeza alama kwa nchi baada ya Rais John Magufuli kuchukua mikoba ya uongozi wa Jumuiya kutoka kwa Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob.

Nimeona leo niendeleze ajenda ya ununuzi wa pamba ya wakulima, kwani bado utatuzi wake haujawa katika kiwango cha kuridhisha.

Hali iko hivyo kwa mujibu wa taarifa alizonazo Muungwana kutoka maeneo mbalimbali yanayolima pamba, hasa Kanda ya Ziwa pamoja na ahadi aliyoitoa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwenye sherehe za Nanenane.

Akiwa kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Nanenane kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, Agosti 8, Majaliwa aliwahakikishia wakulima wa zao hilo kuwa pamba yote itanunuliwa na kuondoka mikononi mwao.

Aidha, akazitaka benki zote zinazotoa fedha kwa kampuni za ununuzi kutoa taarifa kwa serikali kiasi cha fedha walizotoa kuwawezesha wakuu wa mikoa na wilaya kuweka mikakati ya usimamizi ili fedha hizo zipelekwe kwenye ununuzi wa zao hilo na si vinginevyo.

Nia ya maelekezo hayo kwa mujibu wa Majaliwa ni kuhakikisha pamba yote inatoka mikononi mwa wakulima, wanapata fedha zao na hatimaye wajiandae kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo na maboresho ya shughuli zao za kimaendeleo.

Hata hivyo, ikiwa ni takribani wiki mbili sasa toka maagizo hayo yatolewe, bado hali kwenye vyama vingi vya msingi vya ushirika (AMCOS), iko vilevile.

Bado maghala ya AMCOS yamejaa huku pamba nyingine ikiwa imehifadhiwa nje na hasa katika mikoa ya Simiyu na Shinyanga. Bado wakulima walio wengi waliopeleka pamba yao kwenye maghala ya AMCOS, hawajalipwa fedha zao.

Maagizo ya serikali kwamba pamba hiyo iwe imesafirishwa kwenda viwandani ili nafasi ya kuhifadhi pamba ambayo bado iko mikononi mwa wakulima ipatikane, hayajatekelezwa.

Muungwana ana taarifa kwamba bado kampuni za ununuzi hazijapeleka magari ya kusomba pamba, kutoka kwenye maghala ya AMCOS hadi sasa.

Aidha, taarifa zinabainisha kwamba kuchelewa kwa wanunuzi wa zao hilo kutekeleza agizo la serikali pengine linatokana na ukweli kwamba baadhi ya wakulima waliamua kuingia gharama za kupeleka wenyewe pamba kwenye viwanda ili ikanunuliwe.

Na ndiyo maana kwa mfano maghala ya viwanda vya pamba vilivyoko Shinyanga, yalikuwa yamejaa kiasi cha nyingine kuwekwa nje.

Hatua hii ya wakulima kuamua kupeleka pamba yao wenyewe kwenye viwanda bila ya kupitia AMCOS, kimsingi ndiyo ambayo imesababisha hata agizo la serikali la kusomba pamba kutoka AMCOS lisitekelezwe kwa kiwango kikubwa.

Kwamba kampuni za ununuzi hazikuona kwa nini ziingie gharama za kupeleka magari ya kusomba pamba, wakati wakulima wenyewe wanaipeleka katika viwanda vyao.

Ni vyema kwamba Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Tellack, ameiona dosari hii na akapiga marufuku pamba kununuliwa viwandani, badala ya AMCOS.

Kwa kuwa siku zinazidi kusonga mbele na matayarisho kwa ajili ya msimu ujao yanakaribia, Muungwana ana ushauri kwa serikali kwamba iendeshe operesheni toa pamba kwa wakulima, kama ilifanya kwenye zao la korosho.

Muungwana anashauri hilo ili kuwezesha pamba yote iliyoko kwa wakulima iondoke mikononi mwao kama ilivyoelekezwa na Waziri Mkuu.

Aidha, sambamba na hilo anashauri nguvu ya ziada itumike ili kwamba wakulima ambao tayari wana pamba yao kwenye maghala ya AMCOS, walipwe fedha zao.

Hii ni kwa sababu hadi sasa shughuli ya kuwalipa haki yao hiyo inasuasua pamoja na maagizo ya Waziri Mkuu.

# BARUA & MJADALA

## Tuwapige vita wachafuzi hawa Tandale

***Mhariri habari***

*NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lilili na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.*

*Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisaidia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.*

*Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.*

*Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.*

*Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.*

***Mwathirika - Tandale***

## Walezi tusifuge tabia zisizokubalika

***Mhariri***

*KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao kwa kiasi kikubwa hawako tayari kusikiliza ushauri wanaopewa na majirani zao juu ya tabia za watoto wao.*

*Katika mtaa ninaoishi hapa Mbalizi mkoani Mbeya, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya wastaarabu na hata katika mwenendo wa kawaida wa maisha ya watu.*

*Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu. Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.*

*Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.*

***Issa Mwambungu- Mbalizi***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Ibuniwe njia thabiti kuondoa kero usafiri kwa wanafunzi

**Na Sabato Kasika**

**TATIZO** la ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za jijini Dar es Salaam, ni changamoto kubwa inayosababisha wachelewe vipindi shuleni, lakini pia wakati wanaporudi nyumbani jioni.

Hii inatokana na tabia ya baadhi ya makondakta na madereva wa daladala ya kuwazuia kupanda magari hayo kana kwamba hawana haki ya kutumia usafiri huo wa umma.

Changamoto hiyo ni muda mrefu, na imekuwa ikipigiwa kelele na wadau mbalimbali wa elimu, ingawa ni kama ufumbuzi wake haujapatikana, kwani wanaendelea kuachwa vituoni.

Ninatambua jitihada zilizofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, wakati huo, Paul Makonda kwa walimu wa shule za umma za msingi na sekondari kwa kubuni njia ya kuwawezesha kusafiri bure katika magari hayo.

Makonda alifanya hivyo kwa kushirikiana na wamiliki wa vyombo vya usafiri Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa elimu bure na shukrani kwa walimu.

Walimu walianza kusafiri bure tangu Machi mwaka 2016.

Kimsingi hatua hiyo ya walimu kusafiri bure ni moja ya mipango ya kimaendeleo inayogusa uboreshaji wa sekta ya elimu ikiwamo kufuta ada zote shuleni ingawa suala la walimu kusafiri liko katika jiji la Dar es Salaam tu.

**Vilevile ieleweke kwamba kupata wasomi wazuri wa baadaye, kunaanzia katika kupunguza kero kwa wanafunzi zikiwamo hizo za usafiri, ambazo zimekuwa zikisababisha wachelewe kufika shule kwa wakati.**

Kwa mujibu wa Makonda, wazo la usafiri bure kwa walimu limejengwa juu ya msingi wenye sababu kuu tatu ikiwamo ya kuzingatia changamoto za nauli za mara kwa mara wanazolazimika kuzilipa ili kufika kwa wakati kazini.

Msingi wa pili ni kuhakikisha serikali inakuwa sehemu ya juhudi za kuboresha maslahi na mazingira ya walimu ya kufanyia kazi ili kuhakikisha lengo la kukua kwa sekta ya elimu linatimia.

Na ya tatu ni kuwafanya walimu kama watumishi wa serikali wafaidi sehemu ya matunda ya serikali yao ambayo imedhamiria kubadilisha maisha yao ili nao waweze kubadilisha maisha ya wanafunzi kupitia taaluma.

Lakini pamoja na nia njema hiyo kwa walimu, ninadhani kuna haja ya kupiga hatua mbele katika suala hili la usafiri kwa kuwagusa zaidi wanafunzi, ambao wamekuwa wakikutana na changamoto nyingi.

Hata hivyo suala la walimu kutolewa, unyanyasaji kwa wanafunzi unaofanywa na baadhi ya makondakta na madereva wa daladala kwa kuwazuia kupanda katika magari yao unasababisha wachelewe kufika shuleni au kurudi nyumbani.

Mtindo huo ni muda wa mrefu na huwafanya baadhi ya wanafunzi kuomba lifti kwa magari ya watu binafsi ili wawahi shule na hivyo kwa wakike kujikuta wakirubuniwa na wakwale ili wajiingize katika mahusiano ya kingono.

Mazingira ya aina hiyo kwa mwanafunzi wa kike si rafiki, zaidi sana ni kumharibia ndoto zake za baadaye kwa kumpa mimba.

Na ndiyo maana mjadala unashauri zikatafutwa njia za kuwasaidia wanafunzi kupata usafiri bila usumbufu.

Hivyo basi badala ya ubunifu kuishia kwa walimu, basi ungepanuliwa hadi kwa wanafunzi na ikiwezekana vituo vya daladala viwe na askari wa usalama barabarani atakayehakikisha kila daladala inachukua wanafunzi.

Hapa nina maana kwamba kwanza ufanyike utafiti ili kubaini vituo vya daladala ambavyo wanafunzi husafiri kwa wingi, kisha wawekwe trafiki kusimamia zoezi la kuwapakia katika daladala hizo.

Nauli inayotozwa ya Sh. 200 ndio haki yao na waendelee kuilipa bila kunyanyaswa.


Vilevile ieleweke kwamba kupata wasomi wazuri wa baadaye, kunaanzia katika kupunguza kero kwa wanafunzi zikiwamo hizo za usafiri, ambazo zimekuwa zikisababisha wachelewe kufika shule kwa wakati.

Ninasema hivyo kwa sababu baadhi ya makondakta wamekuwa wakiwaacha wanafunzi vituoni kwa kisingizio kwamba nafasi zao zimejaa, kumbe wanawakwepa ili kubeba watu wazima tu.

Bila kubuni njia mwafaka, wanafunzi wataendelea kutokuwa na uhakika wa kufika shuleni mapema kuwahi vipindi au kurudi nyumbani kwa wakati hasa muda wa jioni, kwasababu tu ya ukorofi wa watu wachache.

Kama ni suala la kubeba wanafunzi, nina uhakika makondakta na madereva wa daladala walishaelekezwa, lakini wapo wachache wasiotaka kuwachukua eti kwa sababu nauli zao ni ndogo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Mzumbe yasaidia majeruhi wa ajali Moro kwa mil. 6/-

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Mzumbe Kampasi Kuu ya Morogoro, imekabidhi misaada ya vifaa tiba kwa ajili ya majeruhi wa ajali ya moto iliyotokea mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu na kusababisha vifo vya watu 95.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo; Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, alisema jana kuwa Jumuiya ya Chuo Kikuu Mzumbe wamechangia vifaa tiba vya thamani ya Sh. 6,343,000- vikijumuisha dawa, sindano, dripu, gozi za vidonda, dawa za maumivu, maji, taulo za kike na dawa nyingine baada ya kuonekana uhitaji mkubwa wa vifaa hivyo kufuatia hali ya majeruhi na matibabu wanayoendelea kupatiwa kwenye hospitali hiyo.

"Vifaa tunavyokabidhi ni michango ya watumishi, wanafunzi na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa kuwa na sisi tumeguswa na tukio hili, ni sehemu ya wananchi wa Morogoro, hivyo hatunabudi kujitoa kwa hali na mali kuokoa maisha ya wenzetu. Tunatamani kuona majeruhi wa ajali hii wanatibiwa na kurejea kwenye afya zao," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo; Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, alisema; serikali ya mkoa imefarijika sana kwa namna chuo hicho kilivyojitoa tangu ajali hiyo ilipotokea kwa msaada wa haraka wa gari la wagonjwa kuwakimbiza Hospitali ya Taifa Muhimbili na walivyojitoa kuchangia damu kabla ya msaada wa vifaa walivyokabidhi leo.

"Tunawashukuru sana uongozi na wafanyakazi wa chuo kwa michango yenu kwa hakika haitawasaidia majeruhi wa ajali hii tu, lakini na wagonjwa wengine wenye uhitaji na hasa kwa kuzingatia mkoa wetu uko katikati na hivyo kuwekuwa na majeruhi wengi wa ajali ambao wanahitaji msaada wa haraka wanapofikwa na majanga kama haya," alisisitiza.

Aliwataka kuendelea kujitoa kwa wananchi wa Morogoro kila inapobidi kufanya hivyo kwa kuwa uwapo wao ni muhimu sana katika ustawi na maendeleo ya wananchi.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Kusirya Ukio, alieleza hali ya majeruhi wa ajali ya moto ambapo hadi kufikia jana idadi yao ni 17 wakiendelea na matibabu katika Hospitali ya Mkoa na kati yao, baadhi wameanza kufanya mazoezi. Hata hivyo, matibabu yao bado yatachukua muda mrefu kutokana na aina ya majeraha waliyoyapata, hivyo misaada bado inahitajika vikiwamo vifaa tiba.




Mchuuzi wa ndizi na viazi, akiwa amepanga bidhaa zake kando ya jalala la takataka, nje ya soko la ndizi Mabibo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wa afya yake na wateja. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# AfDB yaipa Tanzania bilioni 400/- za barabara

INATOKA UK. 2

"Barabara hii inaunga na barabara ya Cape Town hadi Cairo inayojulikana kama The Great Road Highway inayopitia katika nchi za Afrika Kusini, Zimbabwe, Zambia, Kenya, Ethiopia, Sudan na Misri, na barabara ya ushorobo wa kati inayounganisha Tanzania na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Rwanda na Uganda."

James alisema ujenzi wa barabara hiyo utaanznia eneo la Nala-Veyula-Ihumwa-Matumbuli hadi Nala, pia uboreshaji wa miundombinu ya huduma za kijamii kama vile maji, vituo vya afya, ukarabati wa barabara za mchepuko na utekelezaji wa mikakati ya usalama wa barabarani.

Naye Meneja wa AfDB Tanzania, Alex Mubiru, alisema mradi huo utaboresha usafirishaji katika mji wa Dodoma, itakuza uchumi wa nchi.

Wakati huo huo, Wizara ya Fedha na Mipango imeipatia Halmashauri ya Mji wa Nzega Sh. bilioni 4.216 kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi, baada ya kusaini mkataba.

Katiku Mkuu wa Wizara hiyo, Doto James, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 284 kwa ajili ya kuzipati halmashauri zitakazoandika andiko la mradi utakaoingizia fedha.

"Masharti ya kupata fedha hizi ni halmashauri iwe na uwezo wa kukusanya mapato ya kutosha, waweze kujiendesha wenyewe bila ya kuitegemea serikali," alisema James.

Alisema kwa mwaka 2018/19 halmashauri 17 zilipata Sh. bilioni 131.5, mwaka 2017/18 halmashauri 12 zilipewa Sh. bilioni 137 kwa kuandika andika la miradi 15.

# Waliofadhiliwa masomo Uingereza wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amewataka watumishi wa wizara hiyo waliopatiwa ufadhili wa masomo na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo (DFID) katika vyuo vikuu vya nchi hiyo kusoma kwa bidii ili kuja kulitumikia taifa kwa umahili zaidi katika nyanja za uchumi na uchambuzi wa masuala ya fedha.

Alisema hayo jana wakati wa hafla ya kuwaaga watumishi watano wa wizara hiyo, waliopata udhamini huo, iliyofanyika katika ofisi za British Council- Tanzania, jijini Dar es Salaam.

Dk. Mpango (pichani) alisema miaka miwili iliyopita aliiomba Serikali ya Uingereza kupitia DFID, wasaidie kusomesha watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango kwenye vyuo vikuu vya Uingereza, kwa kuwa Wizara ya Fedha katika nchi yoyote ndio nguvu ya fikra katika uchumi, hivyo bila watumishi wenye ujuzi kutakuwa na wizara dhaifu.

"Ninawasisitiza sana vijana waliopata fursa ya kwenda kusoma Uingereza, wajue dhamana wanayokwenda nayo, Watanzania takribani milioni 50 wanaimani nao, wanamatarajio kwamba watakapokwenda huko watazingatia kusoma kwa bidii, ili wakirudi wawe wataalamu waliobobea katika masuala ya uchumi na uchambuzi wa masuala yote ya fedha ndani ya wizara," alieleza Dk. Mpango.

Alisema pamoja na kuiomba Serikali ya Uingereza kutoa mafunzo kwa vijana hao, aliwaomba pia iwapatie mafunzo kwa vitendo katika taasisi zinazojihusisha na masuala ya uchumi na fedha nchini humo ili wapate uzoefu.



Alisema anaishukuru Serikali ya Uingereza kwa kukubali ombi hilo na sasa ni timu ya tatu kupelekwa masomoni, awamu ya kwanza na ya pili walipelekwa jumla ya vijana kumi, na sasa tumewaaga rasmi watumishi watano ambao wataenda mwezi ujao na kufikisha idadi ya watumishi 15.

Amewataka watumishi hao wakaitangaze vizuri Tanzania na wakirudi waje kuitumikia Tanzania ili taifa lipate maendeleo yanayotarajiwa baada ya hatua hiyo muhimu ya kuwekeza kwa vijana Watanzania katika kupata ujuzi.

Mkuu wa DFID, Beth Arthy, alisema kuwa tangu mpango huo uanze Serikali yake imekwisha wasomesha wanafunzi kumi katika fani za uchumi na uchambuzi wa masuala ya fedha na idadi ya watumishi watano watakao kwenda kusoma nchini humo itafikisha idadi ya watumishi 15.


**CHAMPION AUCTION MART**

**NOTISI / MNADA**

KWA NIABA YA **UNITY 3E SOLUTION (T) LTD** MWANZA, TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIOTAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA KWA MUDA MREFU.

ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA, DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KWA RATIBA IFUATAYO:-

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | JOEL MANUSA | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO. IGOMA-MWANZA (IGOMA MASHARIKI) | 03/09/2019 SAA 5 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**
A. UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
B. MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TU.
C. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPASALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE NA NYUMBA ITAUZWA TENA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA. 0759 290628 / 0753 959568 / 0755 244442**

HABARI KITAIFA

# Mkoa wa Mara washika mkia usafi wa vyoo

Na Ada Ouko, BUNDA

MKOA wa Mara umetajwa kushika nafasi ya 24 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara ikifuatiwa na mikoa ya Lindi na Kigoma ambayo inatekeleza usafi duni wa mazingira, ujenzi wa vyoo bora na kuvitumia ipasavyo hali inayosadikiwa kusababisha kutokea kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, homa ya matumbo na kuhara.

Hayo yalibainishwa jana wilayani Bunda, mkoani hapa na mratibu taifa wa kampeni ya nyumba ni choo, Anyitike Mwakitalima, ambaye alisema katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mara una asilimia 46.6 ya kaya zenye vyoo bora, huku watu wanaoishi vijijini ndio wanaofikiriwa kuwa kwenye hatari kubwa zaidi ya kupata magonjwa hayo yatokanayo na uchafu wa mazingira.

Kampeni hiyo ya uhamasishaji ujenzi wa vyoo bora yenye kaulimbiu 'Usichukulie poa nyumba ni choo' inatekelezwa nchini na inaoongozwa na msanii Mrisho Mpoto na timu yake na katika Mkoa wa Mara ilizinduliwa rasmi Julai 28, Manispaa ya Musoma na ilifungwa Agosti 18, wilayani hapa.

**Kwa kipindi cha Aprili hadi Juni, mwaka huu, takwimu zinaonyesha kuwa kaya zenye vyoo bora ni 31,725 ambazo ni sawa na asilimia 57 kati ya kaya 55,702 na 2,239 sawa na asilimia nne hazina vyoo.**

Awali wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo mjini Musoma, Ofisa Afya wa Mkoa wa Mara, Bumija Mhando, alisema asilimia 93 ya wananchi mkoa huo wanaongoza kwa kutokuwa na vyoo bora na zaidi ya kaya 22,700 sawa na asilimia saba ya makazi ya watu hawana choo kabisa, huku asilimia 94 ya wananchi wameelezwa kutokunawa mikono kila wanapotoka chooni kujisaidia.

"Takwimu zinaonyesha ni asilimia sita pekee ya wananchi wa Mkoa wa Mara ndio wananawa mikono kila wanapotoka chooni kujisaidia pia changamoto zinazosababisha kutojenga vyoo bora ni wananchi kutumia Ziwa Victoria kujisaidia haja kubwa, madereva kushusha abiria njiani, naomba wananchi waelewe kuwa vyoo bora ni vyoo vyenye kuta nne, paa, sakafu, kifaa cha kunawia mikono chenye maji na sabuni," alisema.

Ofisa Afya wilayani Bunda, Fadhili alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha kila kaya inatumia choo bora ili kujikinga na magonjwa hayo.

Alisema kwa kipindi cha Aprili hadi Juni, mwaka huu, takwimu zinaonyesha kuwa kaya zenye vyoo bora ni 31,725 ambazo ni sawa na asilimia 57 kati ya kaya 55,702 na 2,239 sawa na asilimia nne hazina vyoo.

Mkuu wa wilaya hiyo, Lidya Bupilipili, alitoa wito kwa jamii kubadilika na kuachana na vitendo vya uharibifu wa mazingira kwa kujenga vyoo bora na kuvitumia, pia aliwataka wanawake na wasichana kuacha urembo wa kufuga kucha ndefu au kuweka kucha bandia kwasababu zinaficha uchafu unaoweza kusababisha magonjwa hayo.

Mkuu wa Mkoa huo, Adamu Malima, alionyesha kusikitishwa na baadhi ya tabia mbaya zinazotia dosari mkoa huo kama vile ukatili dhidi ya wanawake, ubakaji wa watoto, ukeketaji na tatizo la wananchi kuchafua mazingira kwa kujisaidia vichakani, kwenye miamba na Ziwa Victoria na kuwataka wananchi kuacha vitendo hiyo vinavyoaibisha kwa kuwa serikali itazingatia sheria kwa atakayebainika.



Fundi wa kampuni ya Estim, akiendelea na ujenzi wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Kimara Stop Over, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: JOHN BADI**

# Wananchi 700 Pemba wadai vitambulisho vya kuzaliwa

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

ZAIDI ya wananchi 700 wa Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba, wanadai vyeti vyao vya kuzaliwa katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Rashid Hadid Rashid, alisema kwa sasa ofisi hiyo inadaiwa vyeti vya mwaka mmoja tu.

Alisema kuwa, katika Wilaya ya Chakechake vyeti vya kuzaliwa havichukui muda mrefu hukabidhiwa wananchi wenyewe, ingawa idadi ya wanaohitaji vyeti ni kubwa na kuwataka wananchi hao kuwa wastahamilivu.

"Upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa wilaya hii, hauzidi mwaka mmoja wananchi wanapatiwa vyeti vyao, lakini tunatoa kulingana na magamba yaliyopo," aisema.

Alisema kila mwezi katika wilaya hiyo wanazaliwa watoto 600, ambapo kila mwaka ni watoto 7,200 wanaohitaji vyeti vya kuzaliwa.

"Wananchi waone kuwa serikali inajitahidi, lakini kiwango cha wahitaji vyeti ni kubwa sana, hivyo tunawaomba watumie uzazi wa mpango ili kuondosha changamoto hiyo," alisema.

Aidha, alieleza kuna vyeti 2,261 ambavyo vimeshatengenezwa tangu mwaka 2014, ingawa wenyewe hawajaenda kuvichukua.

"Hapa ofisini kwetu kuna vyeti tokea mwaka 2014 hadi mwaka jana wenyewe hawajaja kuvichukua, tunaomba waje wavichukue wasiwe wanalalamika tu," alisema mkuu huyo.

Hivi karibuni wananchi wa wilaya hiyo walilalamikia ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto, ambapo waliizungumzia kwenye misikiti changamoto hiyo, ambayo hukaa kwa muda mrefu bila kupatikana huku wananchi wakipoteza fedha nyingi kwa ajili ya nauli kufuatilia kila siku.

## Mkuu wa shule akalia kuti kavu

Na Tiganya Vincent, TABORA

SERIKALI imemsimamisha kwa muda Mkuu wa Shule ya Sekondari Kamagi wilayani Sikonge, Juma Nkungu, kupitisha uchunguzi juu ya tuhuma mbalimbali zinazomkabili ikiwamo mbao 180 zilizoondolewa bila kufuata utaratibu.

Hatua hiyo imechukuliwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bwalo la chakula katika shule na kukuta mapungufu ya kutokuwapo na taarifa inayoonyesha uingizaji wa vifaa vya ujenzi.

Alisema mapema mwaka huu alipotembelea shule hiyo kwa ajili ya kukagua mradi ya ujenzi wa bwalo hilo, alikuta mbao zipato 180 ni mbovu ambazo zilikuwa hazifai kwa ujenzi na kuagiza ziondolewe na mzabuni aliyewauzia mbao hizo alilete nyingine kufidia.

Mwanri alisema baada ya kufika mara ya pili ili kuona kama agizo lake limetekelezwa ndipo alipokuta kuna mapungufu mengine ikiwamo kutokuwapo na ushahidi unaoonyesha kama kweli mbao mbovu zilizoondolewa na zilipelekwa wapi na fidia yake.

"Kukosekana kwa nyaraka zinazoonyesha kutoka na kupokelewa kwa mzigo wa mbao hizo kunatia shaka, jambo linaoonyesha kuwa kuna uwezekano wa mchezo mchafu umefanyika," alisema.

Aliongeza kuwa hata diwani wa eneo hilo na wajumbe wa kamati zote tatu ya ujenzi, mapokezi na manunuzi walipoulizwa walisema hawajui siku mbao mbovu zilizopotoka na siku za fidia zilipopokelewa na kuwa Mkuu wa Shule hiyo ndio pekee anajua.

Kufuatia mapungufu hayo, amemwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Sikonge (OCD) kuimarisha ulinzi katika Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari hiyo, ili hasiingie katika ofisi kwa ajili kupisha timu ya ukaguzi na uchunguzi ifanye kazi na kujua ukweli kwa kupitia nyaraka zote zilizoko katika ofisi hiyo.

Alisema wakati uchunguzi ukiendelea Ofisa Elimu Wilaya ya Sikonge, Yussuf Hamza, atafute mwalimu wa kukaimu nafasi hiyo na kama akimkosa yeye achukue jukumu la kusimamia shule hiyo hadi hapo hatua nyingine zitakapokamilika.

Mwanri alisema baada ya uchunguzi wampatie taarifa na kama watakuta hakuna kasoro Mwalimu Mkuu huyo arudishwe katika nafasi yake.

"Nyie fanyeni uchunguzi endapo mtamkuta hana tatizo, mrudishe katika nafasi yake...mimi sitaki kumwonea mtu ...ninachotaka kujua ni thamani halisi ya fedha ya umma iliyotumika kama inalingana na huduma iliyotolewa," alisisitiza.

Naye Hamza alisema kwa muda mrefu aliomba mchanganuo wa matumizi ya fedha za mradi huo, lakini alizungushwa bila kupata na ndipo alipochukua uamuzi wa kumwita katibu wa ujenzi na kumfungia ofisi kwake, ili atoe taarifa na ndipo ilipopatikana na kuonekana na mapungufu.

# Elimu yatajwa kikwazo kwa wasaidizi kisheria

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WASAIDIZI wa kisheria mkoani Rukwa, wameshauriwa kujiendeleza kielimu ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi na kufuata sheria kwani masuala ya kisheria ni ya kitaaluma, hivyo ni muhimu kuwekeza katika elimu.

Ushauri huo ulitolewa jana na Charles Sylvester, Ofisa Mradi wa Shirika la Kaengesa Environmental Conservation Society (KAESO) lenye kazi ya kuwajengea uwezo wasaidizi wa kisheria mkoani humo, katika mafunzo ya siku mbili ya kujenga uhusiano wa kikazi kati yao na waandishi wa habari yaliyofanyika katika kijiji cha Kirando wilayani Nkasi.

Alisema kuwa changamoto kubwa inayowakabili wasaidizi hao wa kisheria hususani walioko vijijini ni elimu ndogo, kitendo kinachosababisha utendaji kazi mdogo, lakini kama wangekuwa na elimu ya kutosha isingekuwa kazi kubwa.

Sylvester alisema kipindi cha nyuma kabla ya kuwepo sheria rasmi inayowatambua kazi hiyo ilikuwa inaonekana inafanywa zaidi na wanaharakati ambao baadhi yao walikuwa wanapata umaarufu kwa kuzungumza sana na hivyo kujipa kazi hiyo ambayo ni ya kitaaluma.

**Wapo baadhi ya wasaidizi wa kisheria mkoani humo wanashindwa hata kuandaa taarifa ya utendaji kazi wao, lakini imebainika kuwa baadhi yao wana elimu ndogo hali ambayo imekuwa kikwazo katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.**

Alisema wapo baadhi ya wasaidizi wa kisheria mkoani humo wanashindwa hata kuandaa taarifa ya utendaji kazi wao, lakini imebainika kuwa baadhi yao wana elimu ndogo hali ambayo imekuwa kikwazo katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mratibu huyo alisema hivi sasa taasisi hiyo inampango wa kuchagua watu wengine ili wafanye kazi hiyo ambao watakuwa wamehitimu kidato cha sita ambao watakuwa na elimu ya kutosha na iwapo watawajengea uwezo wanaamini wataweza kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa tofauti na ilivyo hivi sasa.

Naye Seth Goliawa, mmoja wa wasaidizi wa kisheria mkoani humo, alisema fursa ya wao kukutana na waandishi wa habari na kujenga uhusiano wa kikazi imekuwa nzuri kwani baadhi ya wananchi hawawaelewi licha ya kwamba wapo na wanafanyakazi kwa mujibu wa sheria za nchi, lakini changamoto kubwa iliyopo ni kutojitangaza.

Alisema wao wamekuwa wakiwasaidia wananchi bila malipo, lakini hata hivyo changamoto iliyokuwa ikiwakabili ni kutofahamika, lakini sasa kwa kuwa wametengeneza ushirikiano na wanahabari itakuwa ni rahisi na wananchi wengi watapata msaada huo ili wapate haki zao kutokana na wanahabari kuwaelimisha wananchi kuhusu majukumu yao.

Israel Mwaisaka, mmoja wa wanasheria mkoani humo, alisema wameona kuwa kuna umuhimu wa kuwa na mahusiano ya karibu ya kikazi na wasaidizi hao wa kisheria kwani jamii inahitaji kuwafahamu na huduma kutoka kwao.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, Bili Chidabwa (kushoto), akizungumza na Wananchi wa mji wa Kongwa, mkoani humo mwisho wa wiki katika mkutano wa hadhara wa kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# WLAC yataka nguvu pamoja kulinda watoto

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto (WLAC), kimesema bado kunahitajika nguvu kubwa ya pamoja katika kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto wadogo vinavyofanyika sehemu mbalimbali nchini.

Wakili wa WLAC, Abia Richard, akizungumza katika tamasha la kutoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili katika Shule za Msingi za Mbagala na Mbagala Anex jijini Dar es Salaam, alisema pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na serikali na wadau mbalimbali katika kupambana na vitendo hivyo, lakini bado ukatili unafanyika kwa watoto.

Alisema kama wadau muhimu ambao wamekuwa wakipambana kila siku kukomesha vitendo hivyo, tayari wameshaanza kuona matunda ya kazi ya utoaji elimu wa namna ya kupambana na vitendo hivyo, kutokana na mwamko uliopo kwa jamii kwa sasa katika kutoa taarifa pindi wanapovishuhudia.

"Sasa hivi tunaona mwamko na kasi ya kuripoti vitendo hivi katikati ya jamii tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma ambavyo ilikuwa ni nadra sana mtu yeyote katika jamii au mzazi kukimbilia katika vyombo vya dola kutoa taarifa anaposhuhudia vitendo hivi, tunaamini elimu ambayo tumeendelea kutoa inasaidia na hii ndiyo dalili njema kwamba tutafanikiwa katika vita hii," alisema Abia.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mbagala Anex, Barnaba Mahinya, alisema kazi inayofanywa na WLAC ya kutoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili kwa wanafunzi shuleni, inasaidia kuwafumbua akili ya kufahamu vitendo hivyo, na kutoa taarifa pindi wanapofanyiwa au kuona viashiria vya kufanyiwa.

# NMB yatoa milioni 570/- uwajibikaji kwa jamii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeshatoa kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 570 mpaka sasa kati ya Sh. bilioni moja ilizotenga kama uwajibikaji wake kwa jamii kwa mwaka huu wa 2019.

Kiasi hicho kimetumika zaidi kusaidia miradi mbalimbali ya kijamii kama elimu, afya na kusaidia majanga mbalimbali yanayoipata nchi ikiwa ni utaratibu wa benki wa kila mwaka kutenga asilimia moja ya faida yake kusaidia miradi mbalimbali ya kijamii.

Utaratibu huo uliendelea tena mjini wilayani Kwimba mkoani Mwanza ambapo NMB imetoa madawati 607 yenye thamani ya Sh. milioni 55 kwa shule tisa za msingi wilayani humo na mbili Wilaya ya Nzega mkoani Tabora.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi sehemu ya madawati hayo iliyofanyika katika Shule ya Msingi Budushi wilayani Mwimbai, Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa wa NMB, Amos Mubusi, alisema mchango huo ni katika kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano.

"Ingawa serikali ya awamu ya tano inafanya makubwa, sisi kama wadau tunawajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii iliyoifanya NMB kufikia hapa ilipo kama benki kubwa kuliko zote nchini," alisema Mubusi.

Alisema ni kwa kutambua juhudi hizo za serikali NMB iliamua kuyafanyia kazi haraka maombi iliyopokea kutoka shule tisa za msingi wilayani Misungwi, hivyo kukabidhi madawati hayo, alisema Mubusi.

Alizitaja shule zitakazonufaika na msaada huo kuwa ni Mhalo, Sangu, Mwankulwe, Luhala, Budushi, Bumyengeja, Mwabaratulu, Kabale na Ng'wambisu zitakazopata kati ya madawati 55 na 58 kila moja.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kwimba, Ally Nyakia, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Senyi Ngaga, alisema sekta ya elimu inatakiwa kupewa kipaumbele wakati serikali ikipiga mbio kuelekea uchumi wa kati.

Alisema wadau kama NMB ni muhimu kuelekea azima hiyo ya serikali na kuomba wadau wengine wa maendeleo kuiga mfano wa benki hiyo, katika kuunga mkono jitihada mbalimbali za maendeleo.

Aliishauri pia NMB kufungua tawi katika mji mdogo wa Sumve ili kuwapunguzia usumbufu watumishi na wananchi kusafiri kwenda Ngudu mwendo wa kama kilometa 40 hivi kufuata huduma mbalimbali za kibenki.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Godfrey Ngupula, alitoa shukrani baada ya kupokea madawati 100 kwa ajili ya Shule za Msingi Nata na ya Sekondari Undumo zilipo Nzega, alisema msaada huo utachangia kuongeza ubora wa mazingira ya kusoma kwa wanafunzi kwenye shule hizo mbili

Ofisa Elimu (Ufundi) wa Wilaya ya Kwimba, Vedastus Nyambalije, alisema wilaya ina jumla ya wanafunzi wapatao 118,026 katika shule za msingi zipatazo 151 za umma na walimu 1,621 na kwamba idadi hiyo ni sawa na mahitaji ya madawati 33,514.

Alisema kabla ya ufadhili wa NMB, Wilaya ya Kwimba ilikuwa na madawati 27,727, hivyo kuwa na upungufu wa madawati 6,978 na kwamba kwa msaada huo sasa upungufu umebaki 5,280 tu.

# Wadau utalii waiomba Israel ifungue ubalozi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WADAU wa utalii wameiomba Israel kufungua ubalozi nchini kuwapunguzia gharama za kufuatilia viza Watanzania wanaotaka kutembelea taifa hilo.

Kwa sasa, Watanzania wanalazimika kufuatilia viza kwenye ubalozi wa Israel Nairobi, Kenya, jambo linaloongeza gharama za safari, hasa kwa watalii na mahujaji wanaotaka kwenda Israel.

Wakizungumza wakati kundi la watalii wa Tanzania 64 likiondoka nchini mwishoni mwa wiki kwenda Israel, wadau hao waliomba nchi hiyo ya Mashariki ya Kati, kufungua hata ubalozi mdogo jijini Arusha, ili kuwapunguzia mzigo wa kwenda nchini jirani kufuatilia viza.

Mratibu wa safari hiyo kutoka Kampuni ya Utalii ya Excellent Guide ya jijini Arusha, Harrison Chonjo, alisema kutokana na hamasa ya Watanzania kutaka kutembelea Israel, nchi hiyo inapaswa kufikiria ombi hilo la kufungua ubalozi wake nchini.

"Hamasa ya Watanzania kutembelea Israel ni kubwa, na hili ni kundi la mwanzo kwenda kwa wingi tunaomba nchi hiyo ifungue ubalozi ili kupunguza gharama kwa watalii wetu na kuongeza idadi yao baada ya gharama kushuka," alisema Chonjo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Aliongeza kuwa wamefanya utaratibu wa watalii kutoka Tanzania kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Israel (El Al) zinazoleta watalii nchini, ambayo hufanya safari zake moja kwa moja kutoka KIA hadi Tel Aviv nchini Israel.

"Waisrael wanakuja nchini mara kwa mara, hivyo nasi tunatumia fursa hiyo kutumia ndege zao kuwapeleka Watanzania huko, badala ya ndege hizo kurudi Israel bila abiria, hali inayorahisisha usafiri wa moja kwa moja na wa uhakika," alisisitiza mratibu huyo.

Kiongozi wa kundi hilo, Padri Melodius Mlowe wa Jimbo Katoliki Njombe alisema, watalii hao Watanzania wanatoka mikoa mbalimbali ambao baada ya kuwahamasisha kupitia kanisa hilo kwenda kujifunza fursa mbalimbali zilizopo Israel pamoja na kuhiji, wamechangamkia fursa.

# Baraza la Ardhi lamaliza mgogoro, latengua umiliki

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

BARAZA la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Arusha, limemaliza mgogoro wa ardhi wa miaka saba kwa kutengua umiliki wa ardhi yenye ukubwa wa hekari 15, iliyokuwa ikimilikiwa na mtu binafsi na kuwakabidhi wananchi wa Kata ya Sokoni One waliokuwa wamiliki tangu awali.

Kabla ya kesi ya ardhi ilimilikiwa na mwanajeshi mstaafu, Willison Rugumamu, aliyeitumia kujenga kituo cha watoto yatima cha Huruma Vision Tanzania.

Hata hivyo rasilimali hiyo imerudishwa tena kwa wananchi wa Kata ya Sokoni One waliofungua shauri hilo tangu mwaka 2012.

Akisoma hukumu hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita katika kesi ya ardhi namba 147 ya mwaka 2012, iliyofunguliwa na Rugumamu akiwalalamikia wananchi saba wa Kata ya Sokoni One, kwa kuvamia eneo hilo na kufanya uharibifu, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Fadhili Mdachi, alidai kuwa mlalamikaji ameshindwa kuthibitisha uhalali wa yeye kuwa mmiliki wa eneo hilo, hivyo baraza limetupa maombi yake.

**Baraza limepitia ushahidi wa pande zote mbili na kuonelea kwamba ushahidi wa upande wa utetezi una uzito, kwani ugawaji wa eneo hilo haukupata baraka za mkutano mkuu wa kijiji.**

Mdachi alisema kuwa Rugumamu alipeleka maombi ya kutaka baraza hilo limtambue kama mmiliki halali wa eneo hilo, lakini ushahidi alioutoa kupitia mashahidi saba, umekosa mashiko ya kulishawishi baraza hilo limtambue kama mmiliki halali wa eneo hilo.

Katika hukumu hiyo, Mdachi alizingatia kuwa mlalamikaji hakuwa amekabidhiwa eneo hilo kihalali, kupitia mkutano mkuu wa Kijiji cha Sokoni One na kwamba hapakuwa na makubaliano yoyote kwamba atajenga ofisi ya kijiji kama mbadala wa eneo hilo, badala yake baraza hilo limeonelea kuwa ofisi ya kijiji aliyojenga, alifanya hivyo kama mfadhili na si makubaliano ya kupatiwa eneo kama alivyodai.

"Baraza limepitia ushahidi wa pande zote mbili na kuonelea kwamba ushahidi wa upande wa utetezi unauzito, kwani ugawaji wa eneo hilo haukupata baraka za mkutano mkuu wa kijiji na kwamba halmashauri iliyomgawia eneo hilo, haikuwa na muhtasari wa mkutano mkuu uliokubaliana eneo hilo ligawiwe kwa malalamikaji," alisema Mdachi.

Mdachi alisema baraza limeamua kulirejesha eneo hilo kwa wananchi, baada ya kuwatambua kama wamiliki halali wa eneo hilo na kumtaka Rugumam kukata rufani ndani ya siku 45 iwapo kama hajaridhika na maamuzi hayo.

Baada ya maamuzi hayo kutolewa nje ya chumba cha baraza hilo, baadhi ya wananchi waliokuwa wamefurika kusikiliza shauri hilo lililodumu kwa takribani miaka saba, walilipuka kwa shangwe na kulishukuru baraza hilo kwa kutenda haki na wameahidi kulitumia eneo hilo kwa shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa kituo cha polisi, shule na zahanati.

Shauri hilo lilifunguliwa katika baraza hilo, mwaka 2012 na mlalamikaji Wilson Rugumamu akiwalalamikia wananchi saba wa kata ya Sokoni One, kwa kuhamasisha wenzao waliokuwa kwenye mkutano kuvamia na kufanya uharibifu wa mali na ukuta wakati wanajua kwamba eneo hilo ni mali yake.

Kufuatia hukumu hiyo Rugumamu aliyekuwa ameambatana na mkewe katika baraza hilo, alishindwa kufafanua iwapo anajipanga kukata rufani au ameridhika na hukumu hiyo, badala yake alidai kuwa anakwenda kutafakari na familia yake juu ya nini cha kufanya.



Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini nchini (Femata), Dk. Bernad Joseph, akizungumza na wachimbaji mkoani Manyara juzi, kuhusu mkutano mkuu wa sita wa Femata, utakaofanyika Agosti 31, mwaka huu, jijini Tanga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tamida yampongeza JPM kuwa Mwenyekiti SADC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA cha wafanyabiashara wa madini nchini (Tamida) kimempongeza Rais John Magufuli, kwa kupokea kijiti cha uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kusema wana imani atasimamia vema ujenzi wa uchumi, viwanda na biashara ya vito na madini katika nchi hizo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Arusha, Mwenyekiti wa Tamida Taifa, Sammy Mollel, alisema kuwa kuchaguliwa kwake kutaongeza biashara ya madini nchini na kwenye ukanda huo, kwa kuwa ameonyesha juhudi kubwa kwenye sekta hiyo na sasa ni miongoni mwa maeneo yanayoongeza mapato ya taifa.

Alisema kuwa kutokana na juhudi hizo ana imani kazi ya kukuza biashara atazielekeza kwenye ukanda huo wa nchi za kusini mwa Afrika na wao wataweza kufaidika na kukua kwa soko na matumizi sahihi ya rasilimali za umma.

Mollel alisema kuwa mageuzi aliyoleta nchini kwa wananchi kukua kiuchumi kwa kasi hiyo hiyo, ataelekeze katika ukanda huo kukua kiuchumi na kuweza kuwanufaisha wananchi wa Kusini mwa Afrika.

"Cha msingi watu wa ukanda huu waache ulanguzi na kufanyabiashara kwa uwazi, ili tuweze kupatia nchi zetu mapato na kukuza uchumi na mwisho wa siku maendeleo ya kiuchumi yaonekane," alisema Mollel.

"Kuchaguliwa kwa Rais Magufuli kunatupa imani kwamba ataleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa nchi yetu na nchi za SADC, ili kufikia uchumi wa kati wa viwanda. Anaweza maana hata hapa kwetu amebadilisha mambo mengi na kila mwenye macho anaona," alisema Mollel.

"Tunamwomba Rais kasi alioanza nayo hapa nchini ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kudhibiti mianya ya rushwa na utoroshwaji wa madini, aipeleke pia kwa nchi hizo, ili kuweza kubadilika na kuondoa umaskini katika mataifa hayo," alisema Mwenyekiti wa Tamida.

# Waziri aagiza mgogoro Umbwe, Lyamungo utatuliwe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kutafuta kiini cha mgogoro baina ya Sekondari za Lyamungo na Umbwe.

Aidha, amewataka wakuu wa shule nchini kuondoa unyanyanyasaji shuleni na shule itakayobainika kukiuka agizo hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Kadhalika alisema miongoni mwa hatua hizo ni pamoja mkuu wa shule kupoteza sifa ya mwalimu mkuu na hata akihamishwa hawezi kuipata tena nafasi hiyo iwe Bara au Visiwani pia atapelekwa shule za pembezoni kufanya kazi.

Jafo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungunza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Umbwe na kuwataka kutobaguana kwa misingi ya kabila rangi au dini.

"Zipo taarifa za chini kwa chini, shule hii ya Umbwe haina uhusiano mzuri na Sekondari ya Lyamungo na sababu bado haijafahamika... Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro nakuagiza fuatilia suala hili hakikisha unapata chanzo cha migogoro hiyo na kutafuta amani miongoni mwao... pia waweke mazingira ya kucheza mechi za kirafiki miongoni mwao," aliagiza waziri.

**Serikali ya awamu ya tano inawekeza nguvu nyingi kwenye ukarabati wa shule kongwe sanjari kutoa elimu bure kwa lengo la kuwapa watoto wa Tanzania elimu bora, hivyo hakuna ruhusa ya kunyanyasa na kujenga chuki miongoni mwa vijana.**

Akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, Waziri Jafo, aliahidi kutekeleza agizo hilo na kuwataka wanafunzi kutumia vyema taaluma wanayoipata kwa ajili ya kuleta tija kwa taifa.

"Sisi kama walezi hatuwezi kukubali dhana ya unyanyasaji na ubaguzi mnayotaka kuianzisha kwa misingi ya udini, ukabila au rangi miongoni mwa wanafunzi kwani italeta chuki hali itakayosababisha kukosekana kwa upendo na amani kwa taifa," alisema Jafo.

"Ninaagiza walimu wote nchini kuhakikisha hakuna manyanyaso yanayoendelea miongoni mwa wanafunzi kutokana na darasa alilopo, dini au kabila, nitakaposikia hivyo, mkuu huyo atakuwa amejipotezea sifa za kuwa mkuu wa shule na badala yake atapangwa kuwa mwalimu wa kawaida," alisema Jafo.

Ifahamike kuwa, ikiwa kutakuwa na unyanyasaji wowote ni lazima kuondoa uongozi uliopo na walimu tutawasambaza kwenye mikoa mbalimbali, ili kujifunza namna ambavyo walimu wengine wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Alisema serikali ya awamu ya tano inawekeza nguvu nyingi kwenye ukarabati wa shule kongwe sanjari kutoa elimu bure kwa lengo la kuwapa watoto wa Tanzania elimu bora, hivyo hakuna ruhusa ya kunyanyasa na kujenga chuki miongoni mwa vijana.

Aidha, waziri aliwataka walimu kwa kushirikiana na wanafunzi kuweka mikakati ya kuondoa sifuri katika shule zote hapa nchini.

Akitoa neno la shukurani mwanafunzi wa kidato cha tano, katika mchepuo wa Uchumi, Biashara na Akaunti (ECA), Abduli Mulokozi, aliahidi kutekeleza agizo la waziri kwa vitendo.

Alieleza kuwa unyanyasaji katika shule unaweza kujenga chuki hata kwenye mazingira ya kazi baada ya kuhitimu katika shule hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba (kushoto) na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya (wa pili kushoto) wakichangia damu kwa ajili ya kuwasaidia majeruhi wa ajali ya moto iliyotokea mkoani Morogoro, katika zoezi lililoandaliwa na UVCCM mkoani humo juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

## Aagiza viongozi kulinda wajane

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewataka viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kusaidia wanawake wajane baada ya kufiwa na waume ili wapate haki zao.

Akizungunza na Nipashe ofisini kwake alisema katika mkoa huu wajane wengi wamekuwa wakinyanyaswa, kufukuzwa na kudhulumiwa mali mara baada ya vifo vya waume zao na kupelekea migogoro katika familia.

Alisema wajane wengi wanapoteza haki zao baada ya waume zao kufariki hali inayosababisha wabaki na visasi, huzuni na ongezeko la watoto wa mitaani na magonjwa kutokana na msongo wa mawazo.

"Nawaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasimamia na kutetea haki za wajane wanapofiwa na wenza ili kupunguza migogoro na dhuluma kwa wajane na watoto," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Alisema umefika wakati kinamama kuwa na sauti moja ya kukemea ukatili, ukeketaji na kurithiwa baada ya waume zao kufariki hali ambayo inaleta ongezeko la mitafaruku katika familia na kukwamisha maendeleo.

Alisema viongozi wote hasa wa wilaya na mkoa wahakikishe wanafanya kazi ya kuwa wasuluhishi wa migogoro katika kutoa elimu kwa wananchi, ili kuondokana na mila na desturi za ukandamizaji wa wanawake katika jamii.

"Nawaomba viongozi wa dini kuombea amani, kuwapa wananchi wa mkoa matumaini mapya kwa kutoa ushauri nasaha wa kuachana na vinyongo vilivyosababishwa na kudhulumia mali kwa muda mrefu. Vinyongo, hasira na mambo yanayofanana na hayo husababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani," alisema Mkuu wa Mkoa.

Akizungumza kwa niaba ya wajane katika Wilaya ya Moshi, Faustina Msaki, alikiri kuwapo kwa ukatili kwa wajane baada ya wenzi kufariki na kuiomba serikali kukemea jambo hilo kwa vitendo .

"Tunaiomba serikali mbali na kushiriki kwenye vikao vya familia na kutoa elimu , lakini pia mahakama zetu zisimamie sharia, haki na usawa bila kumtizama mwenye nacho," alisema Elisaria Masawe mwenye miaka 61.

# Uongozi kuzuia watoto sokoni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UONGOZI wa Soko la Mitumba la Memorial lililoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, umeahidi kupiga marufuku wafanyabiashara kushinda na watoto wadogo kwenye biashara zao sokoni hapo.

Aidha, viongozi wameahidi kuwa watashirikiana na Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi, kupiga marufuku wafanyabiashara wa soko hilo kwenda sokoni hapo na watoto chini ya miaka mitano.

Sababu za kuchukua hatua hiyo ni kukabiliana na malezi hatarishi ya watoto katika maeneo ya ujasiriamali, ikiwamo sokoni, kwa mujibu wa mwenyekiti wa soko hilo, Godffrey Shayo.

Aidha, kabla ya kuanza kutekeleza utaratibu huo mpya, uongozi huo utatoa elimu kwa wazazi na walezi wenye watoto kuanzia miaka sifuri hadi mitano ambao wanaonekana sokoni hapo kuanzia saa 12 alfajiri hadi saa 1:00 usiku wakiwa na wazazi wao. Alisema hayo wakati wa utafiti wa kuongeza uelewa, uwajibikaji wa huduma bora za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto (ECD), unatekelezwa na Muungano wa Vilabu vya Waandishi wa Habari nchini (UTPC) kwa kushirikiana na taasisi ya CiC ya Ireland.

"Ukija sokoni hapo majira ya saa 11 alfajiri utaona wazazi na walezi wakiwa na watoto wachanga...Huu ni ukatili na unaathiri afya ya mtoto na malezi yake ya baadaye, tumeliona hili na tunaandaa mpango wa kutoa elimu kabla ya kuchukua hatua," alisema Shayo.

Mwenyekiti wa Masoko la Mbuyuni, Lameck Mziray na Mwenyekiti Mtaa wa Soko la Pasua, Rahibu Juma, walikiri kuwapo kwa changamoto inayoathiri afya za watoto hao na kuahidi kuandaa mpango wa kushirikishwaji na wafanyabiashara ili kujadili suala hilo.

Daktari bingwa mwandamizi wa afya ya jamii, uzazi na magonjwa ya kinamama, Dk. Moke Magoma, alisema malezi hayo yasipodhibitiwa yatachangia kwa asilimia kubwa kujenga taifa la kizazi kisicho na mweleko na chenye urahisi wa kujihusisha na matukio ya uhalifu.

Alisema maeneo ya ujasiriamali siyo salama kwa malezi na makuzi ya watoto kiafya na kisaikolojia na kwamba jambo la msingi ni kwa wazazi na walezi wakatafuta mbinu mbadala ili kuokoa kizazi hicho.

Baadhi ya wazazi Mwantumu Swalehe na Hadija Omary walisema wanalazimika kwenda katika maeneo ya ujasiriamali na watoto kutokana na kukosa imani na walezi wengine hususani ndugu wa karibu wa kiume ambao huwafanyia ukatili wa kingono.

"Usituone tunahangaika na watoto wetu huku sokoni, tunafahamu kwamba ni hatari kwa afya lakini inatulazimu kutokana na kubadilika kwa dunia ya sasa...huyo unayemwamini ndiye anaye kuharibia mtoto, serikali ilitizame hili," alisema Swalehe.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 20, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15



## Ajali barabarani zinavyoathiri uchumi, nguvu kazi nchini

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Ndege yaanguka baada yakugonga nyumbu Kenya



# CHANGAMOTO SOKO LA MAZAO YA WAKULIMA LAPATIWA MUAROBAINI

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro (aliyeweka mikono mbele), akipokea taarifa kutoka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, ACP Wilbroad Mtafungwa (wapili kulia), baada ya kuwasili eneo la tukio ilipotokea ajali ya lori lililokuwa limebeba mafuta aina ya petroli na kusababisha vifo na majeruhi.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro (wapili kulia), akimpa pole mmoja ya majeruhi wa ajali ya moto iliyotokea eneo la Msamvu Ndege wengi katika Wilaya ya Morogoro mjini, baada ya kuwasili katika Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro.



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, akizungumza na wakazi wa Kata ya Mburahati, Kigogo jijini Dar es Salaam, wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye Kata hiyo kwa lengo la kujua changamoto wanazokutana nazo pamoja na namna wanavyoshirikiana na Jeshi hilo kuzuia uhalifu na wahalifu katika maeneo yao. **PICHA: JESHI LA POLISI**



# TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Visawe, Vitawe, Vitate ni nini? - 3

MATOLEO mawili yaliyopita tuliona maana ya 'Visawe' na 'Vitawe'. Leo twawaletea maana ya 'Vitate' yaani maneno yanayotatanisha au yanayokaribiana kimatamshi lakini yenye maana tofauti.

Aghalabu hutofautiana kwa sauti moja. Mifano ya vitate ni kama ifuatavyo:

Ama: au, pengine. Hama: ajiri; toka katika makao fulani na kwenda kwingine. Asi: goma, kataa kufuata sheria. Hasi: kumfanya ng'ombe dume kuwa maksai; (ashaakum!) ondoa makende kutoka kwa mnyama dume. Bari: jitenga, kaa kando. Bali: ila, isipokuwa. Bibi: mama aliyemzaa baba au mama; peremende. Bua: shina la mhindi au mtama; kifaa cha chuma kinachotumiwa na wahunzi kukoleza moto. Pua: sehemu katika uso inayotumiwa kupumua.

Daawa: madai au jambo linalosababisha ugomvi. Dawa: kemikali inayotibu maradhi au kitu apewacho mtu ili awe katika afya au mienendo mizuri. Doa: kasoro, alama. Ndoa: nikaha, arusi. Faa: kuwa na faida. Vaa: kutia nguo mwilini. Fahari: utukufu au majivuno. Fahali: ng'ombe dume. Fua: osha kitu kama vile nguo ili kuondoa uchafu. Vua: toa nguo mwilini; nasa samaki.

Fuja: tumia vibaya, kwa mfano fedha. Vuja: pitisha kitu hasa maji kwenye upenyo. Fuka: toa moshi. Vuka: pita au enda upande wa pili. Hanja: zunguka huko na huko kwa majivuno. Haja: matlaba, mahitaji. Jabari: mwenye nguvu, shujaa. Jabali: jiwe kubwa; mwamba.

Kataa: zira, goma, kutokubali. Kata: tema, gawanya kwa chombo chenye makali; mteka maji. Komaa: pevuka, kuwa pevu, zeeka. Koma: fikia mwisho; acha. Kura: uchaguzi (aghalabu piga kura), chagua. Kula: bugia mlo. Landa: fanana kwa umbo, sura au tabia na mtu au kitu fulani. Randa: kifaa cha seremala chenye kisu upande wa chini ambacho hutumika kusawazishia mbao na kuzilainisha.

Mahari: malipo ya kuolea. Mahali: maskani au pahali. Masaibu: matatizo yanayomkumba mtu. Mashaibu: wanaume wazee. Masahibu: marafiki. Mchi: mti wa kutwangia katika kinu. Mji: mkusanyiko wa nyumba nyingi, maskani ya watu; sehemu ya tumbo la uzazi kwa wanawake, tumbo la uzazi. Nchi: taifa, jamhuri. Inchi: kipimo cha urefu katika rula au mita.

Pofu: -siyo na uwezo wa kuona. Povu: viputo vidogodogo vinavyotoka kwenye maji kwa kuchemka au kuyasukasuka ili kitu kiwe baridi; malipo yanayotolewa kwa mtu ili kumtuliza kwa shida iliyompata.

Sama: kwama hasa kooni, sakama. Zama: didimia majini; kitambo cha miaka mingi; kale. Suka: songa kama vile nywele. Shuka: teremka. Thibiti: kuwa -a kuaminika, kitendo cha jambo kuwa la kweli. Dhibiti: weka sawasawa, kitendo cha kukamata kitu au mtu vyema mkononi; kitendo cha kutawala taratibu za mtu au uendeshaji wa jambo. Vuta: sukuma kuja upande wako; kitendo cha kutandaza donge la unga katika umbo juu ya kibao ili uwe bapa. Futa: pangusa, ondoa uchafu; achisha kazi.

Baadhi ya watu wa makabila yetu hutamka, kwa mfano: 'fikombe' badala ya vikombe; 'nasi' badala ya nazi; 'mbusi' badala ya mbuzi; 'samani' badala ya zamani; 'shakula' badala ya chakula; 'ukali' badala ya ugali; 'mboka' badala ya mboga; 'mwesi' badala ya mwezi, 'kari' badala ya gari, 'mutu' badala ya mtu, 'wasiri' badala ya waziri n.k.

Tukiacha hayo ya matamshi mabaya, sasa tugeukie makosa yafanywayo na baadhi ya waandishi wetu, hasa wale wanaoandika kwenye magazeti ya michezo kwa kutumia maneno ya mitaani. Kwa namna wanavyoandika, sasa wanashindwa hata kuandika sentensi zinazoeleweka!

Hii yanikumbusha ile methali ya wahenga isemayo: "Tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena." Hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote zuri huwa na mipaka. Linapozidi huwa halivutii tena.

"Mashabiki wa Yanga kwa sasa wana haki ya kunenepa buana. Wana haki ya kutembea kifua mbele mbele pindi msimu ukianza Kwani ule msoto wa misimu miwili mfululizo wakiburuzwa na watani zao Simba haukuwa wa kitoto, lakini utamu zaidi ni kwamba kwa sasa huko Jangwani mambo yao yanazidi kunoga." (Maneno 48 yaliyoandikwa ovyo).

"Yanga ... wana haki ya kunenepa buana." Mwandishi ana uhakika kuwa mashabiki wa Yanga walikonda ila sasa wananenepa? Neno 'buana' lina maana gani? Ana maana gani kutumia neno 'msoto?' 'Sota' ni sogea kwa (ashaakum) matako na mikono kama kiwete; kweta, jiburura.

Ningeandika hivi: "Msimu ujao mashabiki wa Yanga watafurahi kwani hawatakejeliwa tena na Simba kama ilivyokuwa misimu miwili iliyopita kwani usajili wa msimu ujao unafanywa kwa umakini mkubwa."

"ACP Moshy alisema mfungwa huyo alianza kujikata shingoni kwa kutumia wembe huo huku akiendelea kufanya hivyo kwa kasi ya ajabu na walipomfikia tayari ali- (habari ikaishia hapo bila kukamilika!) Hili si kosa la mwandishi bali ni aliyepanga habari za ukurasa huo na kuikata ili akamilishe kazi haraka kumbe haikukamilika!

"Haraka haraka haina Baraka." Maana yake jambo linalofanywa kwa pupa huwa halikamiliki au halifai. Methali hii yatufunza umuhimu wa kufanya mambo yetu kwa utaratibu kama twataka yafanikiwe.

Waandishi wa michezo wanavyochezea lugha ya Kiswahili, utadhani maneno yaliyopo hayaeleweki! "Yondani hapendi kuzinguliwa bana" ni kichwa cha habari. Paragrafu ya pili imeandikwa: "Jamaa anaposimama pale mkoba akisaidiana na Andrew Vincent (Dante) ama Abdalah Shaibu (Ninja) basi ni lazima washambulizi wa timu pinzani wapate shida sana."

Methali: Imara ya jembe kaingoje shamba.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

NA MASHAKA MGETA

# Ajali barabarani zinavyoathiri uchumi, nguvu kazi nchini

MARA nyingi ajali za barabarani zinapotokea, huleta athari kuu tatu ambazo zinajitokeza mara moja, yaani vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

Dhana inayoelekezwa katika mambo hayo si ya kubezwa kwa maana ni matokeo ya haraka na yanayoonekana kila ajali inapotokea.

Pia, zipo athari nyingine 'zilizofichika za muda mrefu' ambazo hazionekani kwa haraka au kirahisi zinazotokana na ajali za barabarani, lakini zina madhara makubwa katika ngazi tofauti kwenye jamii.

Lakini athari za ajali barabarani zinaweza kuzuilika iwapo kila mtumia barabara, atafuata sheria na kuheshimu kanuni za sheria za usalama barabarani ambazo zinazuia mwendo kasi, kuendesha ukiwa umelewa, kuzingatia umuhimu wa kufunga mikanda, uvaaji wa kofia ngumu na matumizi sahihi ya mikanda kwa watoto kuwazuia na mtikisiko, iwapo ajali itatokea kama ilivyoelezwa katika ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Miongoni mwa athari za kutozingatia suala la usalama barabarani ni zile za kiuchumi ambazo hupoteza au hupunguza nguvu kazi ya familia, vikundi vya watu, jamii na taifa zima kwa ujumla.

Ajali za barabarani huathiri uchumi wa taifa kwa wastani wa asilimia tatu ya pato la taifa.

Makala haya yanayoandikwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa alumnae wa uandishi wa habari za usalama barabarani unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari (TMF) unaozungumzia moja ya viashiria vikuu vilivyoainishwa na WHO ambavyo ni ulevi kwa madereva na jinsi unavyoathiri maisha na maendeleo ya nchi, hivyo ni budi kutoa kipaumbele na nguvu kubwa ya kisheria ili kudhibiti tabia ambayo iwapo itakabiliwa ipasavyo, inaweza kupunguza janga la ajali za barabarani nchini Tanzania.



Ajali kama hizi zinaathiri uchumi na nguvu kazi hivyo hatua zichukuliwe kuwa sheria kali zinazodhibiti ajali barabarani. **PICHA: MTANDAO**

**KAMANDA MUSILIMU AFUNGUKA**

Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani, Fortunatus Musilimu, anasema ulevi kwa madereva ni miongoni mwa masuala muhimu yanayotajwa kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani.

Kamanda Musilimu anasema kwa mujibu wa sheria inayotumika sasa, kiwango cha kilevi kinachokatazwa kwa dereva kinachofikia 0.008 ABC (Alcohol Blood Content) ni kikubwa ikilinganishwa na 0.005 ABC kinachotambuliwa na WHO.

"Kwangu mimi ningependa sana sheria inayokuja itamke kabisa pasiwapo kiwango chochote cha kilevi kwa dereva, lakini kwa sababu ya aina ya vyakula na ming'emenyo yake inayosababisha kuwapo aina ya kilevi mwilini, basi angalau tufikie hiyo 0.05 (BAC) kwa madereva wenye uzoefu wa muda mrefu na wale ambao hawana uzoefu yaani vijana kiwango kiwe 0.02 (BAC) kama WHO," ilivyoelekeza anasema.

Kamanda Musilimu anasema, tofauti na zamani ambapo madereva walipimwa kilevi kwa kutolewa damu, hivi sasa kuna vifaa vyenye kutumia teknolojia ya kisasa kwa 'kuwavutisha' madereva.

Anasema matumizi ya kilevi yatakapopungua ama kutoweka, itasaidia serikali kuepukana na gharama za kupata vifaa hivyo, ingawa vilivyopo kwa sasa vilinunuliwa kabla yake (Musilimu) kushika wadhifa huo.

Ingawa hakuwa tayari kutajwa mwaka huo, lakini Kamanda Musilimu aliteuliwa kushika wadhifa huo Julai mwaka juzi na anathibitisha kuwa vifaa vya upimaji vina ubora na hufanyiwa ukarabati kila baada ya miezi sita.

Pia, pamoja na Kamanda Musilimu kutotaja gharama ama idadi ya vifaa vya kupima ulevi vilivyopo, anasema gharama za ukarabati wake unaofanyika kila baada ya miezi sita, zinatolewa na mzabuni aliyeshinda ununuzi wake, kwa mujibu wa mkataba.

**DAKTARI BINGWA AFICHUA SIRI**

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa na magonjwa yanayosababishwa na ajali wa Taasisi ya Mifupa (MOI), Dk. Kennedy Nchimbi, anasema ingawa katika utoaji huduma kwa wanaopata ajali hawapimi kiwango cha ulevi, lakini ushahidi wa kimazingira unaonyesha kupungua hasa baada ya serikali kupiga marufuku kilevi maarufu kijulikanacho kama 'viroba'.

'Viroba' vilijumuisha aina tofauti ya pombe kali zilizohifadhiwa kwenye mifuko midogo ya plastiki yenye ujazo tofauti na kuuzwa kwa bei rahisi, lakini serikali ikavipiga marufuku mnamo Februari 2017.

Takwimu zinazohusu madereva wa pikipiki na magari zilizotolewa na idara ya takwimu ya MOI zinaonyesha kushuka kwa idadi ya waliopata ajali katika kipindi cha 2016 na 2017. Idadi hiyo ikaongezeka mwaka jana.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2016, madereva wa pikipiki waliopata ajali katika maeneo tofauti ya nchi na kufikishwa MOI walikuwa 1,799, ikashuka mwaka 2017 kufikia 1,486 lakini ilipanda tena mwaka jana (2018) kuwa 1,813.

Kwa upande wa magari, madereva 381 walirekodiwa kupata ajali mwaka 2016 ikilinganishwa na 358 kwa mwaka 2017 na idadi hiyo ikaongezeka mwaka jana kufikia 754.

Hata hivyo, takwimu hizo hizo hazikuweka mgawanyo wa vyanzo kwa kila ajali iliyotokea katika kipindi hicho.

**JE VYOTE VILISABABISHWA NA HIVYO VILOBA?**

Dk. Nchimbi anasema upatikanaji wa huduma za uhakika kwa majeruhi wa ajali za barabarani unachangia kwa namna moja ama nyingine, kuwafanya madereva kutokuwa makini na hivyo kupata ajali.

"Kwa mfano, mtu anapopata ajali akavunjika mfupa na kuwekea chuma, anaweza kuendelea na kazi zake siku chache baadaye... sasa hali hiyo inawafanya wengine waone ajali kama ni kitu kidogo," anasema.

Hata hivyo, Dk. Nchimbi anasema vifaa tiba kama vyuma wanavyowekewa majeruhi wa ajali, vinauzwa kwa bei kubwa inayoweza kuwafanya raia wengi kushindwa kuimudu.

Anatoa mfano wa chuma na nati zinazofungwa kwa mtu aliyevunjika mfupa wa mguu, kwamba vinagharimu takribani Sh. milioni mbili, wakati huduma ya kuviweka ni Sh. 300,000.

Anasema kwa sasa vifaa tiba hivyo vinatolewa kwa msaada wa serikali ya Marekani na hivyo kumfanya mgonjwa kugharamia fedha za huduma peke yake.

Dk. Nchimbi anasema ajali inapotokea kunakuwa na mivunjiko ya aina tofauti ikihusisha paja, miguu, kichwani na sehemu nyingine za mwili.

"Lakini ukimkuta majeruhi ana majeraha kwenye mguu na kichwani, inakuwa moja ya ishara kwamba ajali ilikuwa kubwa na mara nyingi, zinatokana na mwendokasi ama kukosekana kwa umakini ikiwamo kwa mtu anayetumia kilevi," anasema.

**KUPOTEA KWA NGUVU KAZI**

Dk. Nchimbi anasema miongoni mwa athari kubwa za ajali ni kupotea kwa nguvu kazi, ikijikita zaidi katika kada ya vijana na watu wenye uwezo wa kuzalisha kwa ajili ya kaya na jumuiya za watu na taifa kwa ujumla.

Anasema wapo wanaojenga hisia tofauti pindi zinapotokea ajali hasa za bodaboda, kwa kuamini kwamba waathirika wanakuwa madereva na abiria wao tu.

"Hawa madereva wanapofanya kazi wanahitaji mafuta kwa ajili ya vyombo vya usafiri, wanakula kwenye migahawa na hotelini, wananunua vipuri nakadhalika, sasa wanapopata ajali na kutofanya kazi, athari zinaenea hadi kwa wafanyabiashara, wanayumba kiuchumi," anafafanua.

Anaongeza, "kwa hiyo madhara ya ajali za barabarani ni kama hayaonekani lakini yanaendelea kuwaathiri watu wengi zaidi."

Ni dhahiri kwamba ulevi bado unachukua nafasi kubwa miongoni mwa vyanzo vya ajali za barabarani, hivyo jitihada za makusudi ikiwamo kuharakisha mchakato wa maboresho ya sheria ya usalama barabarani si jambo la 'kufumbia macho', bali kulitekeleza kwa vitendo na haraka.

**MWANASAIKOLOJIA ANENA**

Mwanasaikolojia Furaha Dimitrious kutoka taasisi ya Save your Generation Tanzania, anasema ulevi una vyanzo tofauti igawa kwa sehemu, watu wengi wanautumia kwa kujifurahisha na kujisahaulisha changamoto za maisha zinazowakabili.

"Ingawa sina matokeo ya utafiti wa kisayansi, lakini sababu hizo zimebainika katika maandiko mbalimbali ya kisaikolojia yakimhusisha dereva na ulevi," anasema.

"Madereva wengine wanakabiliwa na mazingira magumu ya kazi, uhusiano usiokuwa mzuri ama matatizo kwenye familia, na wapo wanaoamini njia sahihi ya kukabiliana na changamoto hizo ni kunywa pombe na matokeo yake wanaishia kusababisha ajali za barabarani," anasema.

Pia Dimitrious anasema madereva wengine wanatumia kilevi kama sehemu ya imani yao kwamba kinachangia kuwafanya kuwa imara barabarani, hali ambayo ni tofauti na uhalisia wake.

**MTAALAMU WA UPIMAJI KILEVI**

Naye mtaalamu wa upimaji kilevi kwa madereva kutoka Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani, H.3620 PC Salum, anasema vifaa vya upimaji vipo katika hali nzuri yenye kutumia teknolojia ya kisasa kubaini kiwango cha ulevi.

Afande au PC Salum anasema vifaa hivyo vinahifadhi kumbukumbu muhimu ikiwamo kiwango cha kilevi, majina ya dereva na jiografia ya mahali alipopimiwa.

Ni wazi kwamba jamii inapaswa kuelimika zaidi kuhusu madhara yanayoonekana na yasiyoonekana kutokana na ajali za barabarani.

Na kwa hali hiyo, ipo haja ya kubuni mbinu tofauti zitakazofanikisha kudhibiti ajali za barabarani ikiwamo kuboresha sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 ili iendane na mazingira yaliyopo sasa.

***Makala haya yameandikwa kupitia mpango wa Alumnae wa usalama barabarani unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF). Mwandishi anapatikana kwa simu 0754 691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.***

## TEKNOLOJIA

NA RAPHAEL KIBIRITI

# Changamoto soko la mazao ya wakulima lapatiwa muarobaini

- Ni baada ya kuzinduliwa mfumo wa kielektroniki wa ATMIS
- Sasa kuomba vibali, leseni na vyeti vya usafi ni kwa njia ya mtandao
- Umeondoa tatizo la muda na gharama wafanyabiashara ya kilimo

USEMI kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Tanzania, bado una mashiko na yumkini utaendelea kuwa na nguvu japokuwa uliasisiwa kutoka zama za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Nasema bado una nguvu kwa sababu mbalimbali lakini kubwa ni mchango wake kwenye ustawi wa taifa na wananchi wake kwa ujumla.

Takwimu za karibuni zinaonyesha kwamba sekta ya kilimo inachangia asilimia 29.1 ya Pato la Taifa (GDP), asilimia 65.5 ya ajira kwa Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi, kati ya Watanzania takribani milioni 55 kwa hivi sasa.

Aidha, katika zama hizi za kuelekea Tanzania ya viwanda, kilimo kinatoa asilimia 65 ya malighafi za sekta ya viwanda na asilimia 30 ya mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya nchi.

Na ndiyo maana serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imechukua hatua mbalimbali kunyanyua kilimo ili kiwe na tija zaidi kwa wakulima wenyewe, wengi wakiwa wadogowadogo.

Imefanya hivyo kwa njia tofauti ikiwa ni pamoja na kufuta kodi na tozo zaidi ya 100 kwenye sekta hiyo, lakini pia kuwekeza zaidi katika mazao ya kipaumbele, yaani Pamba, Korosho, Tumbaku, Kahawa na Chai.

Aidha, inasisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na kilimo cha kibiashara ili kutoa fursa ya wakulima, wengi wakiwa wadogo wadogo, kuongeza tija na hivyo kunyanyua hali zao za maisha.

Ndiyo ajenda ambayo imekuwa ikisimamiwa katika majukwaa takribani yote anayoyapata Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga, kama ilivyokuwa Julai 4 mwaka huu alipokuwa akizindua Bima ya Mazao kwa wakulima mkoani Simiyu.

Bima muhimu katika kukabiliana na hasara zitokanazo na vihatarishi vinavyoathiri uzalishaji.

Kimsingi jitihada hizi za serikali ya awamu ya tano zimeendelea kuleta tija kutokana na ongezeko la uzalishaji kwenye mazao mbalimbali ya kibiashara na yale yaliyo maalumu kwa ajili ya uhakika wa usalama wa chakula na lishe.

Ongezeko la uzalishaji kwenye zao la pamba ni mfano hai wa namna jitihada za serikali zinavyoonekana kuzaa matunda.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba (TCB), Marko Mtunga wakati wa uzinduzi rasmi wa msimu wa ununuzi wa pamba, Mei 2 mwaka huu, uzalishaji wa zao hilo unatarajiwa kuongezeka msimu huu hadi kufikia tani 400, 000 kutoka zaidi ya tani 200,000 za msimu uliopita.

Hiyo inaonyesha kwamba hatua zinazochukuliwa na Serikali kuboresha sekta ya kilimo zinazidi kuzaa matunda na hivyo kuwakwamua wakulima, wafugaji na wavuvi.



Tatizo la masoko ya wakulima kama hawa wa pamba linatarajiwa kumalizika baada ya mfumo wa ATMIS unaokoa muda na gharama ya kuomba vibali na leseni za kuuza mazao nchi za nje kuanzishwa.



Waziri wa Kilimo Japhet Hasunga akisisitiza jambo wakati wa kilele cha maadhimisho ya sherehe za wakulima (Nanenane) zilizofanyika kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi, Halmashauri ya Mji wa Bariadi Mkoani Simiyu Agosti 8 mwaka huu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Hata hivyo katika ya jitihada hizi, bado kuna changamoto zinazohitaji kutatuliwa ili ajenda ya kuinua sekta ya kilimo iweze kuzaa zaidi matunda tarajiwa kwa maana ya kutoka katika kilimo cha kujikimu hadi cha kibiashara.

Zipo changamoto nyingi kama vile suala la kutegemea mvua, mabadiliko ya hali ya hewa, moto, magonjwa ya mimea kwa kutaja baadhi.

Hata hivyo katikati ya changamoto hizo, tafiti zilizofanywa na vyanzo mbalimbali ikiwamo Taasisi ya Utafiti, Sera na Uchumi (REPOA) zinaonyesha kwamba masoko ni changamoto kubwa zaidi baada ya mkulima kuwa amezalisha mazao yake.

Changamoto ya masoko ya mazao mbalimbali ya wakulima na hasa ya nje ya nchi ambako sehemu kubwa ya mazao yanayozalishwa yanauzwa inachangiwa na mengi, lakini kubwa yakiwa masuala ya muda na gharama.

Muda na gharama unaotumika kuomba vibali, leseni pamoja na vyeti vya usafi chini ya dirisha moja (single window system) kwa ajili ya kuuza mazao nje ama kuingiza bidhaa kama viuatilifu, mbolea na mbegu.

Kwa kuona changamoto hizo na hasa wakati ambapo Tanzania inalenga kuwa nchi ya viwanda ifikapo 2021 na ya kipato cha kati mwaka 2025, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Trade Mark East Africa, wamezindua mfumo ulio na suluhu dhidi ya changamoto hizo.

Kwa mujibu wa Ofisa Mfawidhi, Huduma ya Karantini na Usafi wa Mimea wa Wizara ya Kilimo, Daniel Katemani, Mfumo huu unaoitwa ATMIS (Agricultural Trade Management Information System), umeasisiwa na Watanzania.

Katemani anabainisha kwamba umekuwa na mafanikio makubwa toka ulipoanza kufanya kazi Mei mwaka huu, ingawaje ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika Maadhimisho ya Sherehe za Nanenane, yaliyofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu.

"Umepunguza muda na gharama kwa wateja wetu na hivyo kuboresha na kurahisisha biashara ya kilimo na ndiyo maana sasa huwezi ukakuta msururu wa wateja pale bandarini, kama ilivyokuwa siku za nyuma," anasema.

Anabainisha kuwa mfumo huu unahusisha taasisi za udhibiti na idara za serikali tano zilizo chini ya wizara ya kilimo ambazo ni pamoja na Sehemu ya Afya ya Mimea (PHS) kama inavyotambulika kwa wafanyabiashara wengi.

"Vilevile Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu (TOSKI), Kituo cha Utafiti na Uratibu wa Viuatilifu (TPRI) Arusha pamoja na Idara ya Usalama wa Chakula chini ya wizara ya kilimo," anasema.

**BODI**

Kwa upande wa bodi zinazohusika katika mfumo huu, ofisa huyo mfawidhi anazitaja kuwa ni Bodi ya Pamba, Bodi ya Sukari, Bodi ya Chai na Bodi ya Mkonge Tanzania.

"Lakini pia Bodi ya Tumbaku, Bodi ya Korosho, Bodi ya Pareto na Bodi ya Kahawa," anasema.

Katemani anafafanua kuwa taasisi, idara na bodi hizo za mazao ambazo ni mamlaka za uratibu zinawezeshwa kupitia mfumo wa ATMIS kupokea maombi na kutoa vibali kwa wafanyabiashara wanapotaka kupeleka mazao nje ama kuingiza bidhaa za kilimo nchini.

"Zamani ukitaka kupata leseni, vibali ama cheti cha usafi ni lazima uende kwenye ofisi za bodi ama taasisi husika, upewe fomu ili ukajaze, upewe namba ya udhibiti (control number) ili ukalipe benki," anasema na kuongeza:

"Kisha urudi kwenye taasisi au bodi husika na fomu yako, uikabidhi hiyo fomu, uambiwe njoo kesho ama kesho kutwa kwa sababu tunaifanyia kazi, kisha ikiwa tayari ndipo ukaichukue."

Anabainisha, michakato yote hiyo ilimgharimu mteja muda na rasilimali za kwenda na kurudi.

"Sasa kama mteja yuko mbali na ofisi husika ilipo ilibidi asafiri... kwa mfano anahitaji kibali cha viuatilifu na yuko Mtwara, ilibidi aende Arusha ambako ndipo zipo ofisi za TPRI," anasema.

Anabainisha kwamba kupitia mfumo huu wa ATMIS, mteja hahitaji kuingia gharama zote hizo bali ni suala la yeye kuingia katika mfumo huo unaopatikana kupitia kompyuta ama simu za mkononi.

"Unatuma maombi yako kwa njia ya mtandao, unajibiwa, unapewa namba ya udhibiti (control namba), unalipa kwa kutumia simu moja kwa moja kwenye mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG)," anasema na kuongeza.

"Njia hii inapunguza muda na gharama," anasema.

**FAIDA KWA SERIKALI**

Kwa upande wa Serikali, Katemani anasema mfumo huu mpya unaongeza mapato ya serikali kwa sababu ya kuondoa kabisa tatizo la vibali feki lililokuwepo hapo nyuma.

"Matumizi ya vibali vya kizamani kwa maana vya kujazwa kwa mkono viliruhusu watu kuvighushi... kuna matukio ya bidhaa toka nchini kukamatwa nje ya nchi hapo zamani lakini vibali vilivyoruhusu usafirishaji wa bidhaa hizo havikuwa halali, vilighushiwa," anasema na kuongeza:

"ATMIS imewekewa udhibiti kiasi kwamba mtu yeyote wa taasisi yoyote ya serikali kama TRA anaweza akaingia ndani ya mfumo na kujiridhisha kama kibali kimetolewa na serikali kwa maana ya taasisi ama bodi husika."

**MKURUGENZI TRADE MARK**

John Ulanga, ni Mkurugenzi wa Trade Mark East Africa Tanzania ambayo imeshirikiana na wizara ya kilimo kuasisi mfumo huu.

Anasema wao kama shirika lisilolenga faida wanashirikiana na wadau, taasisi za serikali kuboresha mazingira ya kibiashara kwa kuhakikisha biashara nchini ikiwamo ya kilimo zinaboreshwa na kufanyika kwa njia rahisi na yenye ufanisi.

"Na ndiyo maana tumetumia takribani Sh. bilioni 1.6 kuhakikisha mfumo huu umeingia sokoni kwa kushirikiana na serikali...tunapata ufadhili kutoka nchi za Uingereza, Norway na Ireland," anasema.

Akizungumzia faida za ATMIS, Ulanga anasema pamoja na faida zingine mfumo unarahisisha upatikanaji wa taarifa za kibiashara zilivyofanyika kwa sababu inakuwa rahisi kuzipata tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

"Kwa mfano serikali inapotaka taarifa kwamba katika kipindi cha mwezi mmoja ni vibali vingapi vimetolewa kwa ajili ya kusafirisha nini, kwa kiasi gani, vyenye thamani ya kiasi gani," anasema na kuongeza:

"Taarifa hizo unaweza ukazipata ndani ya sekunde tu tofauti na ilivyokuwa huko nyuma ambapo ilikuwa inahitaji siku kadhaa kukaa na kufuatilia vibali vya mkono... hivyo inaongeza kasi ya upatikanaji wa taarifa kwa haraka ambazo zinaweza kutumiwa kufanya maamuzi."

Ulanga anasema mfumo huu unaongeza ufanisi katika biashara ya kilimo, hivyo uwekezaji zaidi katika biashara ya kilimo kwa kuwa sasa kinachozalishwa kinalifikia soko kwa urahisi.

**KUAMINIKA**

Faida nyingine anayoitaja Ulanga ambayo imeanza kupatikana kupitia mfumo huu ni kuaminika kwa vyeti vinavyotoka Tanzania nje ya nchi.

"Hii ni kwa sababu vyeti kutoka kwenye mfumo wa ATMIS unaaminika zaidi tofauti na vyeti vilivyokuwa vikitolewa kwa njia ya mkono, ambavyo vilikuwa rahisi kughushiwa," anasema.

**MAFUNZO**

Kwa upande wa mafunzo kwa wadau juu ya mfumo huu, Ulanga anasema walitoa mafunzo kwa wafanyabiashara takribani 300, wakiwamo mawakala wanaofanya biashara ya kupeleka au kuingiza nje mazao na bidhaa.

**TPRI**

Kwa upande wake Nelson Kawishe ambaye ni Ofisa Tehama wa Kituo cha Utafiti na uratibu wa viuatilifu (TPRI) kilichoko Arusha

Inaendelea Uk. 18

## JIELIMISHE

### WHO: SURUA INAENDELEA KUENEA KWA KASI DUNIANI



Chanjo ya kupambana na mlipuko wa surua imetolewa katika kambi ya wakimbizi iliyoko Bunia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo DRC.**PICHA: MTANDAO**

SHIRIKA la Afya ulimwenguni (WHO), linasema kwamba mlipuko wa surua unasambaa kwa kasi duniani na hivyo kuyaweka maisha ya mamilioni ya watu hatarini.

Taarifa ya shirika hilo iliyotolewa wiki iliyopita inasema miezi sita ya mwanzo ya mwaka huu wa 2019, idadi ya visa vya surua vilivyoripotiwa iko juu ikilinganishwa na mwaka 2016.

Aidha, inabainisha kwamba mlipuko wa surua unaleta shinikizo kubwa katika mifumo ya afya na kusababisha magonjwa, ulemavu na vifo.

Taarifa hiyo inafafanua kuwa kwa kulinganisha na wakati kama huu mwaka jana, mwaka huu visa vilivyoripotiwa ni mara tatu zaidi na nchi zilizotajwa kuwa na idadi kubwa ya visa, ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Madagascar na Ukraine.

Hata hivyo WHO inasema visa nchini Madagascar vimepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia kampeni ya dharura ya chanjo iliyofanyika nchi nzima.

Hivi sasa milipuko mikubwa ya surua inaendelea nchini Angola, Cameroon, Chad, Kazakhstan, Nigeria, Ufilipino, Sudan Kusini, Sudan na Thailand.

Mathalani Marekani imeripoti idadi kubwa ya visa vya surua kuwahi kushuhudiwa kwa miaka 25.

Shirika hilo la afya linasema milipuko mikubwa ya surua iko katika nchi zenye kiwango kidogo cha utoaji chanjo sasa au siku za nyuma, hali ambayo imewaacha mamilioni ya watu katika hatari ya kupata ugonjwa huo.

Wakati huohuo WHO imesema milipuko ya muda mrefu inatokea hata katika nchi zenye kiwango kikubwa cha chanjo kitaifa kutokana na kutokuwapo kwa usawa kwenye utoaji wa chanjo hiyo, mapengo katika jamii, maeneo waliko watu na miongoni mwa rika fulani.

Shirika hilo linaonya kwamba kunapokuwa na idadi kubwa ya watu ambao hawajapatiwa chanjo na kukumbwa na surua, basi inaweza kusambaa haraka sana.

WHO inamtaka kila mmoja kuhakikisha chanjo zao zinakwenda na wakati, kwani dozi mbili zinahitajika ili kumlinda mtu dhidi ya ugonjwa wa surua na kuhakikisha wanathibitisha hali yao ya chanjo kabla ya kusafiri.

**HABARI UN**

# Changamoto soko la mazao ya wakulima

Inatoka Uk. 17

anasema mfumo huo umekisaidia kituo kuwa na data za kielektroniki kwa ajili ya wadau kwa maana ya wauzaji na wasafirishaji.

"Kwamba ukitaka kupata taarifa za hawa wadau, unabofya tu unapata kila kitu ikiwamo mahali mteja alipo," anasema.

Aidha anabainisha faida nyingine iko kwa upande wa serikali, taasisi na kwa wakulima.

"Siku za nyuma kulikuwa na uingizaji wa bidhaa feki kwani mfanyabiashara aliweza kuingiza viautilifu vilivyo chini ya viwango, lakini sasa hilo halipo kwa sababu ni rahisi kufuatilia kilichoagizwa kama kinaendana na matakwa ya mkulima," anasema na kuongeza:

"Ina maana mfanyabiashara ataruhusiwa kuingiza viuatilifu vilivyo vya viwango, kwani visivyo na viwango vinarudishwa palepale bandarini."

Kawishe anasema hiyo inawezekana kwa sababu kupitia katika mfumo wanamtaka muigizaji apeleke sampuli ya viatilifu, viingizwe kwenye maabara kama vinakidhi viwango.

"Kama vinakidhi anapewa cheti cha uchambuzi wa sampuli cha kukidhi viwango, ndipo anapata cheti kinachomruhusu kuingiza.. hivyo sasa hivi hakuna njia za panya kama ilivyokuwa huko nyuma," anasema.

Anabainisha kwamba kupitia ATMIS hakuna mkulima atakayepata viautilifu vilivyo chini ya viwango.

**WATEJA**

Mtaalamu huyo anabainisha wateja wakubwa wa TPRI kuwa ni pamoja na bodi zote za mazao na hata serikali kwa sababu kuna wakati hununua viautilifu kwa ajili ya wakulima kama ruzuku.

"Lakini maduka yote yanayouza viualitifu rejareja na yale ya jumla ni wateja wetu, pia waagizaji wote wa viualitifu nchini na kampuni zote za fumigation, viwanda vinavyotengeneza sumu ni wateja wetu.

**WAFANYABIASHARA**

Joseph Baltazari ni mfanyabiashara anayesafirisha nje marobota ya pamba.

## JE, WAJUA?



Nyumbu wakiwa mbuga ya wanyama. **PICHA: MTANDAO**

# Ndege yaanguka baada ya kugonga nyumbu Kenya

KULIKUWA na hali ya hofu baada ya ndege ya kampuni ya Fly Safarilink nchini Kenya, kugonga nyumbu wawili ilipokuwa ikitua katika uwanja wa ndege wa Kichwa Tembo kwenye mbuga ya wanyama pori ya Maasai Mara.

Ndege hiyo nyepesi kwa jina la Dash 8 yenye namba za usajili 5Y- SLM ilihusika katika kisa hicho baada ya nyumbu hao kupita ghafla kwenye barabara ya ndege wakati ndege hiyo ilipokuwa ikitua.

"Tunashukuru kuthibitisha kwamba abiria wote na wafanyakazi wa ndege yetu wako salama na kwamba hakuna majeruhi ama hata watu kufa," ilisema taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo ya ndege.

Ofisa wa Utalii wa Mara Triangle, David Top, alisema kwamba matairi ya ndege hiyo yalitoka na kuifanya ikose mweleko kabla ya kutoka katika barabara yake.

"Ilikuwa majira ya saa 10.30 alfajiri wakati ndege hiyo ilipopata matatizo ya kiufundi na kuwagonga nyumbu wawili," Ofisa huyo alinukuliwa na gazeti la The Standard akisema.

Ijapokuwa hakuna uwanja wa ndege katika mbuga ya wanyama pori ya Mara, kuna viwanja kadhaa vidogo vidogo vya kutua ndege katika mazingira yake ambapo ndege za abiria huwaweka na kuwachukua abiria kabla ya kurudi Nairobi.

Kampuni ya ndege ya Safarilink husafirisha abiria katika viwanja tofauti vya ndege ndogo ndogo kama vile Keekorok, Mara Kaskazini, Musiara, Serena, Angama, Olkiombo na Kichwa Tembo.

Wakati wa msimu mzuri wa Utalii, wanyama hao hutembea kila mahali katika mbuga hiyo ya wanyama pori, wakitafuta lishe karibu na barabara hiyo ya ndege.

Usimamizi wa kampuni hiyo ulisema kwamba ndege hiyo imeharibika na kwamba wahandisi wake pamoja na wafanya kazi wamepelekwa katika eneo la tukio ili kutazama hali ilivyo.

Wakati ilipokuwa ikitua takriban magari 10 yalikuwa yameegeshwa katika eneo hilo huku madereva pamoja na viongozi wa safari wakisubiri kuwabeba abiria na kuwapeleka katika hoteli na kambi za mahema.

***BBC***

# UTAFITI

## MFUMO WA NYOTA NA SAYARI UNAOUNDA DUNIA UMEPINDA

MFUMO wetu wa sayari na nyota, ama falaki, upo katika umbo la upinde na si nyoofu kama ilivyodhaniwa hapo awali, utafiti mpya umebaini.

Njia hiyo ya falaki, maarufu kwa lugha ya Kiingereza kama Milky Way, katika vitabu vyote vya sayansi na taaluma inaonyeshwa ipo katika unyoofu.

Hata hivyo, utafiti mpya wa nyota zing'aazo zaidi kwenye falaki hiyo umebaini kuwa nyota hizo hazipo kwenye njia nyoofu, zimepinda.

Wataalamu wa unajimu kutoka Chuo Kikuu cha Warsaw nchini Poland, wanadhani kuwa nyota hizo zimepinda kutoka kwenye njia nyoofu ikiwa ni matokeo ya kutangamana na falaki nyingine za karibu.

Ramani mpya tatu za falaki ya Milky Way, zimechapishwa kwenye jarida la Sayansi.

Picha maarufu zaidi ya Milky Way ikiwa katika mstari nyoofu imetokana na utafiti wa nyota milioni 2.5 kati ya nyota zipatazo bilioni 2.5 katika falaki hiyo.

"Undani wa kimfumo na historia ya falaki ya Milky Way bado kabisa kujulikana, na moja ya sababu ni kuwa, ni vigumu sana kupima umbali baina ya nyota na maeneo mengine ya mbali ya falaki yetu," anasema Dk. Dorota Skowron kutoka Chuo Kikuu cha Warsaw.

Ili kupata picha ya kihalisia zaidi, Dk. Skowron na wataalamu wenzake walipima umbali wa baadhi ya nyota zing'aazo zaidi kwenye falaki yetu ya Milky Way.

Nyota hizo ni kubwa, na za umri mdogo ambazo hung'aa mara elfu zaidi ya jua. Pia nyota hizo huongezeka ukubwa kwa kiwango cha juu kinachoendana na ung'aavu wake.

Hali hiyo ya ung'aavu na ukuaji wa nyota hizo unawawezesha wataalamu wa anga za mbali kukagua umbali wao kwa ufanisi wa hali ya juu.

Nyingi ya nyota hizo ziligunduliwa kupitia kifaa kifahamikacho kama Optical Gravitational Lensing Experiment (OGLE) kilichopo kwenye eneo la Las Campanas, jangwa la Atacama nchini Chile.

Przemek Mroz, ambaye ni mjumbe wa timu ya OGLE anasema matokeo ya utafiti huo yanastaajabisha.

"Matokeo yetu yanaonyesha kuwa falaki ya Milky Way Galaxy si nyoofu. Imepinda na kukunja kona kutoka kwenye kitovu chake," anasema na kuongeza:

"Kupinda huko kunaweza kuwa kumesababishwa na kutengamana na falaki nyingine ama kukutana na vitu vyeusi (vitu visivyoonekana lakini vipo ndani ya falaki)."

Matokeo hayo ya wataalamu kutoka Poland, yanaendana na matokeo mengine ya utafiti kuhusu nyota hizo ambayo yalichapishwa mwezi Februari na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Macquarie nchini Australia na Taasisi ya Sayansi ya China. ***BBC***



# lapatiwa muarobaini

Anasema kabla ya mfumo huu kuanzishwa changamoto zilizokuwapo zamani zilikuwa ni pamoja na muda wa kupata vibali lakini pia uwapo wa vibali vingi vya kughushi.

"Kupata kibali zamani ilikuwa inaweza ikakuchukua mpaka siku 20...ujaze fomu, upate namba ya udhibiti (control number), uwasilishe nyaraka, uende benki kulipia na taratibu chungu nzima," anasema na kuongeza:

"Sasa usahihi umeongezeka, hakuna suala la kwenda na kurudi, hivyo inaokoa muda na gharama kwa sababu vyote hivyo unaomba kwenye mtandao kupitia mfumo wa ATMIS, unafanyiwa uchambuzi mtandaoni, kisha unafanya malipo yako mtandaoni hata kwa njia ya simu...ni muda mfupi sana."

Anasema mfumo huu umewaondolea muda mrefu wa kusubiri lakini pia gharama za kushughulikia mchakato mzima wa kupata vibali.

"Ninaona kuna nuru kubwa katika biashara ya kilimo nchini na hivyo tija kwa ustawi wa taifa," anasema.



Mkurugenzi wa Trade Mark East Africa Tanzania, John Ulanga, shirika lililoshirikiana na Wizara ya Kilimo kuanzisha mfumo wa ATMIS.

# Kasi ujenzi wa Veta iongezeke kuwatengenezea fursa vijana

**Na Mwalimu Reubeni Lumbagala**

MOJA ya malengo ya Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kuhakikisha kila wilaya inakuwa na Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Lengo ni kuwawezesha vijana na wananchi wa wilaya husika na maeneo mengine ya nchi kupata fursa ya kujifunza stadi mbalimbali za ufundi.

Hivyo, njia pekee ya kutekeleza mkakati huu mzuri ni kuanza mara moja ujenzi wa vyuo vya Veta kwenye wilaya kwa awamu kutokana na upatikanaji wa rasilimali na hasa fedha hadi kufikia lengo hilo la kila wilaya kuwa na chuo cha VETA.

Vyuo vya Veta ni ukombozi kwa vijana wenye ndoto za kuwa na stadi katika fani mbalimbali kama vile ushonaji, upishi, ususi, upambaji, ufundi wa magari, ufundi wa umeme wa majumbani na udereva.

Lakini pia fani kama za kuchomelea, ufundi wa bomba, uhazili, kompyuta, useremala, upakaji rangi, uchoraji, ukerezaji wa vyuma kwa kutaja baadhi.

Vijana wenye nia ya kupata stadi hizo na nyinginezo hawana budi kujiunga na VETA ili kutimiza ndoto zao.

Hivi karibuni, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akiwa mkoani Tabora katika uzinduzi wa chuo cha VETA, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, serikali imetenga Bilioni 40 kwa ajili ya kujenga vyuo vipya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA) katika wilaya 25 hapa nchini.

Mpango huu wa ujenzi wa vyuo vya VETA ni utekelezaji wa dira ya maendeleo ya taifa ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, ni lazima kuandaa rasilimali watu wa kutosha wenye maarifa, ujuzi na stadi.

Katika hafla hiyo, Waziri Ndalichako alisema "Kadri tunavyoongeza vyuo hivi vya ufundi katika wilaya mbalimbali, tunasogeza elimu ya ufundi itolewayo na vyuo vya VETA karibu na wananchi ili kuwawezesha kupata ujuzi na stadi zinazohitajika katika kipindi hiki ambacho nchi yetu inalenga kujenga uchumi wa viwanda kuiwezesha kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025."

Elimu, mafunzo na ufundi ambao vijana wanapata kupitia VETA utawandaa kuhudumia mahitaji ya rasilimali watu viwandani hivyo kupata ajira. Lakini pia, ujuzi huo utawawezesha wahitimu kujiajiri wenyewe na kupunguza tatizo la ajira miongoni mwa vijana wa Kitanzania.



Wanafunzi VETA wakiwa katika mafunzo ya vitendo. **PICHA: MTANDAO**

Elimu na mafunzo yatolewayo VETA ni ya vitendo zaidi kuliko nadharia. Na ndiyo maana wahitimu wa VETA wapo katika nafasi nzuri ya kujiajiri wenyewe kutokana na kupata mafunzo mengi ya vitendo chuoni.

Changamoto ya vijana wengi kushindwa kujiajiri ni kutokana na kuwa na elimu ya nadharia kwa kiwango kikubwa kuliko vitendo, hali inayowafanya kushindwa kumudu mazingira ya kujiajiri.

Utekelezaji wa ujenzi wa VETA kila wilaya ni njia ya kuwafikishia vijana fursa za kujiajiri.

Jambo la msingi ambalo uongozi wa VETA Taifa unapaswa kuzingatia ni kuendelea kuandaa na kuboresha mitaala ili izidi kuwa bora zaidi na inayoendana na wakati ili mafunzo ambayo wanafunzi wanayapata yawasaidie katika maisha yao.

Dunia inabadilika na mahitaji ya soko yanabadilika pia, hivyo ni muhimu uongozi wa VETA kutafiti kozi ambazo zitawasaidia wanafunzi pindi wanapohitimu mafunzo yao.

> Ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, ni lazima kuandaa rasilimali watu wa kutosha wenye maarifa, ujuzi na stadi.

Maboresho ya mitaala ya VETA yazingatie ushirikishwaji wa wadau wote muhimu ili mitaala hiyo ijibu mahitaji ya soko na hatimaye kuleta matokeo chanya kwa wanafunzi.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iendelee kuwashirikisha wadau na wabia wa maendeleo kusaidia ujenzi wa vyuo vya VETA hapa nchini ili kila wilaya ifikiwe na VETA.

Hii itawasaidia wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi na sekondari kupata nafasi za kujiunga na vyuo hivyo kuwaepusha na suala la kubaki nyumbani bila ya kuwa na fani yeyote ya kuwasaidia katika maisha yao.

HALMASHAURI

Vilevile, uongozi wa Halmashauri ambazo zina vyuo vya VETA katika maeneo yao, wawasaidie wahitimu wa VETA kwa kuwakopesha mitaji ya kuanza shughuli za kujiajiri.

Mikopo ya vijana na wanawake inayotolewa na Halmashauri iwafikie wahitimu waliomaliza VETA ili wanunue mashine kwa ajili ya shughuli za fani walizozisomea.

Mathalani, kuwapa mashine za kuchomelea vyuma, kufyatua matofali, vyerehani na nyingine ili waweze kuanza kuzitumia fani walizozisomea.

Hili likifanyika, itawainua vijana waliohitimu kwa kujiajiri.

Taasisi za fedha pia zifanye kazi na VETA kwa kuwakopesha wahitimu mikopo yenye riba nafuu ili kutimiza malengo yao ya kujiajiri na kuchangia pato na maendeleo ya nchi.

VETA ni mkombozi kwa vijana katika suala la kutoa ajira na kusaidia kutimiza dira ya maendeleo ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025.

Muhimu ni kasi ya ujenzi wa VETA iongezeke zaidi, ili vijana wafurahie maisha ya ajira ya uhakika. Tafakari.

***Mwandishi wa Makala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa, mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764 666349.***



# WADAU SABATO KASIKA

**MLUNDIKANO wa wanafunzi katika madarasa bado ni changamoto kwenye baadhi ya shule nchini. Nini kifanyike ili kuimaliza? Wadau wanajadili.**




**MARIAM MJAGA (MKAZI WA JIJINI DAR)**

KWA shule za mijini ni kama zina unafuu kidogo, kwani zina walimu angalau wa kutosha ingawa suala la msingi ni kuongeza vyumba vya madarasa ili kupunguza mlundikano wa wanafunzi. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, baadhi ya shule zimekuwa zikiruhusu wanafunzi kuingia kwa zamu, yaani asubuhi na wengine mchana. Uamuzi huo ni mzuri, lakini ipo haja ya kuboresha mazingira ya sasa. Yaani kufanya kama ilivyo kwa shule binafsi ambazo zina wanafunzi wachache katika madarasa ingawa ni wazazi wachache wenye uwezo wa kumudu gharama za kusomesha watoto wao huko. Umefika wakati sasa serikali kuangalia upya ni wapi tumekwama katika kuboresha elimu na hasa kwenye hili suala la wingi wa wanafunzi katika madarasa na kutafuta mbinu za kulitatua, kwani ni vyema kuwa na elimu inayokwenda na wakati hasa wakati huu ambao dunia imekuwa kama kijiji, siyo tena wanafunzi kulundikana katika madarasa au kukaa chini wakati jamii ipo na inaweza kushirikishwa, ikachangia kutatua changamoto hiyo, ambayo binafsi ninaiona kama iko chini ya uwezo wa Watanzania.



**TELESPHOLI ANISENT (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NI kweli tatizo hilo lipo na kuna haja ya kulimaliza, kwani inawezekana mwalimu akawa na kazi kubwa katika ufundishaji kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi darasani. Yaani unakuta kwenye baadhi ya shule ziwe za msingi au sekondari walimu ni wachache hali ambayo inawafanya wapate shida kufundisha darasa lenye wanafunzi zaidi ya 100. Katika mazingira kama haya si rahisi mwalimu kuelewa tatizo la kila mwanafunzi. Serikali imejitahidi kuongeza shule ili kuhakikisha watoto wanasoma hasa shule za msingi, lakini bado kuna wingi wa wanafunzi, ndio maana unakuta wamejazana chumba kimoja cha darasa na kusababisha hata ufundishaji kuwa mgumu. Kinachotakiwa hapa sasa ni kuongeza vyumba vya madarasa kadri inavyowezekana ili kuwasaidia wanafunzi na walimu pia kuondokana na kero hiyo. Sasa swali la msingi ni kwamba mwenye jukumu la kujenga hivyo vyumba ni nani? Najua wengi wanaweza kusema kuwa ni jukumu la serikali, lakini ukweli ni kwamba shule ni za wananchi. Hivyo wanatakiwa kuzihudumia na pale wanapokwama, serikali iingilie kati kuwasaidia. Hiyo ndio njia pekee itakayosaidia kumaliza changamoto za wingi wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa nchini.




**FATUMA KUSAGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWANZA kabisa mimi ni mdau wa elimu. Ninaamini kwamba hali hiyo itatulia, kwani ni jukumu la kila mmoja wetu kushiriki kwenye maendeleo ya shule. Huo wingi wa wanafunzi madarasani unatokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, hivyo ujenzi wa vyumba hivyo usiachwe kwa serikali tu kwani shule ni zetu wenyewe. Tunashindwa wapi kukaa na kuamua kuboresha shule zetu kupitia kamati za shule au bodi? Serikali imetusaidia kutuondolea michango mbalimbali ambayo kwa kweli ilikuwa ni kero, sasa kwanini na sisi tusifanye sehemu yetu kwa kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa? Ninajua kuwa kuna changamoto ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi na tutambue kwamba serikali inahamasisha vijana wengi kusoma ndio maana ikaondoa ada kidato cha kwanza hadi cha nne. Hatua hii inaweza kusaidia wakife vyuo vikuu, wapate shahada ya kwanza na kuendelea ili waweze kuingia kwenye soko la ajira hasa kwa kuzingatia kwamba elimu ya kidato cha nne na cha sita kwa sasa haina nafasi. Lakini kama kuna makosa madogo madogo, hayo ni ya kawaida tu na serikali inaendelea kuweka mambo sawa. Hivyo ni wajibu wetu kuunga mkono juhudi hizo ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa na sio kubeza kila kitu hata kama kuna mazuri yanayofanywa.



**MILKA PHINIAS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

CHANGAMOTO za wanafunzi kulundikana katika madarasa zisitukatishe tamaa kwani ziko chini ya uwezo wetu. Kinachotakiwa ni kutambua kuwa tuna mchango mkubwa kwa maendeleo ya shule. Elimu yetu inakidhi haja, kwani kwa sasa kila mtoto anaweza kwenda shule na pia wengi wanafaulu kwenda sekondari, tofauti na miaka nyuma ambapo ni wachache tu walikuwa wakichaguliwa. Hata wale ambao hawakubahatika kusoma nao sasa wanasoma katika madarasa ya MEMKWA. Ninajua kuna changamoto katika kufundisha wanafunzi waliojazana darasani, kwani hakuwezi kuwa na usikivu. Lakini kwa kuwa hayo ndio mazingira yetu, basi tuangalie jinsi ya kuyatatua ili kuboresha elimu na kuwapa walimu unafuu wa kufundisha. Mpango wa utoaji elimu bila malipo unaotekelezwa na serikali ya awamu ya tano umekuwa na faida ya kusaidia wanafunzi wengi kupata elimu. Changamoto kubwa ya mlundikano wa wanafunzi madarasani, inatakiwa kupatiwa ufumbuzi kwa kushirikisha wadau wote wa elimu ili kutoa mchango wao wa maoni badala ya kudhani kwamba jukumu hilo ni la taasisi fulani tu au kwamba jamii haihusiki. Hebu firikia, kuna shule moja kule Tanga iliripotiwa na vyombo vya habari kwamba wanafunzi 160 wamekuwa wakilazimika kukaa darasa moja jambo ambalo limekuwa kero kwa walimu kufundisha na kumfikia kila mwanafunzi.



**RAFIKI WILSON (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KAMA kweli tunataka kufanya mapinduzi kwenye elimu, basi tuhakikishe tunaboresha shule zetu bila kusukumwa, kwani elimu ya Tanzania inakabiliwa na changamoto nyingi siyo hizo tu za wanafunzi kulundikana katika madarasa. Walimu wao nao wana malalamiko kwamba wengine wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hakuna ubishi kuwa hali hiyo inaweza kusababisha elimu yetu ikakosa mwelekeo kutokana na kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa vifaa vya kufundishia na hata wanafunzi kukaa chini. Elimu tulionayo tunaweza kuivusha hapa ilipo na kwenda mbele iwapo tutaacha siasa kwamba tumefanikiwa wakati bado tuna safari ndefu ya kufikia mafanikio. Serikali ina sehemu yake katika changamoto za shule na walimu kwa ujumla, na jamii nayo ina sehemu yake, hivyo nguvu zote zikiunganishwa, nina uhakika wanafunzi hawataludikana madarasani na wala hawatakaa chini. Hivyo wito wangu ni kwamba tutafute kila njia kuhakikisha walimu na wanafunzi wanaepukana na changamoto hizo ingawa inawezekana zisiishe, lakini wakawa na unafuu kuliko hali ilivyo sasa ambayo inaweza kukatisha tamaa. Wanafunzi kulundikana darasani ni dalili mojawapo za kurudi nyuma badala ya kwenda mbele.





# Wafugaji wamkuna RC kuchangia maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameeleza kufurahishwa na namna wafugaji wanavyojitolea kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

Aliyasema hayo wakati wa ziara ya kukagua miradi mbalimbali ambayo itazinduliwa wakati wa mbio za Mwege wa Uhuru, aliyoitembelea mwishoni mwa wiki akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa pamoja na baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Chunya.

Akiwa katika Kata ya Kambikatoto alikagua nyumba ya walimu katika Shule ya Kambikatoto ambayo itakuwa inatumiwa na familia mbili za walimu na wafugaji wakachangia Sh. milioni 3.3 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba hiyo. Aliwapongeza kwa juhudi wanazozifanya katika kuhakikisha wanaboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa walimu na kwamba hali hiyo inatia moyo watumishi kwa kuwafanya wasijute kupangiwa vituo vya kazi kwenye maeneo hayo.

"Nawashukuru sana ndugu zangu wafugaji, hakika mlichokifanya ni fundisho kwa watu wengine, serikali haiwezi kufanya kila kitu kwa wakati mmoja na badala yake inafanya kwa awamu, mlichokifanya hapa hakiwezi kusahaulika," alisema Chalamila.

Pamoja na kuwapongeza pia aliwataka kuzingatia maagizo ya serikali ikiwamo kulinda mazingira kwa kutoingiza mifugo kwenye misitu ya hifadhi na badala yake waichunge kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahudi, alisema serikali wilayani humo imetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuchungia mifugo ili kuepuka mwingiliano wa shughuli za uzalishaji.

Alisema utaratibu huo umesaidia kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na kwamba wanaendelea kutoa elimu ili wafugaji wayatumie maeneo waliyotengewa.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, inaendelea na ukaguzi wa miradi mbalimbali itakayozinduliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru ambao unatarajiwa kuingia mkoani hapa mwanzoni mwa Septemba mwaka huu.

# Wananchi wajichanga kujenga kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAKAZI wa Kata ya Lufilyo kwenye Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, wamechangishana zaidi ya mifuko 160 ya simenti kujenga kituo cha afya cha kata hiyo, kuondoa adha ya kufuata huduma za afya kwa umbali mrefu.

Simenti ilikusanywa kwenye harambee maalumu iliyoitishwa na Diwani wa Kata hiyo, Lucas Mwamafupa na kuwahusisha wakazi na wazawa wa Lufilyo wanaoishi maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza baada ya harambee hiyo, Mwamafupa alisema wanaendelea na ujenzi wa kituo hicho ambacho kinajengwa katika makao makuu ya kata hiyo na kwamba tayari wameshatumia Sh. milioni 25 kujenga jengo moja.

Alisema mbali na mifuko 161 waliyoipata kwenye harambee hiyo pia walipata fedha taslimu Sh. 9,000,000 ambazo alisema zitasaidia kuendeleza ujenzi.

**Wananchi hao wameonyesha kuiunga mkono serikali kwa vitendo, hivyo ni lazima waungwe mkono kwa kusaidiwa pale wanapokwama.**

"Tunawashukuru wale wote waliotuunga mkono kwa kutuchanga kwenye hii harambee ambayo naamini imetusukuma sana, hatutaishia hapa tutaendelea kuchangishana mpaka tuhakikishe tunakamilisha ujenzi," alisema Mwamafupa.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe ilipo kata hiyo, Mnkondo Bendera, ambaye ndiye aliongoza harambee hiyo aliwaasa wananchi kuepuka kuingiza siasa kwenye mradi huo badala yake waendelee kushikamana ili kufikia malengo.

Alisema wananchi hao wameonyesha kuiunga mkono serikali kwa vitendo, hivyo ni lazima waungwe mkono kwa kusaidiwa pale wanapokwama.

Alisisitiza kuwa serikali inapambana kuhakikisha inaimarisha huduma muhimu za jamii ikiwamo afya, ili kupunguza vifo vya wananchi na hivyo akawashukuru wananchi hao kwa kusaidia kutekeleza malengo ya serikali.

"Naamini kuwa mmekubaliana kwa moyo mmoja kujenga kituo hiki ili kiwasaidie kutibiwa na msiweze kufa, hivyo nawaomba mwendelee kushikamana kwa kuepuka siasa chafu ambazo zinaweza zikawakwamisha msifanikiwe," alisema Bendera.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam ambaye ni miongoni mwa walioshiriki harambee hiyo, Lusubilo Mwakabibi, alisema alishiriki ili kuwaunga mkono ndugu zake kwa maelezo kuwa yeye pia ni mzaliwa wa eneo hilo.

Alisema Rais Magufuli, anawapenda wananchi wanaopenda maendeleo na ndiyo maana hata yeye anafanya shughuli nyingi kwa ajili ya manufaa ya wananchi wote bila kujali itikadi zao za kisiasa.

Aliwataka wananchi hao kuendelea kujitolea kama wanavyojitolea kutoa sadaka zao makanisani na misikitini, huku akisisitiza kuwa kituo hicho kitakuwa ni alama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Murangi iliyopo katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, wakipalilia bustani ya nyanya, walipokuwa katika somo la Stadi za Kazi kwa vitendo, shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wahitaji wahimizwa kujiunga na vikundi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) ambao ni wajasiriamali kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe, wameshauriwa kujiunga kwenye vikundi ili wanufaike na mikopo ya halmashauri inayotokana na mapato ya ndani.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kufunga mafunzo maalumu ya kutambua bidhaa zenye ubora kwa viziwi yaliyoandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Katika mafunzo hayo wadau wakiwamo Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) na Kituo cha Uwekezaji (TIC), walikuwapo.

Mkwawa alisema kwa sasa watu wenye ulemavu wanashirikishwa kwenye shughuli za maendeleo, ambapo alisema imetungwa sheria kwa ajili ya kusimamia mikopo kwenye makundi maalumu likiwamo la walemavu.

Aliwapongeza maofisa wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa kuamua kuwasaidia viziwi, huku akiwataka kuendelea kutoa elimu hiyo kwa makundi mengine ya walemavu ili yote yanufaike na elimu hiyo muhimu.

"Mafunzo haya yamekuja katika muda mwafaka ambao serikali inasisitiza kuingia kwenye uchumi wa viwanda, sasa tumieni vyema fursa hii kuzalisha bidhaa bora ambazo zitawaondolea umaskini kwa kuuzwa hata nje ya nchi," alisema Mkwawa.

Alizishauri halmashauri kuepuka kuvikopesha vikundi vya wajasiriamali fedha taslimu na badala yake zikopeshe vifaa kwa madai kuwa uzoefu unaonyesha vikikopeshwa fedha zinaishiwa kuliwa badala ya kufanya kazi iliyokusudiwa.

Akizungumzia mafunzo hayo, Msimamizi wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonda, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha viziwi kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuitambua nembo ya ubora ya shirika hilo.

Alisema awali walikuwa wanatoa mafunzo hayo kwa makundi ya watu wa kawaida wasiokuwa na ulemavu, lakini kwa sasa wameanza kuyatoa kwa makundi ya walemavu baada ya kubaini kuwa baadhi yao ni wajasiriamali kama walivyo watu wa kawaida.

Alisema kwa sasa wameanza na kundi la walemavu wa kusikia na baadaye wataendelea na makundi mengine ya walemavu na kwamba mafunzo hayo yatakuwa yanatolewa kwa awamu tofauti tofauti.

Mwakasonda alisema kutokana na hali za baadhi ya watu wenye ulemavu, wanakusudia kuanza kuwafuata kwenda kutoa mafunzo kwenye wilaya mbalimbali badala ya kuwataka wasafiri kwenda Mbeya ambako ndio Makao Makuu ya Kanda.

"Kwa sasa tunatoa mafunzo haya kwa makundi ili kujua kwamba kuna mafanikio ama la tutaanza kufuatilia kwenye maeneo yao, lakini kwa hawa wenzetu wamefurahia mafunzo maana tulikuwa na wakalimani wa lugha za alama," alisema Mwakasonda.



# Msajili azipa angalizo NGO zisizosajiliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MSAJILI wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO), Vickness Mayao, amesema baada ya muda wa usajili kumalizika kwa mujibu wa sheria, shirika ambalo litakuwa halijasajiliwa litakuwa limejifuta ifikapo Agosti 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Sheria ya NGO Namba 24 ya Mwaka 2002 ambayo ilifanyiwa marekebisho chini ya Sheria Na. 3 ya Mwaka 2019, mashirika yanayotakiwa kusajiliwa ni yanayoendesha shughuli za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, utawala bora, haki za binadamu na mazingira katika ngazi ya jamii kwa lengo la kutogawana faida ambazo hazina mlengo wa kukuza biashara.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mayao alisema hadi sasa mashirika hayo yameongezeka kutoka 404 mwaka 2005 hadi 9,310 mwaka huu, huku mashirika 158 yakiwa yameondolewa kwenye daftari la msajili huyo.

**Kwa mfano kule Brela ukiingiza taarifa zako inaonyesha ifikapo Agosti 30, kampuni au shirika halitakiwi kuwa kwenye mfumo wao kwa sababu masharti ya sheria ya Brela haitambui.**

Alisema kwa mujibu wa sheria, wamepewa miezi miwili kuanzia Julai 10 hadi Agosti 30 kuhakikisha kila shirika liko kwenye sheria inayotakiwa na kwamba kwa yale ambayo hayatakuwa yamesajili kwa kipindi hicho, yatakuwa yamejifuta.

"Sheria imeweka bayana muda wa kuisha. Kila shirika linatakiwa kuwa kwenye sheria yake bila kufanya hivyo watakuwa wamejifuta. Tumefanya usajili katika kanda tano na sasa tumerudi makao makuu hapa Dodoma kuanzia kesho (leo) hadi Agosti 27 ndiyo itakuwa mwisho," alisema.

Alisema zoezi la usajili kwenye kanda lilihitimishwa Agosti 17 na kuamua kutoa fursa kwa mashirika ambayo hayakusajili kwa sababu mbalimbali kufika Dodoma kuanzia leo hadi Agosti 27, mwaka huu.

"Usajili huu unawahusu wale ambao wanahama kutoka kwenye sheria mbalimbali walizosajili mashirika yao awali kama sheria ya jumuiya ya kampuni na wadhamini, wanatakiwa kurudi kwenye sheria inayowahusu ya mashirika yao," alisema.

Mayao alifafanua kuwa kwa sheria hiyo mashirika ya kijamii ambayo awali yalisajiliwa chini ya sheria nyingine kama Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (Brela), Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) na Sheria za Asasi za Kijamii, yanatakiwa kusajiliwa kwenye ofisi ya mashirika hayo.

Kuhusu usahjili wa mashirikia hayo ambao unaelekea mwisho, Mayao alisema hadi sasa wamesajili kwa asilimia 85.

"Kwa mfano kule Brela ukiingiza taarifa zako inaonyesha ifikapo Agosti 30, kampuni au shirika halitakiwi kuwa kwenye mfumo wao kwa sababu masharti ya sheria ya Brela haitambui," alisema.

Alitoa wito kwa wadau wote wa mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo bado hayajasajili kutumia muda huo wa nyongeza kufika ofisi za msajili Dodoma kwa ajili ya kujisajili.

# DC ataka wananchi wanaokata miti kupanda

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

MKUU wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, amewataka wananchi wanaokata miti ovyo kupanda mingine ili kuondokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki wilayani hapa alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru.

Alisema wananchi wanapokata miti ni vyema wakapanda ili kutoathiri mazingira ya wilaya hiyo.

Mkuu huyo alisema upandaji miti katika maeneo mbalimbali ni jambo muhimu kwa sababu linasaidia kutunza mazingira ya sehemu husika.

"Naomba mjifunze kutunza mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yanayowazunguka. Ardhi ni utajiri mkubwa ikitunza vizuri," alisema na kuongeza kuwa hivi sasa kila mmoja anapaswa kuwa balozi wa mwenzake katika upandaji miti jambo ambalo litasaidia Kondoa kuwa ya kijani.

Naye Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, alisema serikali inasisitiza suala la utunzaji mazingira ili kuondokana na mabadiliko ya tabia nchi.

"Hakuna sababu ya wananchi kwenda kinyume cha agizo la serikali kwenye utunzaji mazingira na ukiona mtu anaharibu mazingira unapaswa kumwelimisha ili ajue madhara ya uharibifu wake," alisema.

Katika mbio hizo wilayani Kondoa, mwenge huo umezindua miradi sita yenye thamani ya Sh. milioni 922 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, huku ikizindua mingine ya idadi hiyo katika Halmashauri ya Mji Kondoa yenye thamani ya Sh. milioni 998.




Mwendesha pikipiki akiwa amebeba mzigo kupita kiasi katika eneo la Ipagala, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kuwaruhusu watoto wa kike wasome

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

WAZAZI na walezi wametakiwa kutoa nafasi kwa watoto wa kike ya kupata elimu badala ya kukatisha ndoto zao na kuamua kuwaozesha.

Wito huo ulitolewa jana na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, wakati wa kuzindua mradi wa umaliziaji wa maboma ya madarasa manne katika Shule ya Sekondari ya Mundemu, wilayani humo.

Alisema watoto wa kike wana haki ya kupata elimu kama watoto wengine.

"Nimekagua ujenzi huu nimeridhika nao pamoja na kasoro chache nilizoziona ambazo zinarekebishika naomba nitamke kuwa Mwenge wa Uhuru mwaka 2019 umekubali kuzindua mradi huu," alisema Mkongea.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, aliwashukuru wananchi kwa ushirikiano walioonyesha wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

"Mafanikio tunayoyapata yanatokana na ushirikiano wa wananchi na ushirikiano uliopo baina yetu sisi watumishi. Tukuahidi kufanyia kazi maelekezo yote," alisema Munkunda.

Awali, akisoma taarifa ya mradi huo, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mundemu, Reuben Chimbwi, alisema ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 na umegharimu Sh. milioni 80.

Mbali na kuweka jiwe la msingi katika shule hiyo, Mwenge wa Uhuru 2019 uliweka jiwe la msingi katika ujenzi wa barabara ya km 2.3 katika mji wa Bahi ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Rais John Magufuli wakati wa kampeni 2015.

Pia liliwekwa jiwe la msingi kwenye mradi wa usambazaji maji kijiji cha Mkakatika na kutembelea ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Bahi.

Aidha, Mwenge huo ulitembelea mradi wa utunzaji wa chanzo cha maji ya uhifadhi wa msitu wa Chenene ulioko kijiji cha Mayamaya pamoja na kuweka jiwe la msingi mradi wa kuzalisha kokoto ulioko chini ya kampuni ya KASCCO.

**Mafanikio tunayoyapata yanatokana na ushirikiano wa wananchi na ushirikiano uliopo baina yetu sisi watumishi. Tukuahidi kufanyia kazi maelekezo yote.**



# ‘Waandishi andikeni habari za kuibua matatizo’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuandika habari za uchunguzi na jinsia ili kusaidia kuibua matatizo mbalimbali katika jamii.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Vyombo vya Babari Kusini mwa Afrika (Misa-Tan), Sengeyuva Gasirigwa, wakati akitoa mafunzo ya habari za uchunguzi na jinsia kwa waandishi wa habari Zanzibar.

Alisema kuwa habari hizo zinasaidia kuibua na kugusa matatizo ya watu mbalimbali hasa wenye uwezo mdogo hivyo waandishi wa habari kujikita zaidi kuandika habari hizo.

Alisema baadhi ya watu hutumia mali za umma katika kujipatia kipato na kujinufaisha wao binafsi huku jamii ikiwa na changamoto mbalimbali.

“Ni vyema kuyafanyia kazi mafunzo haya tunayowapatia ili kufichua matatizo mbalimbali hasa yanayowapata wanawake na watoto ikiwamo masuala ya udhalilishaji,” alisema.

Aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha wanawawekea ulinzi mzuri waandishi wa habari kwa kuwa wamezungukwa na maadui hasa pale wanapoandika habari za uchunguzi.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Salome Kitomari, alisema habari za uchunguzi zinahitaji umakini ili unachokiandika kiwe na ukweli na usahihi.

Aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha wanatoa taarifa zinazoigusa jamii ili kuwasaidia changamoto zinazowakabili kutatuliwa na mamlaka husika badala ya kupaza sauti zao.

Kwa upande wao waandishi wa habari walioshiriki mafunzo hayo wameahidi kuwa watayafanyia kazi mafunzo hayo ili kuleta maendeleo.

# Umri wakwamisha kesi za udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KITENDO cha baadhi ya watuhumiwa kurudisha umri nyuma ili waonekane kuwa wapo chini ya umri wa miaka 18 ni moja ya kikwazo katika kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Kaskazini Unguja, Makame Mshamba, alisema baadhi ya watuhumiwa wa kesi hizo wamekuwa wakifoji vyeti vya kuzaliwa na kurudisha umri ili wasitiwe hatiani.

Aliyasema hayo katika kikao cha kujadili udhalilishaji wa kijinsia kilichoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) Ofisi ya Zanzibar, alieleza kuwa kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya Zanzibar ya mwaka 2011, mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 anaekinzana na sheria huwa hapewi adhabu ya kifungo na badala yake hupelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia (Tai).

Alisema watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji wenye umri wa miaka 19 hadi 25 hutumia mwanya huo na hufoji vyeti vya kuzaliwa ili waonekane kuwa bado ni watoto.

**Tunapoletewa kesi za udhalilishaji wa kijinsia kutoka polisi baada ya kukamilika kwa uchunguzi wake kwa kiasi kikubwa huwa hazijakamilika na ndiyo maana tunazifuatilia zaidi kwa kutaka kujua mambo ya ziada.**

Alisema kitendo cha baadhi ya madaktari kukataa kutoa ushahidi mahakamani ni moja ya kikwazo kwa kesi hizo za udhalilishaji wa kijinsia kushindwa kusikilizwa kwa wakati.

Mshamba alisema madaktari wamekuwa wakisumbua huku wakikataa kufika mahakamani wakati wanapoitwa kwa kutoa ushahidi kwa mtu aliyefikwa na tukio la udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo kubakwa au kulawitiwa.

Alisema hilo ni kosa kwa mtu anapoitwa mahakamani na kukataa wito na inachukuliwa ni sawa na kukwamisha juhudi za mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake.

“Madaktari wanatusumbua sana katika uendeshaji wa kesi zetu kwa sababu wao wamefanya kazi ya uchunguzi kwa muathirika sasa wanaitwa waje wathibitishe kazi yao, lakini hawataki,” alisema.

Alisema zipo baadhi ya kesi zimekwama kwa sababu ya kushindwa kupatikana kwa ushahidi kutoka kwa madaktari waliofanya kazi ya kupima mtu aliyedhalilishwa.

Naye Ofisa kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Rashida Ahmed, alisema baadhi ya kesi zinazoletwa kutoka katika Jeshi la Polisi uchunguzi wake kwa kiasi kikubwa huwa haukamiliki huku ukiacha maswali mengi ya msingi yanayotakiwa kufanyiwa kazi.

“Tunapoletewa kesi za udhalilishaji wa kijinsia kutoka polisi baada ya kukamilika kwa uchunguzi wake kwa kiasi kikubwa huwa hazijakamilika na ndiyo maana tunazifuatilia zaidi kwa kutaka kujua mambo ya ziada,” alisema.

Taarifa fupi ya uchunguzi wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia iliyofanywa na Tamwa imebaini kwamba matukio hayo yamekuwa yakiongezeka ikiwamo ubakaji na ulawiti kwa watoto wa kiume na wanawake.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akimwapisha Khadija Khamis Rajab kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, Ikulu Mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# RC awataka walimu kutumia nafasi zao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka walimu kutumia nafasi zao kupinga na kukemea vitendo vya udhalilishaji ili kupata jamii iliyo bora.

Akifungua mkutano wa tisa wa Chama cha Ushirika wa Maendeleo ya Walimu (TDS) katika Shule ya Sekondari Haile Selassie Mjini Zanzibar, alisema kufanya hivyo pia kutaimarisha ustawi wa jamii na maendeleo nchini.

Alisema katika baadhi ya shule kumejitokeza makundi ya wanafunzi wanaoshiriki katika vitendo viovu vikiwamo vya mapenzi ya jinsia moja jambo linalopaswa kufanyiwa kazi kwa pamoja kati ya walimu, wazazi na serikali.

“Ni lazima tuwe na mkakati wa pamoja kuvidhibiti vitendo hivi kwa kuwa mbali ya kuwa ni kinyume cha maadili yetu, vina madhara makubwa katika jamii,” alisema Ayoub.

Alipongeza uamuzi wa kuanzisha chama hicho kwa kuwa kinasaidia kukuza uchumi na maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Alisema uimara wa chama hicho utachochea kasi ya maendeo ya walimu na elimu nchini na kuwataka walimu kujiunga kwa wingi ili kuongeza uwezo wa chama hicho kuwahudumia wanachama wake.

“Niungane nanyi kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuifanyia marekebisho Sheria ya vyama vya ushirika ambayo inatoa mwanya kwa vyama kama vyenu kujitanua na kuwa na uwezo mkubwa zaidi kwa kuwekeza katika maeneo,” alisema Ayoub.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya ushirika ambaye pia ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika Zanzibar, Khamis Daudi Simba, aliwakata wanachama na viongozi wa ushirika huo kuzingatia sheria na kanuni za vyama vya ushirika ili kuendeleza chama chao.

“Mwaka jana serikali imepitisha sheria mpya ya vyama vya ushirika, hivyo ipo haja ya kila mmoja wenu kuielewa sheria hiyo ambayo inatoa nafasi ya vyama kama chenu kuendelea zaidi,” alisema Simba.

Akizungumza kwa niaba ya Chama cha Walimu Zanzibar (ZATU), Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Salim Ali Salim, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu na ualimu jambo ambalo litapunguza changamoto za walimu nchini.

“Tunamshukuru kwa dhati Rais wa Zanzibar kwa kudumisha amani na utulivu nchini, lakini pia kuiimarisha sekta ya elimu jambo ambalo limeongeza ari ya walimu na wanafunzi na matokeo yake yameanza kuonekana,” alisema Mwalim Salim.

Awali akisoma risala kwa niaba ya wanachama wa ushirika huo, Mwalimu Aley Rashid, alisema ushirika huo ulioanzishwa mwaka 2002 umekuwa kimbilio la walimu ambao hutoa mikopo ya aina mbalimbali ikiwamo ya kujiendeleza kimasomo kwa wananchama na watoto wao.

HABARI KITAIFA

# Mwenyekiti CCM awatega wataalamu kujitathmini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Thomas Myonga, amesema hoja na malalamiko yanayotolewa na madiwani dhidi ya wataalamu katika vikao vya Baraza la Madiwani, wataalamu wanaweza kujitathmini kwa kuangalia kama wanafaa kuendelea kuwapo kwenye eneo hilo au hawastahili.

**Hoja zinazotolewa na madiwani katika vikao vya Baraza la Madiwani, wataalamu wanaweza kujipima kwani hatopenda mtaalamu kulalamikiwa katika eneo lake.**

Myonga alisema hoja zinazotolewa na madiwani katika vikao vya Baraza la Madiwani, wataalamu wanaweza kujipima kwani hatopenda mtaalamu kulalamikiwa katika eneo lake.

Aliyasema hayo juzi katika kikao cha baraza hilo la Halmashauri ya Ushetu baada ya kusikitishwa na wataalamu wa halmashauri kushindwa kutoa maelezo mazuri kwa madiwani wakati wakiuliza utekelezaji wa miradi katika maeneo yao.

"Inashangazwa serikali inatoa fedha, lakini zinaenda kukaa benki miradi inasimama, hivyo hatutaki kutukanwa na wananchi kwenye majukwaa sababu ya uzembe wa wataalamu... turekebishe mifumo kwenye vichwa vyetu ili tuweze kwenda kuwahudumia wananchi," alisema Myonga.

Diwani wa Nyakende, Doa Limbu na Diwani wa Viti Maalum, Pili Sonji, walihoji kwanini mfuko wa jimbo uendelee kuwa na dosari, wakati kuna miradi 41 katika halmashauri yote baadhi ya majengo hayajakamilika na mafanikio ya fedha za mfuko huo zimefikia asilimia 62.

Diwani Limbu alisema kuwa kupitia mapato ya ndani bajeti ya maendeleo ya miradi 41 ilitengwa kiasi cha Sh. bilioni 1.2 ikiwa fedha zilizotumika ni Sh. milioni 484 na iliyopokelewa ni Sh. milioni 683 zaidi ya Sh. milioni 700 haikukusanywa ili kufanikisha miradi hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Juma Kimisha, alisema kuwa asilimia 40 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ziwe zinaenda kama ilivyoazimia pia kwa kuanza na robo ya kwanza ya mwaka miradi iliyopo kwenye bajeti ikamilishwe yote.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Athanas Lucas, alikubali mapendekezo yaliyotolewa ndani ya Baraza la Madiwani, na atahakikisha wanajipanga na ofisa mipango kuona miradi gani inayokuwa kwenye bajeti sambamba na fedha za mfuko wa jimbo.



Wananchi wa Kitongoji cha Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam, wakifua nguo kisimani jana, kutokana na kutokuwapo kwa majisafi na salama katika maeneo wanayoishi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi yaomba ushirikiano wa wadau kukabili uhalifu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JESHI la Polisi Mkoa wa Tabora, limewataka wadau kushirikiana nao kwa kuwafichua wahalifu ili kukomesha tatizo hilo.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa, wakati wa kikao cha wadau mkoani humo.

Alisema polisi pekee yao hawawezi kumaliza uhalifu bila kupata ushirikiano wa wadau mbalimbali wakiwamo wakazi wa Tabora, viongozi mbalimbali wakiwamo wa kiroho.

Mwakalukwa alisema wahalifu wapo ndani ya jamii na wakati mwingine baadhi ya wanajamii wasio waaminifu ndio huficha taarifa za wahalifu na wakati mwingine hawajitokezi kutoa ushahidi pindi wahalifu wanapokamatwa.

Alisema endapo jamii itakuwa mstari wa mbele wa kusaidia kufichua wahalifu na maeneo yao na washirika wao na kutoa ushahidi, tatizo hilo litakwisha mkoani humo.

Aidha, kamanda huyo alitoa wito kwa viongozi wa kisiasa na kiroho kusaidia kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kushiriki katika kukomesha tatizo hilo kwa kutoa taarifa zitakazosaidia kukamata.

Alisema baadhi ya uhalifu unaofanyika mkoani humo yakiwamo mauaji kwa imani za kishirikina na wivu wa mapenzi, yanahitaji zaidi elimu kutoka kwa viongozi wa kiroho ili kuondoa tatizo hilo.


ITV

JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA WANAKIKUNDI CHA MAZINGIRA KUTOKA KIGAMBONI TUINUANE GROUP WAKIJIENDELEZA KWA KUNUNUA BAJAJ AINA YA TOYO MAALUM KWA UZOAJI TAKA KATIKA MITAA MBALIMBALI YA KIGAMBONI.


# Wazazi, walezi wakumbushwa malezi ya watoto

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI na walezi wamekumbushwa kutohangaikia maisha na kusahau na kuweka pembeni malezi kwa watoto wao, bali watenge muda wa kukaa na kuzungumza nao ili kujua matatizo yanayowakabili ya kuyatafutia ufumbuzi.

Hayo yalisemwa juzi na mtaalamu wa masuala ya kijinsia, kijamii na maendeleo kutoka Taasisi ya Kuwezesha Wanawake na Kulinda Watoto ya Ekama Development Foundation Tanzania (EDF), Mary Nsemwa.

Mtaalamu huyo alikuwa akizungumza katika mkutano wa kuwasilisha matokeo ya tathmini na mbinu zinazotumiwa na vikundi vya wanawake vya wilaya ya Temeke na Kigamboni Dar es Salaam, katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto.

Vikundi hivyo vinajishughulisha na kazi ya kuzuia vitendo vya ukatili nyumbani na shuleni chini ya taasisi hiyo, kwa lengo la kuhakikisha watoto wote katika wilaya hizo wanakuwa salama.

Alisema baadhi ya wazazi na walezi hawakai na kuwasikiliza watoto wao badala yake wanasingizia kutingwa na shughuli nyingi, hali ambayo watoto wanaweza kufanyia vitendo vya ukatili bila wao (wazazi) kujua.

"Suala la kujitafutia riziki ni la muhimu, lakini malezi kwa watoto pia kwa ajili kupunguza vitendo vya ukatili kwao, hivyo pamoja na majukumu hayo, ni muhimu kutenga muda wa kuwasikiliza watoto," alisema Nsemwa.

Alisema watoto wanakumbana na changamoto nyingi nyumbani, mitaani na hata shuleni, na wanatakiwa kuzifikisha kwa wazazi, wanashindwa kwa vile hawawaoni wazazi wao na hivyo huamua kukaa kimya.

"Wanaweza kufanyiwa vitendo vya ukatili na wafanyakazi wa ndani, ndugu, majirani au hata walimu na wanafunzi wenzake kwa wale ambao wako shule. Hayo yote wazazi wanatakiwa kuyajua mapema na kuyazuia," alisema.

Alisema wakati umefika sasa kwa wazazi kutimiza majukumu ya malezi kikamilifu, na kubwa zaidi likiwa ni kutenga muda wa kukaa na kuwauliza watoto wao wana matatizo ili wayatafutie ufumbuzi.

Alikuwa akizungumza kwenye mkutano wa kuwasilisha matokeo ya tathmini na mbinu zinazotumiwa na vikundi vya wanawake wilayani Temeke Dar es Salaam, katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto.

"Kimsingi malezi ni uangalizi wa karibu wa wazazi kwa watoto wao, kiafya, kiakili, kitabia na hata kiroho, hivyo wazazi wakisaidiana katika malezi ya watoto hasa kuwa nao karibu na kuwasikiliza itasaidia kwa kiasi kikubwa kugundua changamoto zinazowakabili," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

## Rais atangaza hali ya dharura nchini mwake

**NDJAMENA, Chad**

RAIS wa Chad, Idriss Deby ametangaza hali ya dharura kitaifa katika majimbo mawili ya mashariki nchi humo baada ya kutokea kwa mapambano ya wenyewe kwa wenyewe yaliyosababisha idadi kubwa ya vifo.

Rais Deby alichukua mamlaka hayo baada ya mapigano huko mashariki mwa Chad kati ya wakulima na wafugaji ambayo yalisababisha vifo vya watu takribani 50.

Kiongozi huyo pia alisema serikali itapeleka vikosi vya jeshi kuhakikisha usalama kwenye eneo hilo

Taarifa kutoka ofisi ya rais ilieleza kuwa hali ya dharura kitaifa itakuwapo kwa muda wa miezi mitatu katika maeneo ya Sila na Ouaddai mahala ambapo watu 50 walifariki tangu Agosti 9 katika mapigano kati ya wafugaji na wakulima.

Rais Deby alieleza akiwa safarini kuelekea Sila kwamba serikali yake itapeleka vikosi vya jeshi ambavyo vitakwenda kuhakikisha usalama wa watu katika eneo hilo. Pia alisema lazima raia wote watue silaha zao chini.

Sila ni eneo lililopo mashariki mwa Chad na kwamba lipo kwenye mzunguko wa ghasia kati ya wafugaji ambao wengi ni kutoka kundi la kabila la Zaghawa mahala ambapo Deby anatokea na baadhi ya wakulima wanatoka jamii ya Ouaddian.

Ukame na ongezeko la watu vimechangia mzozo kwenye eneo hilo pamoja na upatikanaji holela wa silaha kutoka maeneo jirani yenye mzozo kwa jumla vimechangia vifo kuongezeka.

**VOA**

## Wauawa kwa kupigwa risasi wakiandamana

**KINSHASA, Congo**

WATU watatu wameuawa kwa kupigwa risasi na polisi wakati wa maandamano ya kupinga ukosefu wa usalama katika eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

Mkuu wa wilaya ya Beni katika mkoa wa Kivu Kaskazini, Donat Kibwana alisema: "Kulikuwa na maandamano ambapo watu watatu wameuawa, mvulana mdogo wa miaka 25 ambaye amepigwa risasi tumboni amefariki baada ya kufikishwa hospitalini"

"Mwingine ni kutoka jamii ya Mamburikimo amepigwa risasi, na kufariki papo hapo, mtoto mwingine pia amepigwa risasi na kufariki". Hali ya usalama katika eneo hilo la Mashariki mwa DRC si shwari, usalama umekuwa mdogo, huku matukio ya mauaji yakiendelea kuongezeka.

**RFI**

# Omar Bashir apandishwa kizimbani, akiri kosa

**KHARTOUM, Sudan**

ALIYEWAHI kuwa Rais wa Sudan, Omar al- Bashir amekiri kupokea mamilioni ya dola kutoka Saudi Arabia.

Bashir alipandishwa mahakamani jana ambapo alisomewa mashitaka yanayomkabili mojawapo likiwa ni kukutwa na kiasi kikubwa cha fedha, lingine likiwa ni ufisadi, ambayo mawakili wake wanasema hayana msingi.

Mashtaka mengine ni kupokea zawadi kinyume cha sheria.

Bashir alitimuliwa madarakani Aprili baada ya maandamano ya miezi kadhaa, yaliofikisha kikomo utawala wake wa takriban miaka 30.

Mnamo Juni, waendesha mashtaka walisema kiwango kikubwa che fedha za kigeni zilizohodhiwa ziligunduliwa katika magunia ya nafaka nyumbani kwake.

Siku ya Jumapili, wanaharakati wa kutetea demokrasia na viongozi wa jeshi nchini humo waliomtimua madarakani Bashir, walisaini makubaliano yanayotoa fursa kufanyika uchaguzi mkuu nchini humo.

Kiongozi huyo wa zamani, aliyefika mahakamani na kusimama kizimbani alikuwa amevaa nguo nyeupe na kilemba, hakujibu tuhuma zinazomkabili.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kulikuwapo na maofisa wengi wa usalama walioshika doria nje ya mahakama katika Mji Mkuu Khartoum, wakati Bashir aliposwasili.

Mnamo April, kiongozi wa Jeshi Sudan, Abdel Fattah al-Burhan alisema zaidi ya dola za Marekani milioni 113 ya fedha katika sarafu ya pauni ya Sudan na sarafu za kigeni ziligunduliwa nyumbani kwake.Hata hivyo, mwakili wanaomtetea Bashir wanapinga mashtaka hayo.

Kiongozi huyo aliyetimuliwa alitarajiwa kufikishwa mahakamani Julai, mwaka huu lakini kesi yake iliahirishwa kutokana na sababu za usalama.

Mnamo Mei, mwendesha mashtaka Sudan alimshtaki Bashir kwa uchochezi na kuhusika katika mauaji ya waandamanaji.

Mashtaka hayo yanatokana na uchunguzi wa kifo cha daktari aliyeuawa wakati wa maandamano yaliochangia kutimuliwa kwa Bashir madarakani mnamo Aprili.

Shahidi mmoja alieleza kuwa daktari huyo aliyekuwa akiwatibu majeruhi alitoka nje ya jengo akiinua mikono juu, na kuarifu polisi kwamba yeye ni daktari, na papo hapo akapigwa bunduki.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wanasema kuwa kesi inayomkabili Bashir inaonekana kama mtihani iwapo utawala mpya unaweza kukabiliana na uhalifu unaotuhumiwa kutekelezwa na utawala uliokuwapo.

Siku ya Jumamosi, baraza la utawala wa kijeshi Sudan uliongia madarakani baada ya kuondoka kwa Bashir, lilisaini makubaliano muhimu ya ugavi wa mamlaka na muungano wa kiraia wa upinzani.

Makubaliano hayo yanatoa fursa ya kuidhinishwa baraza jipya la utawala linalowajumuisha raia na majenerali wa jeshi, kutoa fursa ya kufanyika uchaguzi mkuu na hatimaye utawala wa kiraia.

Wanachama wapya wa baraza huru jipya walitarajiwa kuapishwa jana, lakini hafla hiyo iliharishwa kwa siku mbili kutokana na ombi la wanaharakati wa kuunga mkono demokrasia.

***BBC***



Ahmed al-Rabie, mwakilishi wa Alliance for Freedom and Change (kulia) na Mohammed Hamdan Daglo, kiongozi namba mbili wa Baraza la Kijeshi Sudan (mwenye sare ya jeshi) wakati wa kusaini makubaliano.**PICHA:AFP**

# Wanaoishi msituni kutimuliwa

**NAIROBI, Kenya**

SERIKALI ya Kenya imeanza utaratibu wa awamu ya pili ya kuwaondoa watu wanaoishi katika Msitu wa Mau kwa sababu ya uhifadhi wa chemchem zilizomo kwenye msitu huo muhimu.

Waziri wa mazingira wa Kenya, Keriako Tobiko ameeleza kuwa wakati huu wanawakusudia wamiliki wa mashamba makubwa msituni humo pamoja na takribani hatimiliki 1,200 zinazoaminika kuwa sio halali.

Wanaharakati wa mazingira wanaunga mkono juhudi hizo ila wanahimiza suluhu ya kudumu wakihofia uhalifu katika zoezi hili.

Serikali ya Kenya ilianza harakati za kuwaondosha watu kutoka msitu huo kwa minajili ya uhifadhi wa msitu huo wakati huu zoezi hili likiwalenga wamiliki wa mashamba makubwa.

Hii ni awamu ya pili na Waziri Tobiko amefanya mkutano na maofisa wa usalama pamoja na maofisa wa huduma ya misitu huko Narok.

Haya yanajiri baada ya serikali ya Kenya kuchapisha katika magazeti kuwa takriban hatimiliki 1,274 za ardhi zitabatilishwa.

Mwanaharakati wa mazingira na haki za binadamu, Joseph Towett alisema ni hatua muhimu hasa ikizingatiwa kuwa wamiliki wakubwa wa mashamba katika misitu hiyo ni wanasiasa walio na ushawishi mkubwa:

Mwaka 2013 siasa kuhusu kuwaondoa watu katika msituni wa Mau ili kuuhifadhi lilimnyima kura kiongozi wa ODM, Raila Odinga baada ya wakazi wa eneo hilo kumpa uungwaji mkono mkubwa mwaka 2007.

Wakati huo huo, Makamu wa Rais wa Kenya, Wiliam Ruto alizipiga vita juhudi zake za uhifadhi wa msitu huo.

Hata hivyo, Waziri Tobiko amesema kuwa hakuna litakalositisha zoezi hilo.

Awamu hiyo ya pili inalenga kuwaondoa watu 60,000 baada ya awamu ya kwanza iliyowaondoa watu 10,000. ***DW***

# Bilioni 9/- zatekeleza miradi ya maendeleo

**Na Elisante John, SINGIDA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Singida imetumia zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, sawa na asilimia 101 ya fedha zilizoidhinishwa na serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Kiasi hicho cha fedha ni pamoja na kile kilichopelekwa na serikali, ambacho kiko nje ya ukomo wa bajeti ya halmashauri kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 30, mwaka huu.

Katika bajeti ya mwaka uliopita, halmashauri iliidhinishiwa na serikali kutumia Sh. 8,942,870,229.15 sawa na asilimia 31.76 ya bajeti yote iliyoziomba ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 28.15 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Eliya Dighah, alisema hayo jana kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, ambalo pamoja na mambo mengine lilimchagua makamu mwenyekiti, wenyeviti na wajumbe wa kamati mbalimbali za halmashauri hiyo.

Alisema kati ya fedha hizo, zaidi ya Sh. bilioni 1.5 ziligharamia miradi iliyoko chini ya elimu ya msingi, huku zaidi ya Sh. bilioni 1.4 zikigharamia miradi ya elimu ya sekondari, wakati miradi ya afya ilitumia zaidi ya Sh. bilioni 3.5.

Mwenyekiti huyo pia alisema zaidi ya Sh. bilioni 2.4 zilitumika kwa ajili ya miradi ya maji, usafi wa mazingira, mfuko wa jimbo na kiasi kingine kilichosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kwa familia maskini zaidi.

"Ninachukua fursa hii kumshukuru Rais John Magufuli kwa serikali yake kutupatia fedha hizi. Mkurugenzi mtendaji na timu yake ya wataalamu pia wanapongezwa kwa usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema Dighah.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alisema pamoja na pongezi hizo, bado huduma za jamii hazitolewi kwa asilimia 100 kutokana na changamoto nyingi. Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni uhaba wa vyumba vya madarasa, nyumba za watumishi wa umma, matundu ya vyoo, maabara na kutopata fedha zote kama zilivyoidhinishwa.

Katika hatua nyingine, baraza hilo lilimchagua Omari Mande kwa mwaka wa nne mfululizo kuwa makamu mwenyekiti wa halmashauri hiyo kwa kura zote 30 za ndiyo.

Naye Iddi Kijida alishinda nafasi na mwenyekiti wa huduma za jamii, Mchaga Guffa akapitishwa kuwa mwenyekiti wa kamati ya uchumi na Salma Kundya mwenyekiti wa kamati ya maadili.

# Serikali kuimarisha shamba la mifugo Nanyumbu

**Na Edward Kondela**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2019/20 imeweka mikakati ya kuliimarisha shamba lake la kuzalisha mifugo la Nangaramo, wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara ili kusogeza zaidi huduma hiyo kwa wananchi.

Akizungumza baada ya kutembelea shamba hilo kujionea mafanikio na changamoto, Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Felix Nandonde, alisema wizara imedhamiria kuhakikisha shamba la Nangaramo linapata ng'ombe bora wa kisasa wa maziwa, wazazi pamoja na kumpeleka mtaalamu katika Kituo cha Uhimilishaji (NAIC), kilichopo mkoani Arusha kujifunza na kutoa huduma katika shamba hilo.

"Shamba linatoa huduma katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, nia ya kuleta ng'ombe bora wa kisasa hususan kwa wafugaji ni kupata uzalishaji bora pamoja na wafugaji hao kufuga kisasa, shamba la Nangaramo ni muhimu sana tutahakikisha mwaka huu wa fedha tunalisaidia ili liweze kutoa tija kwa wananchi kwa kununua ng'ombe bora na kisasa kutoka katika shamba hili," alisema Dk. Nandonde.

Akizungumzia miundombinu ya shamba hilo, alisema hajaridhishwa na hali ilivyo sasa kwa kuwa mifugo iliyopo shambani hapo ni michache na kutaja idadi ya ng'ombe waliopo ni 295 na mbuzi 64.

Pia alisema mifugo hiyo haifugwi katika maeneo yaliyo rasmi ya uchungaji na kwamba serikali katika kipindi cha miaka kumi inatarajia kuwa na ng'ombe katika shamba hilo ifike 1,000, huku Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiendelea na mikakati ya kuboresha zaidi miundombinu ya shamba.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Shamba la Nangaramo, Salum Kamota, alisema kwa sasa shamba hilo limekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa wananchi wengi kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma wanahitaji kununua ng'ombe bora na kisasa ili kufuga kwa tija na kupata matokeo mazuri yakiwamo ya upatikanaji wa maziwa mengi kutoka katika ng'ombe hao kwa kuwa shughuli nyingi za kiuchumi zimeongezeka katika mikoa hiyo na kusababisha ongezeko la watu na mahitaji yao.

Shamba hilo ni kati ya mashamba matano yanayomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, yanayozalisha ng'ombe bora wa kisasa na kuuza kwa wananchi kwa bei nafuu ili waweze kufuga kisasa na kupata mazao mazuri.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kuwaaga wanafunzi wanaokwenda kusoma nchini China. Kulia ni Balozi wa China hapa nchini, Wang Ke. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 30 kizimbani tuhuma za uzururaji

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WATU 30 wamefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Nunge Manispaa ya Morogoro kwa shtaka la uzembe na uzururaji.

Walikamatwa baada ya kudaiwa kukutwa wakizurura bila kuwa na shughuli wala sababu maalum majira ya usiku katika eneo la Kahumba Manispaa ya Morogoro.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Emmilia Mwambagi, alisema kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Agosti 16, saa 5:45 usiku na askari waliokuwa doria katika maeneo hayo.

Akisoma mashtaka hayo Hakimu Mwambagi alisema, washtakiwa hao wakiwamo wanawake 23 na wanaume saba walifikishwa mahakamani hapo kwa tuhuma hizo, na kwamba wote walikana kuhusika na tukio hilo.

Hakimu Mwambagi alisema washtakiwa hao huku wakijua kufanya hivyo ni kosa, wametenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha sheria namba 107 ya makosa ya jinai. Hata hivyo, kesi hiyo iliahirishwa kusubiri mashahidi wa upande wa mashtaka wafike mahakamani.

Kesi hiyo itaendelea tena Agosti 20, mwaka huu, na kwamba dhamana ipo wazi kwa kila mtuhumiwa.

Alisema masharti ya dhamana ni kuwa na mdhamini mmoja mwenye vitambulisho vinavyotambulika sambamba na Sh. milioni 1.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

**MASHAMBA YANAUZWA DODOMA:** Kuanzia ekari 1 hadi ekari 50 bei maelewano, wasiliana na Dodoma Pazuri Group (DPG) Simu:0745312845/0657746365

**VIWANJA VINAUZWA KISEMVULE:** Malipo awamu mbili urefu futi 50 kwa upana futi 40 bei Sh.1,700,000/=na Sh.1,200,000/= tu, Simu:0714564651/0623528465.

**MAFUTA ORIJINO YA ALIZETI:** Toka Singida, lita 5 tunauza kwa Sh.20,000/= tu ukiagiza kuanzia lita 20 tutakuletea mahali ulipo. Simu:0623528465/0655782175.

**Pata Ramani za majengo** mbalimbali kama Nyumba na Shule Simu: 0744113969

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**Veronica Nyansambo** anatangaza kupotea kwa Result Slip yenye index namba **E526-0146** iliyotolewa na Chuo cha Ualimu Patandi Arusha mwaka 2003. Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KBA/RB/6077/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



**MARIA BERNARD NDITTI**

Mwenye picha hapo juu anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha IV kilichotolewa na NECTA mwaka 2011 sekondari ya WIGAMBA chenye Index no. **S.3133/0042** namba ya Ripoti ya Polisi **RB ni DAR/GOG/RB/219032/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI




**SALAMA KIPENYAPENYA** Amepotelewa na Cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea katika shule ya Secondari HIGH LANDS, Alichomaliza mwaka 1980 na chenye index namba **S.312/49.**

Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi,

Taarifa ya polisi;
**MOR/MOR/RB/221693/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**Norbert Norbert Nombo** anatangaza kupotelewa nam cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2064-0180** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika Shule ya Sekondari Nkuyu .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: UD/B.1/1/VOL.1XV/258/2019**


### KUPOTEA KWA CHETI



Pastory Charles anatangaza kupotelewa nne cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1498/0103** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Luyege

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: WBW/RB/8378/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



**Abraham Ahmed Msangi** anatangaza kupotelewa nam cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1267-0015** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari Brooke bond .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: WBW/RB/8378/2019**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DITRICT COURT OF KIGOMA**
**AT KIGOMA**
**CIVIL CASE NO 3 OF 2019**
**JUMANNE RAMADHANI PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**PILI MRISHO DEFENDANT(S)**
**Summons to Witness**
**(OxV, r 1 &5 of the Civil procedure Code)**

**TO PILI MRISHO**
**WHEREAS** your attendance is required to testify on behalf of ………………in the above suit, you are hereby required (personally) to appear before this court on the 21st day of AUGOST 2019 at 9:00AM in the forenoon/afternoon and to bring with you all relevant documents materials.

If you fail to comply with this order without lawful excuse, you will be subject to the consequences of non-attendance laid down in rule 12 of Order XVI of the Civil Procedure Code, 1966.
GIVEN under my HAND and the SEAL of the court, this 19th day of AUGOST 2019.

DEPUTY REGISTRA/REGISTRAR /MAGISTRATE
NOTICE (1) If you are summoned only to pro…. Document and not to give evidence, you shall be deemed to have complied with the summons if you cause such document to be produced in this Court on the day and hour aforesaid.

(2) If you are detained beyond the day aforesaid, a sum of T shs…………will be tendered to you for each day's attendance beyond the day specified.

1, HEREBY acknowledge the receipt ofa duplicate of this summons this……………………day of ……………………20………………………………..

Signature……………………………………………
Date……………………………………………………

215381202

### VIWANJA NA MAKAZI VIANUZWA

Viwanja vipo Mpamaa mkabala na uwanja wa ndege wa kimataifa Jijini Dodoma. Ukubwa ni kama ifuatavyo

1. Sqm 1,864.79
2. Sqm 1,836.73
3. Sqm 27,287.94
4. Sqm 5844.99
5. Sqm 5122.19
6. Sqm 757.07
7. Sqm 666.38
8. Sqm 1247.47
9. Sqm 1399.74
10. Sqm 1072.93
11. Sqm 1930.28
12. Sqm 860.48

**Piga sim 0787433058 au 0754433058**
**REV. JOHN KASHEKYA**

215381002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;160/2019**

Ombi la **MACKLINA LULENGA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MAGRETH EBERHAT LULENGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/08/2019

215380302

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# POCHETTINO

## ALIA DIRISHA EPL KUFUNGWA MAPEMA



**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, amesema kufungwa mapema kwa dirisha la usajili nchini Uingereza ni "kosa kubwa" na ana matumaini "watamaliza tatizo lao msimu ujao ".

Pochettino bado hajui hatima ya Christian Eriksen, ambaye amebakiza miezi 12 kwenye mkataba wake, huku kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark akitajwa kwamba anataka kuhamia nchini Hispania.

Kama klabu za Ulaya zitatoa ofa ya Eriksen kama ambavyo imeripotiwa kuwa Real Madrid wanataka kumsajili kabla ya kufungwa dirisha la usajili Septemba 2, Spurs watapata fedha, lakini hawatakuwa na uwezo wa kusajili hadi Januari mwakani, kwani dirisha la usajili kwa nchini Uingereza limeshafungwa Agosti 8, mwaka huu.

"Sikuwapo kwenye makubaliano, lakini wakati ule waliamini kwamba ulikuwa bora kwa klabu," alisema kocha huyo wa Spurs.

"Lakini nafikiri (Mwenyekiti wa Tottenham Daniel Levy) na watu wengi wanakubali kwamba lilikuwa kosa kubwa. Natumaini tutalimaliza tatizo hilo msimu ujao.

"Tunatakiwa kurudi nyuma na kwenda sawa na sehemu nyingine Ulaya, kwa sababu nafikiri litakuwa jambo gumu kushinda kwenye michuano ya Ligi ya Europa au Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ligi ya Mabingwa unaweza kutangaza tatizo kwa timu kama zetu na ni wazi kwamba sitaweza kuwa kocha mwenye furaha wakati timu nyingine za Ulaya zinaweza kurekebisha vikosi vyao wiki tatu zaidi

"Kwa upande wangu naona hili si jambo nzuri, tunatakiwa kurudi kuwa pamoja wakati wa kufungwa kwa dirisha la usajili, natumaini litaweza kurekebishwa."

# ABRAHAM: MTAFUNGA MDOMO MNAONICHUKIA

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham, amesema yeye ni "mwenye mawazo chanya" na amepanga "kuwanyamazisha wanaomchukia" baada ya kushambuliwa kwa ubaguzi wa rangi kwenye mitandao ya kijamii.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alibaguliwa na kutukwana kwenye mitandao ya kijamii baada ya Chelsea kufungwa na Liverpool kwa mikwaju ya penalti katika kinyang'anyiro cha Uefa Super Cup Jumatano iliyopita, ambapo ilishuhudiwa kinda huyo wa timu ya Taifa ya England akikosa penalti ya mwisho.

"Mambo kama haya huwa yanatokea kwenye mpira wa miguu. Bahati mbaya kwangu nilikumbwa katika dakika ya mwisho," alisema Abraham akiiambia Sky Sports News baada ya sare ya Chelsea kufungana bao 1-1 na Leicester kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England katika dimba la Stamford Bridge juzi Jumapili.



"Nilikuwa na uzoefu wa kupiga penalti zenye presha na bahati mbaya nilikosa.

"Nilitukwana na kubaguliwa, lakini mimi ni mtu mwenye mawazo chanya. Sisikilizi upuuzi hasa kutoka kwa watu wanaojaribu kunishusha chini."

## GUARDIOLA AZIPA UBINGWA CHELSEA, UNITED, ARSENAL

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaamini Klabu za Chelsea, Manchester United na Arsenal ndizo zenye nafasi kubwa ya kutoa changamoto ya ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu huu.

Kauli hiyo imekuja baada ya Jose Mourinho kunukuliwa akisema kwamba, timu ya Man City B inaweza kushinda ubingwa wa ligi hiyo pamoja na Manchester City, Tottenham na Liverpool.

Lakini Guardiola, anaamini kwamba Chelsea, Man United na Arsenal zina nafasi kubwa ya kuwa kwenye mbio za farasi watatu wa kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

"Kwa uhakika nimevutiwa na Chelsea na jinsi walivyocheza dhidi ya Manchester United na Liverpool," alisema Guardiola.



"Nilishangazwa na namna timu ya Frank Lampard ilivyocheza.

"Na tuliona ubora wa United hasa safu yake ya ushambuliaji, walicheza vizuri. Arsenal imenunua wachezaji wazuri pia, hivyo nao wana nafasi ya kupigania ubingwa."

Guardiola pia aliwasifia Tottenham, ambao walicheza nao Jumamosi kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

"Tangu nimekuja hapa England, Tottenham wamekuwa kwenye nafasi ya kuwania ubingwa kila msimu," alisema Guardiola.

HABARI MICHEZO



# LAMPARD:

## UCHOVU SABABU KUPATA SARE

**LONDON, England**

FRANK Lampard anaamini kwamba uchovu wa mchezo wa Uefa Super Cup Jumatano iliyopita ndiyo ulichangia Chelsea kucheza kwa kiwango duni katika kipindi cha pili wakati wakitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Leicester kwenye mechi ya Ligi Kuu England, juzi Jumapili.

Chelsea ya Lampard ilirudi kutoka jijini Istanbul nchini Uturuki Alhamisi baada ya kufungwa na Liverpool kwenye Super Cup kwa changamoto ya mikwaju ya penalti, na licha ya kuanza vizuri kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Stamford Bridge, lakini Wilfred Ndidi akasawazisha kipindi cha pili.

Leicester ingeweza kuibuka na ushindi rahisi, kwani kipindi cha pili walicheza vizuri na kukosa nafasi kadhaa za wazi za kufunga.

"Nachukia uchovu kuwa sababu, lakini ndio ukweli uliotokea katika kipindi cha pili," alisema kocha huyo wa Chelsea akinukuliwa na Sky Sports.

"Niliwaona Liverpool walicheza juzi (Jumamosi), na nilijua kwamba mchezo huo ungekuwa mgumu kwao.

"Lakini bado nafikiri kikosi changu kilicheza vizuri na kilikuwa bora kwenye mchezo huo. Najua wachezaji walicheza, lakini walicheza kwa kujituma zaidi."

Mason Mount alianza kuiweka mbele Chelsea katika dakika ya saba, lakini Ndidi alisawazisha kwa kichwa mpira wa kona.

Hii inamaanisha kwamba, Lampard hajashinda mchezo wowote kati ya mitatu tangu abebe jukumu la kuinoa timu hiyo.

# Inter Milan yajitosa rasmi kwa Sanchez

**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan imeonyesha nia yake ya kutaka kumsajili Alexis Sanchez kutoka Manchester United, kwa mujibu wa ESPN FC.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ambao tayari wameshamsajili Romelu Lukaku kutoka hapo Old Trafford kipindi hiki cha majira ya joto, wanatumaini kukamilisha dili hilo la kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile kwa mkopo kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la Ulaya Septemba 2, mwaka huu.

Sanchez atakuwa tayari kuzungumza na Inter kama klabu hizo mbili zitafikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji huyo, ambaye anaonekana kutokuwa kwenye mipango ya kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer.

Inter ina matumaini ya kufikia makubaliano ambayo yataifanya United kumlipa Sanchez sehemu ya mshahara wake kabla ya kununuliwa rasmi kipindi kijacho cha majira ya joto, ingawa chanzo kimoja kimeiambia ESPN FC bado makubaliano hayajafikiwa.

Solskjaer alisema Ijumaa kwamba, Sanchez mwenye umri wa miaka 30, anakaribia kurudi uwanjani akiwa fiti, kwani sasa anaelekea kupona majeraha yake ya misuli ya nyama za paja.

Na kocha huyo raia wa Norway alidai kwamba, mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal anaweza kuwa mchezaji muhimu wa United msimu huu.

Lakini chanzo kingine kimeiambia ESPN FC kwamba, kocha huyo yupo tayari kumuachia Sanchez aondoke, licha ya kwamba imeshampoteza Lukaku kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Sanchez bado ana miaka mitatu imebaki katika mkataba wake tangu alipotua hapo Old Trafford akitokea pale dimba la Emirates Januari 2018.

Ameichezea mechi 45 United, lakini amefunga mabao matatu tu kwenye Ligi Kuu na hajawahi kucheza kwa dakika zote 90 kwenye Ligi Kuu tangu alipoanza kuvaa jezi ya United Agosti 2018.







# Balotelli asajiliwa rasmi na Brescia

**ROME, Italia**


MARIO Balotelli amejiunga na timu ya nyumbani kwake Brescia kwa uhamisho huru, klabu hiyo ya Serie A imethibitisha.

Balotelli, ambaye aliachwa na Marseille mwishoni mwa msimu uliopita, amerudi nchini Italia kwa mara ya tatu, baada ya kuichezea Inter, ambako alitwaa mara tatu taji la Ligi Kuu na AC Milan.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 29, jana Jumatatu alitambulishwa rasmi katika uwanja wa Mario Rigamonti, huku taarifa zaidi zikieleza amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo, ambayo imerudi kwenye Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2011.

Msimu wa Ligi Kuu ya Italia unanza wikendi hii, lakini Balotelli hataanza kucheza kwa sababu anatumikia kifungo cha mechi nne baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwenye mchezo wake wa mwisho kuichezea Marseille dhidi ya Montpellier Mei, mwaka huu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: POGBA WA HAPAHAPA MAN UTD

Bado tunabaki na swali kubwa, sina wasiwasi juu ya Paul, kwangu mimi, atabaki...

**Manchester, england**

Ole Gunnar Solskjaer amerudia tena kueleza kwamba Paul Pogba hataondoka Manchester United majira haya ya joto licha ya nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa kusema kuna "swali kubwa" kuhusu mustakabali wake wa baadaye.

Kuelekea mechi ya jana ugenini dhidi ya Wolves, Sky Sports, ilimuuliza swali kocha huyo wa United kuhusu Pogba - na wapi anaweza kuishia - kufuatia matamshi ya hivi karibuni ya kiungo huyo baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Chelsea Jumapili wiki moja iliyopita.

"Mara zote unaweka ulizo kuhusu Paul, siyo?" Solskjaer aliwauliza wanahabari waliokusanyika katika mkutano wa waandishi wa habari. Tunajua kuna mambo yanazungumzwa. Muda utazungumza. Bado tunabaki na swali kubwa.

"Sina wasiwasi juu ya Paul. Kwangu mimi, atabaki, " kocha huyo wa United aliendelea.

"Sidhani kama si la kawaida kusema, 'ninafurahi kucheza na wachezaji wenzangu, nafurahia kile ninachofanya, napenda kazi yangu na ninafurahia mchezo'.

"Bila shaka, sentensi hiyo na swali kubwa kumhusu mara zote kuna swali kuhusu Paul Pogba.

"Si mkutano mmoja na waandishi wa habari ambao nimejibu swali hilo kuhusu Paul Pogba.

"Asilimia 80 ya kile nilichosema 'ninafurahia mchezo' na wakati wangu sasa."

Pogba amekuwa akihusishwa na Real Madrid tangu alipokiri wakati akiwa katika majukumu na timu ya Taifa ya Ufaransa Machi mwaka huu, kuwa kuichezea klabu hiyo ya La Liga chini ya Zinedine Zidane itakuwa ni "ndoto kwa kila mtu".

Tangu mwishoni mwa msimu uliopita, Pogba alisema inaweza kuwa muda wa changamoto mpya, na wakala wake, Mino Raiola, baadaye akathibitisha kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26-anataka kuondoka United.

United inasisitiza hauzwi wakati Real ikionekana haiwezi kukamilisha dili hilo licha ya msisitizo wa Zidane wa kumnasa mchezaji huyo. Walitoa ofa ya fedha iliyomjumuisha na mchezaji James Rodriguez, ambayo ilikataliwa Julai mwaka huu.

## KWA UFUPI

**PSG YAMFUATA DYBALA JUVE**
MABINGWA wa Ufaransa Paris St-Germain wamefanya mazungumzo na Juventus kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya mshambuliaji Muargentina Paulo Dybala, 25, kwa pauni milioni 73. ***(Mail)***

**COUTINHO YUPO BAYERN**
KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho, ametua Ujerumani kukamilisha mpango wake wa kujiunga kwa mkopo wa muda mrefu na mabingwa Bayern Munich. ***(Sun)***

**NEYMAR KWA MKOPO BARCA**
Barcelona inatumai kumrejesha Neymar Nou Camp, lakini kuwapo na ulazima wa kifungu cha kumnunua. ***(Sport - in Spanish)***

**LLORENTE AKARIBIA NAPOLI**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tottenham, Fernando Llorente, 34, anakaribia kujiunga na miamba ya Italia, Lazio. Lakini Inter Milan, Fiorentina na Napoli pia zinavutiwa kuipata huduma ya Mhispania huyo ambaye kwa sasa hana klabu. ***(Corriere Dello Sport - in Italian)***

**VARANE, VINICIUS WATAKIWA PSG**
Paris St-Germain imeiulizia Real Madrid kama itakuwa tayari kumwanchia beki Mfaransa Raphael Varane, 26, na mshambuliaji Mbrazil Vinicius Junior, 19, ili kubadilisha na Neymar, 27. ***(Telefoot - in French)***

**INTER KWA SANCHEZ, VIDAL**
Inter Milan inaitaka huduma ya mshambuliaji wa Manchester United na Chile, Alexis Sanchez, 30, kwa mkopo na pia inavutiwa na kiungo wa Barcelona, raia wa Chile pia, Arturo Vidal, 32. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**POCHETTINO NA DIRISHA LA USAJILI**
KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anatumai majira ya joto yajayo Premier League itarejea kuwa na dirisha la usajili litakalofungwa tarehe moja kama ilivyo kwingineko Ulaya. ***(Telegraph)***

**SARRI AMKATAA EMRE CAN**
Paris St-Germain na Bayern Munich zinaweza kumfuata kiungo Mjerumani Emre Can, 25, baada ya kuelezwa na kocha Maurizio Sarri hahitajiki tena Juventus. ***(Tuttosport, via Mail)***

**COUTINHO AMZUIA CAN BAYERN**
Bayern Munich haitamfuata kiungo wa Juventus, Emre Can, 25, kama itafanikiwa kukamilisha uhamisho wa kiungo wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho, 27. ***(Goal)***

**BAKAYOKO AWINDWA MONACO**
Paris St-Germain na Monaco zinataka kutoa ofa kwa kiungo Mfarasa Tiemoue Bakayoko, 25, kufuatia kuonekana kutohitajiki tena Chelsea. ***(Daily Express)***

**AURIER ANUKIA KUSEPA SPURS**
BEKI wa kulia wa kimataifa wa Ivory Coast, Serge Aurier, 26, anaweza kuachana na Tottenham na kujiunga na AC Milan kama Muitaliano Andrea Conti, 25, ataachana na miamba hiyo ya Serie A kabla ya dirisha la usajili la Ulaya kufungwa. ***(Calciomercato)***

**BAILLY KUONGEZWA MKATABA UTD**
Manchester United inajadili uwezekano wa kumuongezea mkataba beki Eric Bailly, 25. ***(Sun)***



HABARI MICHEZO

# SHAIBU 'NINJA' AANZA KWA KUTOA PENALTI LA GALAXY

Na Mwandishi Wetu

BEKI wa zamani wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja', ameichezea kwa mara ya kwanza timu yake ya Klabu ya LA Galaxy inayoshiriki Ligi Kuu ya nchini Marekani (MLS), huku akianza kwa makosa yake yaliyozoeleka wakati akicheza soka nchini.

Ninja amejiunga na timu hiyo kwa mkopo wa mwaka mmoja akitokea timu ya MFK Vyskov inayoshiriki Ligi Daraja la Tatu Jamhuri ya Czech ikiwa ni baada ya kumaliza mkataba wake wa miaka miwili na Yanga aliyojiunga nayo akitokea Taifa Jang'ombe ya Zanzibar.

Akiichezea LA Galaxy kwa mara ya kwanza Jumamosi, Ninja aliisababishia penalti baada ya kumchezea rafu mshambuliaji wa New Mexico dakika ya 74, makosa ambayo kwake ilikuwa si jambo la ajabu kuyafanya wakati akiwa Yanga.

Makosa hayo yaliipa New Mexico bao na kufanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Wakati akiichezea Yanga kwa mara ya kwanza, kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, Ninja alijifunga.

Ninja ambaye alianzia kujifua na wachezaji wa akiba alipotua LA Galaxy, Ijumaa alitambulishwa rasmi katika mtandao wa klabu hiyo na kukabidhiwa jezi namba 51 kabla ya Jumamosi kuichezea timu hiyo ambayo ina nyota wengi wa kimataifa akiwamo mshambuliaji wa zamani wa Barcelona, PSG na Manchester United, Zlatan Ibrahimovic.

KAMBA MGUUNI...



Wanafunzi wa shule za msingi zenye mahitaji maalum za jijini Dar es Salaam, wakishiriki katika mbio za Kamba Mguuni zilizoandaliwa na Shule ya Al Muntaziri na kufanyika katika viwanja vya JMK Youth park jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Azam: Rekodi Chamazi itawaliza Waethiopia

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kukubali kipigo cha mabao 4-2 kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba Jumamosi iliyopita, Azam FC imesema Fasil Kenema haitanusurika na kichapo kwa kuwa rekodi yao katika mechi za kimataifa ndani ya Uwanja wao wa Chamazi, hakuna timu inayotoka salama.

Azam FC itarudiana na Waethiopia hao ikiwa ni baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini kwenye mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Msemaji wa Azam FC, Jaffari Maganga, jana aliliambia Nipashe kuwa timu hiyo inaendelea na maandalizi mazito na tayari Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Etienne Ndayiragiji ameanza programu maalum kuelekea mchezo huo.

Maganga alisema mechi hiyo itapigwa Jumamosi saa 10:00 alasiri katika Uwanja wa Chamazi na akasisitiza kwa kuwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kuipa sapoti timu yao.

"Hakuna timu iliyotoka salama katika Uwanja wa Chamazi kwenye mechi za kimataifa, hivyo kwa maandalizi ambayo tunayafanya ikiwa ni pamoja na progamu za kocha, tuna uhakika hata Fasil Kenema hawatatoka.

"Lengo letu ni kuendelea kuipeperusha vema bendera ya Tanzania na hatutakubali kufanya makosa kwenye uwanja wetu wa nyumbani ambao tuna rekodi ya kushinda mechi za kimataifa," alisema.

Azam inatakiwa kushinda kuanzia mabao 2-0 ili kusonga mbele, na endapo itafanikiwa itakutana na mshindi wa jumla kati ya Triangle FC ya Zimbabwe na Rukinzo FC ya Burundi.

## Tanzania U-15 yaanza vibaya nchini Eritrea

Na Somoe Ng'itu, ASMARA

TIMU ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 15 ya Tanzania imeanza vibaya mashindano ya kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati kwa kukubali kufungwa mabao 2-0 na Uganda katika mechi iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea.

Kwa matokeo hayo ya jana, Uganda imefikisha pointi tisa na kuwa timu ya kwanza kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu.

Mabao yote ya Uganda yalifungwa na Travis Mutyaba ambaye jana alifikisha mabao matatu tangu kuanza kwa mashindano haya yanayosimamiwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Tanzania ambayo ilishindwa kutumia nafasi nne za wazi ilizotengeneza katika mchezo huo, italazimika kushinda mechi zake tatu za hatua ya makundi zilizosalia ili iweze kusonga mbele kwenye michuano hii.

**Yosso hao wa Tanzania wanaonolewa na Kocha Mkuu, Maalim Saleh, watashuka tena dimbani kesho kuvaana na Sudan Kusini huku Ijumaa kucheza dhidi ya Rwanda na itamaliza mechi zake za hatua hiyo ya makundi Jumapili dhidi ya Ethiopia.**

Akizungumza kuhusu mchezo huo wa jana, Saleh, alisema kuwa wachezaji wake wamecheza tofauti na maelekezo aliyowapa, lakini kwa sababu bado ni wadogo, atawarekebisha ili wafanye vema katika mchezo unaofuata.

Saleh alisema suala la wapinzani wao Uganda kudaiwa kutumia wachezaji "vijeba", kwake si muhimu, kwa sababu anatumia mechi hizi kuwapa uzoefu wa kushiriki mashindano ya kimataifa.

Mashindano haya yanatarajiwa kuendelea tena leo kwa kuwakutanisha yosso wa Kenya dhidi ya Burundi huku wenyeji Eritrea wakiwakaribisha Sudan.

# Michezo

Jumanne Agosti 20, 2019

Nipashe




## Solskjaer: Pogba wa hapahapa Man Utd

HABARI UK 30

SAWAZISHA...




Kiungo wa Leicester City, Mnigeria Wilfred Ndidi ( Na. 25), akiruka na kuunganisha mpira wa kona kimyani kwa kichwa na kufanya matokeo kuwa bao 1-1, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi. **HABARI UK. 29**

# ZAHERA AICHOMOLEA YANGA BETRI IKIPAA

●●●Asema isiwe sababu, 'Dege la ATCL' laiwahisha kuivaa Township Rollers ikiwa na nyota 20, Molinga aachwa...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera kuamua kuwasha moto ('kuchomoa betri') kuhusu kutoona manufaa ya kambi waliyoweka mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania ya Moshi na AFC Leopards ya Kenya, amekiongoza kikosi chake kuifuata Township Rollers ya Bostwana akiwa na matumaini makubwa.

Yanga ikiwa katika kambi hiyo, ilikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi iliyopigwa Ijumaa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi kabla ya juzi, Jumamosi kuichapa AFC Leopards kwa bao 1-0 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Na mara baada ya mechi hiyo, Zahera alichomoa betri kwa uongozi wa Yanga akieleza kuwa ziara hiyo haikuwa na manufaa hasa katika kipindi hiki ambacho wanakabiliwa na mchezo mgumu wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana.

"Tuna mchezo mgumu na muhimu wa marudiano dhidi ya Township Rollers, hivyo tulihitaji muda kuiandaa timu lakini tunakuja kupoteza muda huku Moshi na Arusha.

"Mechi zetu dhidi ya Polisi na AFC Leopards tumecheza katika viwanja vibovu hakuna jambo la maana tulilofaidika nalo hii ziara tungeweza kuifanya muda mwingine si huu," alisema Zahera baada kuifunga AFC Leopards. Aliongeza kuwa kwenye michezo hiyo ya kirafiki hakuwa anachezesha kikosi kamili, na kwamba kupoteza mchezo dhidi ya Polisi Tanzania haoni tatizo jambo ambalo bado anaamini wanaweza kufanya vizuri dhidi ya Township Rollers ugenini Jumamosi.

Zahera aliahidi kuishushia Township Rollers kikosi tofauti na kilichocheza mechi hizo za kirafiki na kufafanua kwamba watacheza katika uwanja mzuri, hivyo ana imani ya kupata matokeo. "Nilichokuwa naangalia ni wachezaji kuonyesha uwezo wao, kama huwezi kunionyesha uwezo katika mechi za kirafiki utaonyesha wapi? Kupata nafasi kwenye kikosi cha Yanga mwaka huu unapaswa kuonyesha tofauti kubwa, kwa kuwa ushindani ni mkubwa," Zahera alifunguka.

Katika hatua nyingine, Yanga haikuona sababu ya kupoteza muda baada ya mechi hiyo, kwani juzi saa tisa usiku ilikwea pipa la ATCL hadi Afrika Kusini kabla ya kuunganisha ndege nyingine kuelekea Botswana tayari kwa mechi hiyo ya marudiano.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Dismas Ten, aliliambia Nipashe jana kuwa timu hiyo imeondoka na msafara wa watu 27, wakiwamo wachezaji 20 na viongozi na benchi la ufundi saba.

"Tayari timu imefika salama Afrika Kusini ikiwa na wachezaji 20 na viongozi saba, na baadaye leo (jana) mchana itaunganisha ndege nyingine kuelekea Botswana tayari kwa mechi yetu ya marudiano," alisema Ten huku akiongeza miongoni mwa wachezaji walioachwa ni pamoja na David Molinga.

Hata hivyo, jana mchana Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela aliliambia Nipashe kuwa tayari kikosi hicho kimetua salama Gaborone, Botswana kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo.

"Timu imefika salama Botswana na tumeweka kambi mjini Gaborone, leo (jana) wachezaji hawataweza kufanya mazoezi kutokana na uchovu, hivyo hadi kesho (leo) asubuhi," alisema. Yanga inahitaji ushindi wowote ama sare kuanzia ya mabao mawili ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la soka Afrika (Caf), kufuatia mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kulazimishwa sare ya bao 1-1.

## Lampard: Uchovu sababu kupata sare



**LONDON, England**

FRANK Lampard anaamini kwamba uchovu wa mchezo wa Uefa Super Cup Jumatano iliyopita ndiyo ulichangia Chelsea kucheza kwa kiwango duni katika kipindi cha pili wakati wakitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Leicester kwenye mechi ya Ligi Kuu England, juzi Jumapili.

**UK. 29**

## Guardiola azirudisha Utd, Arsenal mbio EPL



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaamini Klabu za Chelsea, Manchester United na Arsenal ndizo zenye nafasi kubwa ya kutoa changamoto ya ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu huu.

**UK. 28**

## Balotelli asajiliwa rasmi na Brescia

**ROME, Italia**

MARIO Balotelli amejiunga na timu ya nyumbani kwake Brescia kwa uhamisho huru, klabu hiyo ya Serie A imethibitisha.

Balotelli, ambaye aliachwa na Marseille mwishoni mwa msimu uliopita, amerudi nchini Italia kwa mara ya tatu, baada ya kuichezea Inter, ambako alitwaa mara tatu taji la Ligi Kuu na AC Milan.

**UK. 29**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >